# Nipashe

Jumatatu Desemba 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580108

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

ARIGATOU INTERNATIONAL | GNRC CEFA

2155447102




## Mwalimu madrasa jela miaka 10 kumdhalilisha mwanafunzi wake

UKURASA 2

# Mambo 5 ya Chadema kuelekea uchaguzi 2020

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**HOSPITALI ZAFUNGIWA KUTUMIA MASHINE ZA MIONZI ZISIZOKIDHI**

HOSPITALI 106 nchini zimefungiwa kwa mujibu wa sheria mwaka jana kwa...

UKURASA WA 4

**MVUA, DHORUBA BAHARINI VYAUA MVUVI, NG'OMBE 46**

MVUA kubwa iliyoambatana na dhoruba baharini imesababisha kifo cha mtu...


## Mshukiwa afariki dunia akitoroka askari polisi

UKURASA 3




Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## LHRC yaibua maswali mazito utata ofisa wake kukamatwa

UKURASA 2


**MICHEZO** WASHIRIKI 12 WAIBUKA KIDEDEA CHEZA KIDANSI UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mambo 5 ya Chadema kuelekea uchaguzi 2020

**Na Enock Charles**

TAKRIBANI siku nne baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kukamilisha uchaguzi wa safu ya viongozi wake wa kitaifa, sasa chama hicho kikuu cha upinzani nchini kimetoa mwelekeo wake kuelekea uchaguzi mkuu wa mwakani.

Mwelekeo huo ambao unahusisha mambo makuu matano ya msingi uliwekwa hadharani jana, jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu mpya, John Mnyika.

Mnyika alizungumza na waandishi wa habari, alitaja vipaumbele vitano katika uongozi wake katika kipindi hicho cha kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Mnyika alisema kuwa kuanzia sasa na kuendelea, chama hicho kitajikita kwenye kuhakikisha kunakuwapo tume huru ya uchaguzi.

Vipaumbele vingine ni kuandaa wagombea wa chama hicho kuelekea mwaka 2020, kuandaa ilani ya uchaguzi mkuu ujao, kuendeleza Chadema ni msingi na kuweka utaratibu wa matumizi ya Chadema digitali.

"Kutokana na yaliyotokea katika uchaguzi wa serikali za mitaa, kazi ya kwanza na kipaumbele chetu itakuwa ni kudai tume huru ya uchaguzi hadi ipatikane," alisema Mnyika, ambaye kabla ya kushika nafasi hiyo kutoka kwa mtangulizi wake, Dk. Vincent Mashinji, alikuwa Naibu Katibu Mkuu Bara.

Katibu Mkuu huyo mpya alisema chama hicho kimejipanga kudai tume hiyo kwa namna tofaut ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki nchini.

Alipoulizwa kama tume hiyo haitaundwa watatumia mkakati gani kushinda uchaguzi, alisema chama hicho kina uhakika wa kushinda kutokana na maandalizi ya wagombea na kwa kutegemea nguvu ya umma.

INAENDELEA UK. 26

## Mwalimu wa madrasa jela miaka 10 kumdhalilisha mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MWALIMU wa madrasa ya Alkhalil katika kijiji cha Afrikana shehia ya Msingini Wilaya ya Chakechake, Othman Issa Abdalla, mwenye miaka 35, amehukumiwa kifungo cha miaka 10, baada ya mahakama ya mkoa Chakechake kumtia hatiani kwa kosa la kumdhalilisha mwanafunzi wake wa kike.

Mahakama hiyo, chini ya Hakimu Lusiano Makoye Nyengo, iliridhia ushahidi uliotolewa na mashahidi wanne, akiwamo mtoto mwenyewe na daktari, ambao wote waliithibitishia mahakama hiyo, kwamba mwalimu huyo alimwingiza vidole mwanafunzi wake.

Mahakama ililezwa kuwa kitendo hicho kilimsababishia maumivu makali kwenye sehemu zake za siri mtoto huyo mwenye umri wa miaka tisa.

Wiki tatu zilizopita upande wa mashtaka uliokuwa ukiongozwa na wakili wa serikali, Juma

INAENDELEA UK. 26



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isaac Kamwele (wa tatu kulia), akimkabidhi vitendea kazi Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Prof. Iggnas Rabaratuka, wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka hiyo, Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala kutoka Wizara ya Uchukuzi, Gyeyson Mwaigombe. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## SHUKRANI



115564202

Familia ya Marehemu **J. J. Philip Tesha wa Njari Kyaurinde** - Uru Kaskazini – Moshi wanapenda kutoa shukurani zao za dhati kutoka moyoni kwa wale wote walioshirikiana nasi katika kumuuguza baba yetu mpendwa Mzee J. J. Philip Tesha hadi alipofariki siku ya Jumamosi tarehe 7 Desemba, 2019 akiwa na umri wa miaka 105 na miezi 11 na hatimaye kumpumzisha kwenye nyumba yake ya milele siku ya Alhamisi tarehe 12 Desemba, 2019.

Kwa vile ni ngumu kumshukuru kila mtu mmoja mmoja tunaomba taarfa hii itumike kuwashukuru wote waliohusika kwa namna moja au nyingine bila kuwasahau Mapadre wa parokia za Moyo Mtakatifu wa Yesu – Uru, Kristu Mfalme – Moshi, Bikira Maria Mama na Malkia – Korongoni na Mt. Yoseph Mfanyakazi –Mwenge kwa huduma za kiroho, Madaktari na Wauguzi wa Dispensari ya Uru na Hospital ya Mt. Joseph/Soweto kwa matibabu, ndugu, jamaa na marafiki waliotufariji kwa hali na mali katika kipindi hiki kigumu.

**RAHA YA MILELE UMPE EE BWANA NA MWANGA WA MILELE UMWANGAZIE APUMZIKE KWA AMANI AMINA**


# LHRC yaibua maswali kutekwa Magoti

**Na Salome Kitomari**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeibua maswali matatu kwa polisi baada ya kuthibitisha kumshikilia ofisa wake wa Kitengo cha Elimu kwa Umma, Tito Magoti, kwa siku tatu bila kujulikana kituo alichoshikiliwa kupata msaada wa kisheria na kuonana na ndugu zake.

Kupitia ukurasa wa kituo hicho, maswali yalihoji; "Tamko la polisi linauthibitishia umma kwamba wanamshikilia, lakini hawaruhusu wakili, ndugu wala mwajiri wake kumuona na kusimamia mahojiano yake kwa mujibu wa sheria na kuhoji kwanini Jeshi la Polisi linaficha."

Pia kituo kilihoji, Jeshi la Polisi linapata wapi mamlaka ya kumshikilia mtuhumiwa kwa zaidi ya saa 24 bila kumwachia kwa dhamana ya polisi au kumfikisha mahakamani.

Kadhalika kupita ukarasa huo kituo kimedai imekuwa ni tabia kwa Jeshi la Polisi kuwashikilia watuhumiwa kwa kipindi kirefu kinyume na sheria.

Ujumbe mwingine ulisomeka; "Hakuna aliye juu ya sheria wote tuko sawa mbele ya sheria. Tuungane kupinga maonevu ya Jeshi la Polisi dhidi ya raia. Hili la Tito liwe la mwisho. Inatosha."

Kituo hicho pia kimehoji: "Ni wananchi wangapi wanaonewa na Jeshi la Polisi kwa kukosa mtu wa kuwasemea? Tuseme inatosha tuchukue hatua."

Vile vile ukurasa huo ulikuwa na maneno: "Tusiruhusu tena Jeshi la Polisi kuvunja sheria na haki za binadamu bila kukemewa na kupingwa. Wakati ni sasa tuchukue hatua."

Akizungumza jana na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, alisema toka juzi alivyotekwa na watu wasiojulikana walitembelea vituo vyote vya polisi na hawakufanikiwa kumpata.

"Licha ya polisi kusema wanaye, lakini hatujafanikiwa kumuona, tumetafuta kwenye vituo vyote vya polisi wanasema hakuna mtu kama huyu, tumeongea na Kamanda wa Kanda Maalum, Lazaro Mambosasa akatuelekeza mtu wa kuwasiliana naye tumeongea naye hatupi jibu la kueleweka zaidi ya kutukwepa," alisema na kuongeza:

"Tunashindwa kuelewa kama

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA WA TANZANIA**



115564102

HII NI KWA TAARIFA KWAMBA **VINODCHANDRA RAMBHAI PATEL,** S.L.P 24, NGUDU KWIMBA

Mwenye picha hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake kwa sasa ni Uingereza. Anajishughulisha na shughuli binafsi. Anwani yake ya Posta ni S.L.P 24 Ngudu Kwimba na yupo hapa nchini toka mwaka 1948 alipozaliwa.

Kwa yeyote mwenye taarifa / sababu za kwa nini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es Salaam.

**ASI MUKUTA, O.J**
**KNY KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

## HABARI KITAIFA



Kiongozi wa Uhamasishaji Utalii wa Mapango ya Amboni, Mzee Salim Mashi (katikati), akimpa maelezo Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala (kushoto), alipotembelea mapango hayo juzi. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

# Mtuhumiwa sugu ujambazi afariki akiwatoroka polisi

**Na Hellen Magabe,** TARIME

MTUHUMIWA anayedaiwa kuiba kwa kutumia dawa ya usingizi anayopulizia watu usiku na kuingia ndani mwao, amepoteza maisha baada ya kuruka katika gari la polisi.

Akizungumza na wanahabari jana, Kamanda wa Polisi wa Tarime/Rorya, Henry Mwaibaimbe, alimtaja marehemu ni Boniface John (24) aliyekuwa mkazi wa mtaa wa Bimbwi mjini Tarime.

Alisema alifariki Jumamosi Desemba 21, saa tano wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime.

Alisema John alijaribu kuruka katika gari la polisi PT .2016 Toyota Land Cruiser, akiwa njiani kuwaonyesha mahali zilipofichwa mali za wizi.

Alisema aliruka na kuanguka chini na alijeruhiwa sehemu ya nyonga na mguuni, lakini baada ya kufikishwa hospitalini, alifariki wakati akipatiwa matibabu.

Mwaibambe alisema mtuhumiwa huyo alikuwa amebuni mbinu ya wizi kwa kuvunja nyumba usiku baada ya kuwapulizia dawa za usingizi aliowavamia, akifanya hivyo kupitia madirishani na badaye kuingia ndani na kuiba kila kitu alichotaka ikiwa ni pamoja na kuwatoa watu kwenye magodoro waliyokuwa wamelalia na kuwaweka chini.

Aidha, alisema alikuwa akitumia wizi wa silaha pamoja na ubakaji, na baada ya kuhojiwa alikitaja kikosi chake ambacho kinatafutwa.

Alisema alikuwa anatumia dawa hiyo ya usingizi aliyoitoa nchi jirani.

Wakati huo huo katika Kijiji cha Nyabirongo Mzee Chacha Kereto (76) aliuawa kwa kukatwa panga na mtoto wake Chacha Magaiwa (30).

Alisema alidaiwa kumvamia usiku

INAENDELEA UK. 8

# Hospitali zafungiwa kutumia mashine za mionzi zisizokidhi

**Daniel Sabuni,** ARUSHA

HOSPITALI 106 nchini zimefungiwa kwa mujibu wa sheria mwaka jana kwa kukutwa na mashine zinazotumia mionzi ya kuchunguza au kutibu wagonjwa, ambazo hazijakidhi matumizi salama.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC), Profesa Lazaro Busagala, alisema mwaka jana Tume hiyo ilifanya ukaguzi kwenye hospitali 664 ambazo zina mashine za kuzalisha mionzi kwa ajili ya matibabu na uchunguzi wa magonjwa na 106 zilikuwa na mashine ambazo hazikukidhi matumizi salama.

Prof. Busagala, alisema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku tano, jijini hapa juzi ya wanaradiolojia 104, yaliyohusu kuwajengea uwezo wa wakaboresha huduma kwa wagonjwa hospitalini.

Wataalamu hao wa radiolojia wanaotumia mionzi ya x-ray kuchunguza na kutibu magonjwa ya binadamu nchini.

Aliwaasa wataalamu hao kuwa wagonjwa wanaofika hospitali wahakikishe wanaondoka bila kupata madhara ya mionzi.

Alisema wataalamu waliopata mafunzo yanayofanyika kila mwaka wakahakikishe

INAENDELEA UK. 8

# Wanafunzi elimu juu wapigiwa debe nyumba za NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imezitaka taasisi za elimu ya juu kuchangamkia fursa ya uwapo wa nyumba za Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa kuwapangishia wanafunzi wanaosoma kwenye taasisi hizo.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, baada ya kutembelea miradi ya nyumba zinazojengwa na shirika hilo, Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Alisema shirika hilo limejenga nyumba nyingi ambazo zina nafasi ya kuchukuwa wanafunzi wengi kwa wakati mmoja, na kwamba ni wakati mwafaka kwa taasisi za elimu nchini kuwapangishia wanafunzi wake.

Alisema mradi wa nyumba uliopo Mtoni Kijichi ambao una nyumba 820, una uwezo wa kuchukua wanafunzi 7,020, na kuwawezesha wanafunzi kuishi mahali pazuri na penye usalama wa kutosha.

Kwa mujibu wa waziri huyo, amefurahishwa kuona Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) akitekeleza agizo la Waziri Mkuu la kutengeneza miundombinu ya barabara katika mradi wa Mtoni Kijichi.

Aidha, aliitaka menejimenti ya shirika hilo kuhakikisha kila mradi unaendana na thamani ya fedha iliyopangwa kutumiwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamani ya NSSF, Balozi Ali Siwa, alisema wataisimamia menejimenti kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa ubora na viwango vinavyostahili.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alisema watahakikisha kazi iliyobaki ya kumalizia nyumba hizo itatekelezwa kwa wakati.

Katika ziara hiyo Mhagama alitembelea mradi wa nyumba 161 zilizoko Tuangoma, 820 zilizoko Mtoni Kijichi na 439 zilizoko Dungu.

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA**

TANESCO
We light up your life

**TAARIFA KWA UMMA**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lina watangazia wateja wake wote zikiwemo Taasisi za Serikali na binafsi, Mashirika ya umma, Viwanda na watu binafsi wenye madeni ya bili za umeme kuwa;

TANESCO inaendesha zoezi maalum la kusitisha huduma ya umeme kwa wateja wote wanaodaiwa bili za umeme.

Wateja wote wenye madeni wanatakiwa kulipa bili zao haraka ili kuepuka adha ya kusitishiwa huduma ya umeme katika msimu wa sikukuu.

**TANESCO HAITATOA TAARIFA NYINGINE ZAIDI YA TANGAZO HILI.**

**Imetolewa Na:**
**OFISI YA UHUSIANO**
**TANESCO MAKAO MAKUU**
**18 Disemba2019**

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### TAREHE YA MWISHO YA MSAMAHA MAALUM WA KODI KWA MUJIBU WA AGIZO NAMBA, 282A, 2018 YA MSAMAHA WA RIBA NA ADHABU

**Dar es Salaam, 19 Desemba 2019:**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (Ijulikanayo kama"TRA" au "Mamlaka") inapenda kuwakumbusha walipakodi wote kwamba mnamo tarehe 14 Juni 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu chini ya **AGIZO Namba 282A, 2018 ya msamaha wa Riba na Adhabu** kwa walipakodi wenye malimbikizo ya madeni ya kodi na wale ambao kwa hiyari yao waliweka wazi au kuthibitisha malimbikizo ya madeni yao ya Kodi na walikuwa tayari kulipa malimbikizo hayo ya kodi ya msingi katika kipindi na masharti yaliyowekwa na AGIZO hilo.

Msamaha huo wa kodi ulibuniwa ili utekelezwe ndani ya muda maalum ukianzia **tarehe 1 Julai 2018 hadi 30 Juni 2019**. Hata hivyo, kulingana na sababu za msingi, Serikali kupitia **Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu),** (Nyongeza ya muda wa Kulipa), 2019, iliongezea muda wa malipo ya Kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Desemba 2019, kwa walipakodi ambao: -

a) Waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) Walipatiwa msamaha wa riba na adhabu;
c) Walioingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyo ainishwa katika **AGIZO Namba 282A, 2018 ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi (msamaha wa Riba na Adhabu).**
d) Walikubali kulipa Kodi ya msingi iliyokadiriwa kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) Wale ambao mpaka tarehe **30 Juni 2019,** alishindwa kulipa kwa ukamilifu, kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa.

Hivyo, walipakodi wote waliopewa msamaha wa riba na adhabu wanakumbushwa kutumia fursa hii kumalizia madeni yao ya kodi ya msingi kabla ya au **tarehe 31 Desemba 2019** kama ilivyoainishwa katika makubaliano. Izingatiwe kwamba, mlipakodi yoyote ambaye atakuwa amepewa msamaha chini ya **AGIZO namba 282A, 2018 ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu),** na akashindwa kukidhi au kutekeleza masharti ya mkataba wa makubaliano ya malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano na kudai kiasi cha kodi ya msingi kilicho salia pamoja na riba, na adhabu kama vile hakukuwa na masamaha uliotolewa.

Aidha kwa taarifa hii ya mwisho, walipakodi wote wanajulishwe kwamba, kuanzia **tarehe 1 Januari 2020,** Kamishna Mkuu atachukua hatua za kukusanya kodi dhidi ya walipakodi wote walioshindwa kuheshimu msamaha uliotolewa na kukusanya kodi stahiki, riba, na adhabu zote BILA taarifa nyingine zaidi ya hii.

**Kwa taarifa hii, tekeleza kama ilivyoelekezwa.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa letu"**

**Msafiri Mbibo.**
**KAIMU KAMISHNA MKUU**

# Mvua, dhoruba baharini vyaua mvuvi, ng'ombe 46

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

MVUA kubwa iliyoambatana na dhoruba baharini imesababisha kifo cha mtu mmoja, ng'ombe 46 huku nyumba kadhaa zikijaa maji na madaraja kubomoka katika maeneo mbalimbali kisiwani Pemba.

Aliyepoteza maisha katika maafa hayo ni mvuvi kijana ambaye hajafahamika aliyezama baharini kufutia mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali na mawimbi makubwa ya kupindua chombo alichokuwa anavulia baharini, madhara yaliyotokea usiku wa kuamkia jana kisiwani Pemba.

Mkuu wa Wilaya Mkoani, Isajuma Ali, alisema kijana aliyepotea aliondoka na wenzake wawili kwenda baharini kuvua, lakini mvua iliyoambatana na upepo iliwapindua boti yao na wavuvi wawili walifanikiwa kujiokoa lakini mmoja hadi sasa hajulikani alipo.

Alisema kutokana na mvua kubwa na mawimbi kuchafuka bahari Kikosi cha KMKM kilishindwa kumtafuta.

Mkuu wa Wilaya alisema wananchi katika wilaya hiyo wameripoti kuwa zaidi ya ng'ombe 46 wamekufa kutokana na mvua hiyo, huku wengine wakisombwa na maji kutokana na mvua kubwa kunyesha ghafla nyakati za usiku wakati mifugo hiyo ikiwa imefungwa mabondeni.

Alisema maeneo ambayo ng'ombe wengi wamepotea ni katika Kijiji cha Mkungu Kengeja ambapo 18 walikufa na Mahudusi walikufa 15.

Mkuu wa Wilaya Chakechake, Rashid Hadidi Rashid, alisema maeneo mengi ya wilaya yake yameathiriwa na mvua hiyo kwani baadhi ya nyumba zimejaa maji huku miundombinu ya barabara ikitatizwa.

Alisema baadhi ya madaraja yamejaa maji na kwa kiasi kwa huduma za usafiri kusimama.

Alieleza kuwa miongoni mwa athari hizo ni pamoja na kushindwa kupitika na wananchi wa Pondeani kukosa usafiri huku nyumba kadhaa zilizozingirwa na maji watu wakikosa makazi.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Ahmed Muhamed Baucha, alisema miundombinu ya barabara katika maeneo kadhaa iliharibiwa ikiwamo barabara inayojengwa ya Kinga Kengeja ila kwa sasa hali imeanza kutengemaa.

Baadhi ya wananchi walioathirika na mvua hizo walisema imetokea ghafla nyakati za usiku wakiwa wamelala saa 7:00 usiku.

# Waziri awatangazia kibano wadaiwa NHC

**Na Munir Shemweta**



NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, (pichani) amekutana na menejimenti ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa saa nne na kulitaka shirika hilo kuhakikisha kufikia Januari 2020, inawachukulia hatua wapangaji wote wanaodaiwa kodi inayofikia Sh. bilioni 8.23.

Mabula alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam ikiwa ni mkakati wake wa kulifanya shirika hilo kuimarika kimapato pamoja na kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Alisema, katika kuifanya NHC inaimarika kimapato ni lazima madeni kutoka kwa wapangaji wake yanakusanywa kwa kuanzisha opreresheni maalum inatakayowezesha kutambuliwa wadaiwa wote wa kodi ili waweze kulipa kwa wakati.

"Ukiacha zile taasisi za serikali, wote wanaodaiwa ikifika Januari 2020 wafikishwe kwenye vyombo vya sheria na zile taasisi za serikali mkamwone Katibu Mkuu Hazina ili taasisi hizo zikatwe fedha moja kwa moja," alisema Mabula.

Kwa mujibu wa Mabula, wakati wa zoezi la kufanya operesheni ya kukusanya madeni sheria lazima ifuatwe ikiwamo kutoa hati za wito wa madai kwa wadaiwa wote kabla ya hatua nyingine kuchukuliwa.

Mkurugenzi wa Umiliki na Uendelezaji wa NHC, Greyson Godfrey, alimweleza Mabula kuwa pamoja na shirika kuimarika katika makusanyo, lakini liko kwenye mkakati maalum wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa wake na moja ya jitihada zake ni kuingia makubaliano maalum ya namna wadaiwa watakakavyolipa madeni.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Dk. Maulid Banyani, alisema shirika lake limekuwa na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha linaimarika kimapato ikiwamo kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya vizuri katika mikoa itakayofikia lengo la makusanyo na kutokuwa na malimbikizo ya madeni kutoka kwa wadaiwa wa kodi.

"Tumekuwa tukitoa motisha kwa watumishi wanaofanya vizuri na sasa tunaangalia ile mikoa ambayo haina malimbikizo ya madeni kwa wapangaji wake kwa asilimia mia moja tuone namna tutakavyotoa motisha ili kuhamasisha mikoa kutokuwa na madeni," alisema Dk. Banyani.

Aidha, Dk. Banyani alisema, kwa sasa NHC imeanza kufanya uhakiki kwa wapangaji wake ili kubaini wapangaji waliopangisha watu wengine ambapo eneo la Ubungo limetumika kama eneo la majaribio na tayari wapangaji sita washaondolewa na kusisitiza kuwa zoezi hilo litakuwa ni la nchi nzima.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Mabula aliagiza kupatiwa orodha ya nyumba zote za NHC zilizouzwa, zisizouzwa, zilizopangishwa na zisizopangishwa, viwanja vya shirika hilo visivyoendelezwa pamoja na nyumba zilizokuwa za msajili wa majumba zilizohamishiwa NHC ili kujua hali ya shirika na mkakati wake katika kuleta ufanisi.

Pia Mabula alitembelea maendeleo ya ujenzi wa machinjio ya Vingunguti na kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi huo ambao uko katika hatua za mwisho za kukamilika.

TANGAZO


M-Pesa, familia imezidi kukua!
Wateja Milioni
10
Asanteni wateja wetu
Tunawatakia heri ya krismas na mwaka mpya
Yajayo yanafurahisha.
Uko tayari?
vodacom
m-pesa

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko Katiba TFF yachochee maendeleo

**MKUTANO** Mkuu wa mwaka wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), umefanyika mwishoni mwa wiki na moja ya ajenda ya mkutano huo ilikuwa ni kubadilisha baadhi ya vipengele vya katiba ya shirikisho hilo ambavyo vilipita kwa asilimia 100.

Mabadiliko hayo yamefanyika kwa kufuata mwongozo kutoka Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) pamoja na la Afrika (Caf), kama ambavyo vyama vingine vya soka barani Afrika vilivyotekeleza maelekezo kutoka kwa wasimamizi hao wa ngazi za juu kabisa kwenye mchezo wa kandanda Afrika na duniani. Katiba ndio msingi wa kila jambo, hivyo hili limepita na kilichobakia ni kutekeleza matakwa yaliyomo kwenye katiba hiyo mpya ambayo kiuhalisia yatakwenda hadi kwenye ngazi za mikoa.

Hata hivyo, kipengele ambacho kilionekana kuleta mjadala mkubwa miongoni mwa wajumbe wa mkutano huo mkuu ni idadi ya wapiga kura kupungua, hasa kukizingatiwa kuwa awali kila mkoa uliwakilishwa na wajumbe wanne, lakini katiba mpya inasema wapigakura sasa watakuwa wawili kutoka kila mkoa.

Kipengele hiki kimesumbua na kuleta changamoto kwa wajumbe, lakini mwisho wa siku ibara hiyo ilibadilishwa na hatimaye sasa mkutano mkuu wa TFF utakuwa unahudhuriwa na wajumbe 87 badala ya awali ambao walikuwa ni zaidi ya 137. Baada ya wajumbe kupitisha katiba mpya na kusajiliwa, viongozi wapya watakaoingia katika mkutano mkuu watakuwa ni wenyeviti wa mikoa na wajumbe wa mkutano mkuu, huku ikielezwa kwa “mdomo” kuwa siku za usoni, makatibu ambao sasa watakuwa wasimamizi wa vituo, wataajiriwa ili kufanya watumie muda mwingi kufanya kazi za maendeleo ya soka mikoani mwao.

Nipashe inaamini kuwa mabadiliko yoyote yanayofanywa na Fifa, Caf na TFF yanalenga kuimarisha na kuukuza mchezo wa soka ambao unapendwa na mashabiki wengi zaidi duniani, hivyo wadau wote wanapaswa kuhakikisha hakuna kinachokwamisha katika kufikia maendeleo.

Hatuamini hata siku moja viongozi wakuu watakubali kufanya mabadiliko ambayo yatarudisha nyuma maendeleo ya soka na hivyo kuondoa ushindani na burudani ambavyo mashabiki wake husubiri kila wanapokuwa viwanjani au mbele ya televisheni (nyumbani au vibanda umiza).

Tunashauri kuwa katiba imeshapitishwa hivyo kinachohitajika ni utekelezaji sasa, na pia ni wakati wa kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia malengo ya mikoa yote ya hapa nchini na kwa kufanya hivyo, TFF itakuwa na kazi nyepesi ya kuunganisha nguvu za wanachama. Lengo letu ni kuona soka linapiga hatua kutoka hapa tulipo kwa klabu zetu kutisha katika michuano ya kimataifa jambo ambalo litasaidia wachezaji wanapoitwa timu za taifa kuwa msaada mkubwa na hatimaye kuweza kuiletea nchi yetu sifa kwa kutwaa mataji, na hilo litawezekana tu kama mabadiliko haya yatafuatwa bila kupepesa macho.

Itakuwa ni jambo la kushangaza kama viongozi wa mikoa wataacha kuangalia majukumu yao ya msingi ya kuendeleza soka ili klabu na timu zao za mikoa ziweze kufanya vema katika mashindano mbalimbali, hatimaye kuwa msaada kwa timu za taifa, na badala yake kuhamishia nguvu kwenye kuwania nafasi za uchaguzi pekee.

Tunawakumbusha kuwa huu ni wakati wa kuweka mbele maslahi ya soka na kusahau maslahi binafsi ambayo kama wadau watayapa kipaumbele, mikoa na baadhi ya klabu zitaendelea kuwa wasindikizaji kwenye mashindano mbalimbali wanayoshiriki ndani na nje ya Tanzania.

Kama mataifa mengine yamekubali kufanya mabadiliko haya, Tanzania pia tunatakiwa tuchukulie kuwa ni jambo la kawaida kwa sababu tunaamini hakuna suala ambalo litapitishwa na lisiwe na malengo ya kuleta mafanikio.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Karia na mzigo mzito Cecafa kuliko wa TFF

Na Adam Fungamwango

**TANZANIA** imepata bahati nyingine kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, baada ya Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Nichukue fursa hii kumpongeza Karia na Watanzania wote kwa dhamana hii ya miaka minne.

Ninatambua kama Karia ni kiongozi ambaye tangu aanze kuiongoza (TFF), soka la Tanzania siyo kama limekua sana, lakini limeonekana kuanza kutoka shimoni na kuelekea ambako Wabongo walikuwa wanataka lielekee.

Kwa maana hiyo huenda kile alichokileta TFF au bahati aliyokuwa nayo tangu atue huko, inaweza pia kuifanya Cecafa nayo kuinuka.

Kwa sasa Cecafa iko hoi bintaaban. Ni shirikisho kongwe kabisa Afrika, lakini kwa sasa linapitwa hadi na Cosafa ambalo lilikuja kwenye miaka ya karibuni, nchi za Kusini mwa Afrika zote zilipopata uhuru, sasa zinainyang'anya Cecafa baadhi ya wanachama wake, nchi za Malawi, Zimbabwe na Zambia ambazo zilikuwa zinacheza michuano ya Afrika Mashariki na Kati (sasa Kombe la Kagame) na Kombe la Chalenji, wakati huo ikiwa na msisimko wa aina yake.

Pamoja na kwamba kuna baadhi ya watu wamekuwa wakimsema sana Katibu Mkuu, Nicolaus Musonye kuwa ni mmoja wa watu ambao wamesababisha Cecafa kudumaa, lakini pia akikaa madarakani kwa zaidi ya miaka 25, binafsi pamoja na mapungufu aliyokuwa nayo, nampongeza kutokana na uvumilivu alionao, kiasi cha kuifikisha hata hapa ilipo.

Tatizo la Cecafa wala si Musonye, bali kuna matatizo mengi mtambuka ambayo yakifanyiwa kazi yanaweza kurekebishika.

Utawala wa Musonye, hadi anatangaza kuondoka mwakani, bado anaiachia Cecafa ikiwa na mdhamini ambaye anatoa zawadi kwa mshindi wa kwanza, wa pili na wa tatu kwa miaka mingi sasa. Naye ni Rais wa Rwanda, Paul Kagame.

Ni wajibu wa Karia na safu mpya ya uongozi kukaa na Rais huyo, kumwomba aendelee na udhamini wake ambao ndiyo unaofanya michuano hiyo iendelee kuwapo, ikiwezekana hata kama kuna kidogo cha kuongeza basi aongeze, na Musonye ataendelea kukumbukwa kwa hilo.

Pia Karia anatakiwa alete vitu vingine vipya ambavyo vitafanya michuano hiyo kuwa bora zaidi kama vile mfumo mpya, pamoja na wadhamini.

Sidhani kama kitengo cha masoko kikifanya kazi yake sawa sawa kwenye nchi zote za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kinaweza kukosa wadhamini walau watatu au wanne ili kuboresha michuano hiyo.

Pia mfumo wa Kombe la Kagame na Chalenji uangaliwe upya kuanzia kipindi cha ratiba, kutoka kuwa ya kituo kimoja hadi kuwa ya nyumbani na ugenini.

Karia aangalie kuwapo na uwezekano wa kuchezwa kwa hatua ya mtoano nyumbani na ugenini na kubakisha timu nane ambazo zinapangwa makundi mawili ambazo nazo zicheze kwa mtindo wa nyumbani na ugenini kutafuta timu mbili za juu zitakazokwenda kucheza nusu fainali na fainali.

Na ratiba ya michuano hii iwe kwenye muda wa Kalenda ya Fifa, klabu zinapokuwa kwenye mapumziko kupisha mechi za kimataifa. Hajalishi hata kama ikiwa ni kwa mwaka mzima, lakini unapopatikana mwanya wa tarehe za Fifa, basi mechi zichezwe.

Haya ni baadhi tu ya mambo ambayo Karia anatakiwa ayaangalie kwa macho mawili ili kuitoa Cecafa hapa ilipo na kuipeleka mbele badala ya kuendelea kuiendesha kwa kukariri. Hongera Karia, lakini Cecafa ni mzigo mzito zaidi ya TFF, kwa sababu inahitaji mabadiliko makubwa.

## TANGAZO

FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
Facilitating Partnerships for Development

# WITO WA MAOMBI YA RUZUKU KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KUIMARISHA USHIRIKI WA WATU WENYE ULEMAVU KWENYE UCHAGUZI MKUU MWAKA 2020

**Utangulizi**
Foundation for Civil Society (FCS) ni Shirika lisilo la Kiserikali lililoanishwa mwaka 2020 ambalo hutoa ruzuku na huduma za kuzijengea uwezo Asasi za Kiraia za Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake FCS imechangia kwa kiwango kikubwa katika kuimarisha uwezo wa sekta ya kiraia nchini Tanzania. Kwa namna moja ama nyingine imeziwezesha asasi za kiraia kuwa na mchango unaoleta chachu ya maendeleo na kuhakikisha uwepo wa utoaji wa huduma bora zaidi, hasa katika ngazi za chini za jamii. FCS kupitia kazi za Asasi za Kiraia imeweza kuchangia uwepo wa hali bora ya maisha kwa Watanzania wengi ikiwemo makundi maalum kama wanawake, watoto na watu wenye ulemavu. Iwapo utapenda kupata taarifa zaidi kuhusu FCS, tembelea tovuti yetu: **www.thefoundation.or.tz.**

**Malengo mahususi ya Ruzuku, Wahusika na Miradi itakayofadhiliwa**
Tangu kuanzishwa kwake FCS imekua ikiwezesha asasi za watu wenye ulemavu kwa kutoa ruzuku ili kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika jamii. Kadhalika FCS imewezesha kujenga uwezo wa kiutendaji kwa mashirika ya watu wenye ulemavu. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata fursa na nafasi stahiki katika jamii ikiwa ni pamoja na kupata huduma bora za kijamii, kushiriki na kushirikishwa katika uongozi, michakato mbalimbali ya kimaendeleo na kidemokrasia kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Watu wenye Ulemavu Namba 9 ya 2010 na Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu (UNCRPD) wa mwaka 2006.

Hata hivyo, pamoja na juhudi nyingi zinafanywa na Serikali na pamoja na Wadau wengine wa maendeleo zikiwemo Asasi za Kiraia katika kuboresha ustawi na maisha ya Watu wenye Ulemavu, kundi hili bado linakumbana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni unyanyapaa kuanzia kwenye ngazi ya familia hadi jamii juu ya ulemavu. Hali hiyo hupelekea Watu wenye Ulemavu kukosa fursa ya kushiriki ama kushirikishwa kikamilifu kwenye michakato ya kimaendeleo na kidemokrasia na hivyo kukosa nafasi ya kushiriki moja kwa moja kwenye vyombo vya maamuzi.

Tukitambua kuwa Tanzania inatarajia kufanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2020, FCS inatoa fursa ya ruzuku kwa Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu pekee ili kuimarisha ushiriki wao katika uchaguzi huo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa malengo na mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu yanapewa kipaumbele.

**Aina za miradi inayolengwa katika wito huu.**
FCS itatoa ruzuku kwa Mashirika, Taasisi na Vyama vya Watu wenye Ulemavu ambavyo watawasilisha maandiko ya miradi itayoweza kueleza kiundani na kiubunifu ni kwa namna gani wataweza kufanikisha moja wapo kati ya matokeo tajwa hapo chini. Tunaweka msisitizo katika kufikia matokeo tarajiwa kwa kutumia mbinu shirikishi, bunifu na za kiufanisi.

**MATOKEO 1:** Ilani za Uchaguzi za Vyama vya Siasa zimetilia mkazo na kuweka kipaumbele mahitaji ya watu wenye ulemavu.
**MATOKEO 2:** Zoezi la kupitisha Wagombea katika Uchaguzi Mkuu 2020 ndani ya Vyama vya Siasa linazingatia uhusishwaji na ushiriki wa watu wenye ulemavu.
**MATOKEO 3:** Mamlaka za Uchaguzi ikiwemo Tume ya Taifa ya Uchaguzi zinaweka mazingira wezeshi na rafiki kwa Watu wenye Ulamavu kushiriki katika Uchaguzi Mkuu 2020.

**Walengwa**
Walengwa katika Rukuzu hii ni **Mashirika, Taasisi na Vyama vya Watu wenye Ulemavu. Taasisi hizo pia ziwe zinaendeshwa na Watu wenye Ulemavu wenyewe (Disabled People Organizations)** na ambazo hazifungamani na Vyama vya Siasa kutoka mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani.

**Vigezo vitakavyozingatiwa katika kuidhinisha miradi**
Kigezo kikuu kitakachozingatiwa katika kuidhinisha na kuuthibitisha mradi wowote ili kupata ruzuku kutoka FCS ni baada ya kujiridhisha kwamba shughuli za mradi husika zinadhihirisha pasipo shaka kuwa zitawanufaisha (moja kwa moja) walengwa wa maombi haya kama ilivyobainishwa katika Malengo Makuu ya wito huu.
Vigezo vingine mahsusi ambavyo vitazingatiwa katika uidhinishaji wa mradi ni;

- Ni kwa jinsi gani shughuli zilizopangwa, matokeo tarajiwa pamoja na mbinu pendekezwa katika andiko la mradi zinaendana na malengo makuu ya programu kama ilivyoelezwa kwenye tangazo.
- Uwezo na ubunifu wa miradi yenye kuleta tija kwa gharama nafuu.
- Nafasi ya jamii na ushirikishwaji - kiwango cha uhusishwaji wa jamii katika kutekeleza miradi inayowahusu na kwa jinsi gani mradi utaweza kuinufaisha jamii hadi katika ngazi ya chini kabisa kwa uthibitisho wa takwimu na ushahidi.
- Historia ya Taasisi, uwezo wa wafanyakazi wake na sifa zao katika kutekeleza miradi na matumizi ya Fedha hususani kuzuia Ubadhirifu
- Jinsi na namna ambavyo mradi husika utahusisha Taasisi na Mamlaka husika za Serikali katika utekelezaji ili kuleta uendelevu wa mradi.
- Uwepo wa nyaraka zote za muhimu zinazohitajika katika fomu ya maombi, zikiwemo fomu ya bao mantiki, mpango kazi, na bajeti, zinazopatikana kwenye tovuti ya Foundation.

**Taasisi na shughuli ZISIZOLENGWA kupata ruzuku.**

FCS itatoa ruzuku kwa Taasisi ambazo zimesajiliwa, kufanya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na ambazo hazizalishi faida. Kama maelezo na ufafanuzi zaidi vitahitajika juu ya kigezo hiki, basi wasiliana na FCS kabla haujafanya maombi yako ya ruzuku.

**FCS haitatoa ruzuku kwa:**

| | |
|---|---|
| • Udhamini na ufadhili<br>• Miradi au shughuli zitakazo fanyika nje ya Tanzania<br>• Miradi au shughuli ambazo zimeshawahi kufanyika na kukamilika.<br>• Miradi ambayo imekwisha wezeshwa ruzuku na mashirika mengine.<br>• Kutumika kama Malipo ya ziada kwa wafanyakazi wanaolipwa na taasisi husika<br>• Kipato cha mtaji kwa taasisi ndogondogo za fedha<br>• Maombi toka kwa wataalamu wa ushauri au watunisha mifuko kwa niaba ya taasisi. | • Watu binafsi<br>• Vyama vya siasa<br>• Miradi ambayo inalenga kuinufaisha dini/dhehebu fulani, kabila fulani au kikundi fulani chenye mlengo wa kikabila.<br>• Sekta binafsi (isipokuwa kama haipo kwa ajili ya manufaa ya kuzalisha faida)<br>• Taasisi zenye madeni<br>• Waendesha Semina, warsha, na mikutano tu, isipokuwa kama ni sehemu ya shughuli zilizounganishwa na tokeo mahususi.<br>• Gharama kubwa zisizo tarajiwa (dharura) |

**ANGALIZO KWA WAOMBAJI WOTE**
Foundation for Civil Society, ni asasi ya kiraia inayojitegemea kimamlaka. Tunayo sera ya kuendesha shughuli zetu zote kwa uaminifu, kimaadili na uwazi. Katu hatuvumilii hongo, rushwa wala aina yoyote ya ubadhirifu. Tumejitoa kuendesha mambo yetu kitaalamu, kwa haki, na uadilifu katika shughuli zetu na mahusiano yetu yote. Katika mchakato mzima wa kutoa ruzuku, FCS haitozi ada, wala kuomba fedha ama kupiga simu kwa wadau kwa minajili ya kuwasaidia ili wapitishwe kwenye ruzuku.

Hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa wapo matapeli wanaojifanya kuwa wanaweza kuwasaidia. Tunawaalika wadau wote, iwapo unazo taarifa za uhakika zinazoashiria vitendo vya rushwa ama ubadhirifu katika mchakato huu au pia kwamba unaifahamu moja ya Taasisi iliyotuma maombi FCS na unajua kuwa wanachangamoto ya masuala ya rushwa ama ubadhirifu wa aina yoyote kama vile matumizi mabaya ya fedha za miradi, ikiwa ni pamoja na fedha za wafadhili wengine tafadhali usisite kutuandikia ili hatua stahiki zichukuliwe. Tafadhali zingatia njia sahihi za mawasilino kama inavyooneshwa hapa chini.

a. Kwa mawasilino ya kawaida na maulizo (Inquiries) tafadhali wasiliana nasi kwa kupiga simu kupitia nambari **+255 22 266 4890-2,** simu ya mkononi **+255 754 005708** au barua pepe: **information@thefoundation-tz.org.** Zingatia pia kuwa Maafisa wote na wafanyakazi wa FCS wanatumia barua pepe inayoishia na **@thefoundation-tz.org** na si vinginevyo iwapo una mashaka tafahdali usisiste kuwasiliana nasi kwa ufafanuzi na uhakika.
b. Kwa mawasiliano yote yanayohusu Rushwa, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za rushwa ama ubadhirifu tafadhali tuandikie kwenye barua pepe: whistleblower@thefoundation-tz.org. Taarifa zote zitakazotumwa kwenye narua pepe hii ni za siri na zitafanyiwa kazi kwa weledi na bila upendeleo. Kadhalika FCS inayo sera ya kulinda watoa taarifa.

**Kiwango cha Ruzuku kitakachotolewa na muda wa Utekelezaji**
FCS itatoa kiasi cha takriban **TZS 20,000,000** kwa kila taasisi kwa ajili ya kutekeleza mradi. Kwa kuzingatia kuwa ruzuku hizi ni ndogo tunatarajia kuwa waombaji watakuwa na shughuli za kimkakati zaidi ili kufikia malengo. Muda wa utekelezaji wa mradi utakuwa ni **(Machi – Novemba 2020)**

**Utaratibu wa Uombaji**
Mashirika, Taasisi na Vyama vya Watu wenye Ulemavu vinavyokidhi vigezi wanaalikwa kuomba ruzuku kwa kufuata utaratibu ufuatao.

a. Taasisi ijipime ni eneo gani kati ya matokeo 3 inauwezo zaidi wa kiutekelezaji na kuleta matokeo tarajiwa. Taasisi haitakiwi kuomba eneo zaidi ya moja la matokeo yaliyoainishwa.
b. Chagua moja kati ya Matokeo Tajwa hapo juu (Mfano Matokeo 1)
c. Jaza fomu mahususi inayopatikana katika tovuti ya Foundation for Civil Society www.thefoundation.or.tz
d. Weka viambatisho vyote muhimu (Orodha ya mambo yote muhimu imeambatanishwa katika fomu ya maombi)
e. Wasilisha maombi yako (Nakala 2) kwenda kwenye anuani iliyoambanishwa hapo chini (Unaweza kuleta kwa mkono katika Ofisi ya FCS ama kutuma kwa njia ya EMS/Rejesta) kwenda:

**Kwa Mkurugenzi Mtendaji**
**Foundation for Civil Society**
**7 Madai Crescent, Ada Estate Plot Na. 154**
**S.L.B 7192**
**Dar es Salaam**
**Simu ya mezani +255 22 266 4890-2**
**Simu ya mkononi +255 754 005708**
**Tovuti: www.thefoundation.or.tz**

FCS haitapokea wala kufanyia kazi maombi yoyote yaliyoletwa kwa njia ya kieletroniki kama vile kupitia barua pepe.

215564902

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### MAWASILIANO YA KIKODI BAINA YA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA NA WAWAKILISHI WA WALIPAKODI

**Dar es Salaam, Desemba 20, 2019**

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inatambua na kuthamini umuhimu wa mawasiliano, kwa njia ya majadiliano, yanayohusu masuala ya kikodi baina ya Mamlaka yenyewe na walipakodi wetu. Kimsingi, majadiliano haya ni moja ya nguzo za kutusaidia TRA katika kutekeleza kwa ufanisi jukumu letu la kukadiria, kukusanya, na kuhasibu kodi ya Serikali. Pia, kupitia majadiliano haya, walipakodi hupata fursa ya kupata uelewa mkubwa ili kuwasaidia kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

Vile vile, tunapenda kuwataarifu walipakodi na wananchi kwa ujumla kuwa, kwa mujibu wa **Kifungu cha 27(1)(a) cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015,** mlipakodi ana haki ya kuwakilishwa na mwakilishi atakayemteua kwa ajili ya majadiliano baina ya TRA na mlipakodi husika. Hata hivyo, kwa kuwa taarifa za mlipakodi ni siri baina ya mlipakodi na TRA (kama ilivyoelekezwa katika **Kifungu cha 21 cha Sheria tajwa),** uwakilishi wowote tofauti na mlipakodi mwenyewe ni sharti uzingatie matakwa ya **Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria** tajwa ambapo ni lazima mlipakodi amtaarifu, kwa maandishi, Kamishna Mkuu wa TRA kuhusu uwakilishi huo. Ikumbukwe kwamba, mtu yeyote ambaye ama si Mmiliki au Mkurugenzi wa kampuni (mlipakodi), hana uhalali wa kumwakilisha mlipakodi iwapo hana Hati ya Uwakilishi (Power of Attorney), kutoka kwa mlipakodi, ambayo itawasilishwa TRA baada ya kufuata taratibu zote za kisheria, ikiwa ni pamoja na kusajiliwa na Msajili wa Hati (Registrar of Documents).

Aidha, wawakilishi Wataalam, kama vile Mawakili (Advocates), wanaweza kuwawakilisha walipakodi kama wateja wao endapo watateuliwa rasmi na wateja hao na uteuzi wao kutaarifiwa kwa Kamishna Mkuu kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria tajwa kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Kwa upande wa wawakilishi ambao ni Wataalam Elekezi wa Kodi **(Tax Consultants),** kama Kifungu cha 28 cha Sheria tajwa kinavyotambua uwepo wao, ni lazima wawe wamesajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi za mwaka 2016.

Kwa upande wa masuala ya forodha yanayosimamiwa na TRA kupitia Idara yake ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa, **Kifungu cha 6 cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015** kinampa Kamishna Mkuu mamlaka ya kutumia vifungu vya Sheria hiyo kwenye masuala ya forodha endapo matumizi ya Sheria hiyo hayakinzani na utaratibu uliowekwa na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Hivyo, Mawakala wa Forodha (waliosajiliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 145 na kwa kuzingatia matakwa ya **Kifungu Na. 146, 147 na 148 cha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004),** Mawakili, na Wawakilishi wowote watatambuliwa rasmi kama wawakilishi wa walipakodi iwapo taarifa za uteuzi wao zitawasilishwa kwa Kamishna wa Forodha. Aidha, tunaomba ieleweke kwamba kitambulisho cha mfanyakazi (Identity Card) au sare ya kazi sio kibali cha uwakilishi halali kwa mujibu wa Sheria.

Hivyo, natoa wito kwa walipakodi na wananchi kuzingatia ufafanuzi huu kwa lengo la kuwa na majadiliano baina ya TRA na walipakodi yanayotambulika kisheria. Tunaomba ieleweke kwamba ushiriki wa watu ambao si wawakilishi halali wa walipakodi, sio tu ni uvunjifu wa matakwa ya **Kifungu cha 21 cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015,** kwa upande mmoja, lakini pia, kwa upande mwingine, husababisha majadiliano mengi yasiyo na tija na ambayo ama huwa hayafikii muafaka au hufikia muafaka usiokubalika kisheria na walipakodi husika wanapopelekewa maamuzi ya kikodi.

**Tunatanguliza shukrani kwa ushirikiano.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Msafiri Mbibo.**
**KAIMU KAMISHNA MKUU**

# Hospitali zafungiwa kutumia mashine za mionzi zisizokidhi

**INATOKA UK. 3**

wagonjwa wanaofika katika hospitali zao kwa uchunguzi wa magonjwa mbalimbali na matibabu waondoke wakiwa wamepata suluhisho la magonjwa yao badala ya kuondoka na madhara yanayosababishwa na uzembe au ubovu wa mashine zinazozalisha mionzi.

"Mgonjwa anaweza kufika hospitali kuchunguzwa afya au matibabu yanayotolewa kama ya saratani, sasa badala ya kuondoka akiwa ametibiwa anaweza kupachikwa magonjwa mengine kufuatia uzembe, kama mashine ya mionzi haikaguliwi inaweza kutoa kiasi kikubwa cha mionzi na kumdhuru mgonjwa, tuepuke haya na ndio maana tunafanya mafunzo ya wataalamu kote nchini kila mwaka," alisema.

Alisema kadiri teknolojia inavyoongezeka wataalamu wanatakiwa kuwa makini kuhakikisha afya ya binadamu inakuwa salama na kama kuna changamoto TAEC itaitatua na hata ikilazimu msaada kutoka kwa wataalamu kutoka Ulaya.

Vile vile, Profesa Busagala alisema waradiolojia ni kiungo muhimu kati ya TAEC na maeneo wanayofanyia kazi hivyo ushirikiano unahitajika zaidi ili kuboresha ustawi wa uchunguzi na utoaji wa huduma ya mionzi. "Tunasisitiza kuwa usalama dhidi ya mionzi uko mikononi mwa TAEC na watoa huduma wa radiolojia, hivyo sheria, kanuni, taratibu na weledi vitumike ili wagonjwa wanaopofika kwenye vituo vya afya kupata huduma ya mionzi warudi nyumbani kwao wakiwa salama na sio kurudi wakiwa wamepata magonjwa yaliyosababishwa na mionzi," alisema.

Alisema wataalamu hao waliomaliza mafunzo na kupata cheti warejee kazini wakiwa wapya katika eneo hilo la mionzi na kuwa na uelewa mpana katika maeneo ya utumiaji salama wa mionzi, kuongeza utii wa sheria na kanuni zinazosimamia matumizi salama ya mionzi sehemu za kazi, kutumia kwa usahihi vifaa vinavyotoa mionzi katika uchunguzi na tiba ya mgonjwa kujikinga na kudhibiti na madhara yatokanayo na mionzi.

Naye mtaalamu wa radiolojia kutoka Hospitali ya Mkoa wa Pwani ambaye pia ni Katibu wa wataalamu wa mionzi wa mikoa ya Tanzania Bara, Faustine Mulyutu, kwa niaba ya washiriki aliitaka TAEC kuwakutanisha katika mafunzo ya pamoja kati ya wataalamu wa radiolojia na waganga wakuu ili kuepusha migongano inayotokea mara kwa mara.

"Kuna wakati mwingine wataalamu wanashauri masuala muhimu ya kuboresha mashine za kuzalisha mionzi kama ununuzi wa vipuri au ushauri, kutokana na kukosa uelewa utekelezaji unashindikana, tukipata mafunzo haya pamoja tutazungumza lugha moja kwa maana ya maboresho na usalama wa utoaji wa huduma kwa ujumla, nina hakika mambo yataenda vizuri ombi letu likitekelezwa," alisema.

Alishauri wataalamu wa radiolojia wapewe barua na waajiri za kuwatambulisha kama wahusika na wataalamu sahihi wa mionzi ombi ambalo Mkurugenzi Profesa Busagala aliliafiki na kusema hilo litakuwa moja ya vigezo katika ukaguzi wa stahiki za mitambo ya kuzalisha mionzi.

# Mtuhumiwa sugu ujambazi afariki akiwatoroka polisi

**INATOKA UK. 3**

akiwa amelala na chanzo ni ugonvi wa kifamilia ambao kijana huyo alikuwa akitaka baba yake amgawie ng'ombe na mashamba.

Mtuhumiwa huyo amekamatwa na polisi akisubiri kufunguliwa kesi ya mauaji.

Aidha, katika tukio jingine la Desemba 20, wilayani Rorya, mkazi wa Kijiji cha Mkoma, Mbirinya Mayama (24) ambaye ni mkulima alikatwa panga kwenye bega la kushoto na Ocheng'i Gibore (38).

Mwaibabe alisema kisa cha mashambulizi hayo kimedaiwa kuwa ni mgogoro wa aridhi.

Kamanda Mwaibabe aliwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari za kiusalama wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa kujiepusha na uhalifu ikiwa ni pamoja kuacha nyumba bila ulinzi na ulevi kupindukia.

Aliwataka wazazi kutowaruhusu watoto wao kuzagaa barabarani ili kuepuka ajali zinazoepukika na hata kufanyiwa vitendo vya ubakaji na kuongeza kuwa wazazi na walezi waandame na watoto wao kwenye kumbi za watoto na si kuwaacha waende peke yao.

Aidha, amewataka madereva kujiepusha na ulevi pamoja na mwendo kasi ili kuepusha ajali na maafa mengine.

# LHRC yaibua maswali kutekwa Magoti

**INATOKA UK. 2**

wamemkamata wao tangu siku hiyo, lakini hawaruhusu mtu yeyote kumuona wala kupata msaada wa kisheria hii si sawa kabisa, tunajipanga zaidi kuchukua hatua kubwa na leo asubuhi tutatoa tamko."

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum, Mambosasa, alisema taarifa ya tukio hilo itatolewa leo (kesho) kwa waandishi wa habari na kuwataka kutokuwa na haraka.

Katika ukurasa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), waliandika kuwa wamemtafuta Magoti kwenye vituo vyote bila mafanikio na walikwenda kituo kikuu cha polisi na kuangalia jina lake mara mbili kwenye kitabu cha wanaoshikiliwa na polisi, lakini hawakuona jina lake.

Naye Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema watetezi wa haki za binadamu wamekutana kujadili suala hilo na kwamba watachukua hatua baada ya kumtafuta kwenye vituo vyote jijini Dar es Salaam bila mafanikio.

TANGAZO

FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
*Facilitating Partnerships for Development*

# WITO WA MAOMBI YA RUZUKU KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ZANZIBAR KWA MWAKA 2020

**UTANGULIZI**
Foundation for Civil Society (FCS) ni asasi huru iliyoanzishwa Tanzania mwaka 2002 na kuanza shughuli zake rasmi mwaka 2003 kama Kampuni yenye Dira ya kuchangia maendeleo endelevu kupitia kuimarisha uwezo wa asasi za kiraia Tanzania, ushawishi wa kisera na kuimarisha utamaduni wa kujifunza. FCS inafanya kazi katika kuhakikisha kwamba asasi za kiraia Tanzania zinakuwa chachu kwenye michakato ya maendeleo yenye kulenga katika kuleta mabadiliko kwa wananchi; FCS inafanya kazi na asasi za kiraia katika maeneo makuu matatu ambayo ni: Utawala Bora; Kuimarisha hali ya maisha (kipato) na maendeleo ya kiuchumi, na Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa wadau wa maendeleo. Taarifa zaidi kuhusu dira, lengo mahsusi na kazi tunazofanya tembelea: **http://www.thefoundation.or.tz.**

**MAENEO YA UTEKELEZAJI PROGRAMU**
FCS kwa mwaka 2020 itatoa ruzuku kwa asasi za kiraia zilizopo Zanzibar (Unguja na Pemba) kutekeleza miradi katika maeneo yafuatayo:-

**A. Haki za Wanawake na Watoto:**
- o Miradi inayolenga kupinga mila potofu na unyanyasaji kwa wanawake na watoto (ikiwemo ubakaji, mimba za utotoni, ndoa za utotoni, pamoja na ukatili mwingine kwa wanawake na watoto.

**B. Haki za Ardhi kwa Wanawake:**
- o Miradi inayolenga katika kuwezesha upatikanaji wa ardhi na haki nyingine za kumiliki mali kwa wanawake.

**C. Ujenzi wa Amani na Utatuzi wa Migogoro katika Jamii:**
- o Miradi inayolenga ujenzi wa amani na utatuzi wa migogoro katika jamii na kuchangia katika kukuza udugu na mshikamano katika jamii na makundi mbalimbali ya watu.

**Kiwango cha Ruzuku kitakachotolewa na muda wa Utekelezaji**
FCS itatoa kiasi cha takriban TZS 40,000,000 kwa kila taasisi kwa ajili ya kutekeleza mradi. Kwa kuzingatia kuwa ruzuku hizi ni ndogo tunatarajia kuwa waombaji watakuwa na shughuli za kimkakati zaidi ili kufikia malengo. Muda wa utekelezaji wa mradi utakuwa ni (Machi – Novemba 2020)

**Vigezo vitakavyozingatiwa katika kuidhinisha miradi**
Kigezo kikuu kitakachozingatiwa katika kuidhinisha na kuuthibitisha mradi wowote ili kupata ruzuku kutoka FCS ni baada ya kujiridhisha kwamba shughuli za mradi husika zinadhihirisha pasipo shaka kuwa zitawanufaisha (moja kwa moja) walengwa wa maombi haya kama ilivyobainishwa katika Malengo Makuu ya wito huu.

Vigezo vingine mahsusi ambavyo vitazingatiwa katika uidhinishaji wa mradi ni;
- Ni kwa jinsi gani shughuli zilizopangwa, matokeo tarajiwa pamoja na mbinu pendekezwa katika andiko la mradi zinaendana na malengo makuu ya programu kama ilivyoelezwa kwenye tangazo.
- Uwezo na ubunifu wa miradi yenye kuleta tija kwa gharama nafuu.
- Nafasi ya jamii na ushirikishwaji - kiwango cha uhusishwaji wa jamii katika kutekeleza miradi inayowahusu na kwa jinsi gani mradi utaweza kuinufaisha jamii hadi katika ngazi ya chini kabisa kwa uthibitisho wa takwimu na ushahidi.
- Historia ya Taasisi, uwezo wa wafanyakazi wake na sifa zao katika kutekeleza miradi na matumizi ya Fedha hususani kuzuia Ubadhirifu
- Jinsi na namna ambavyo mradi husika utahusisha Taasisi na Mamlaka husika za Serikali katika utekelezaji ili kuleta uendelevu wa mradi.
- Uwepo wa nyaraka zote za muhimu zinazohitajika katika fomu ya maombi, zikiwemo fomu ya bao mantiki, mpango kazi, na bajeti, zinazopatikana kwenye tovuti ya Foundation.

**Taasisi na shughuli ZISIZOLENGWA kupata ruzuku.**
FCS itatoa ruzuku kwa Taasisi ambazo zimesajiliwa, kufanya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na ambazo hazizalishi faida. Kama maelezo na ufafanuzi zaidi vitahitajika juu ya kigezo hiki, basi wasiliana na FCS kabla haujafanya maombi yako ya ruzuku.

**FCS haitatoa ruzuku kwa:**
- Udhamini na ufadhili
- Miradi au shughuli zitakazo fanyika nje ya Tanzania
- Miradi au shughuli ambazo zimeshawahi kufanyika na kukamilika.
- Miradi ambayo imekwisha wezeshwa ruzuku na mashirika mengine.
- Kutumika kama Malipo ya ziada kwa wafanyakazi wanaolipwa na taasisi husika
- Kipato cha mtaji kwa taasisi ndogondogo za fedha
- Maombi toka kwa wataalamu wa ushauri au watunisha mifuko kwa niaba ya taasisi.
- Watu binafsi
- Vyama vya siasa
- Miradi ambayo inalenga kuinufaisha dini/dhehebu fulani, kabila fulani au kikundi fulani chenye mlengo wa kikabila.
- Sekta binafsi (isipokuwa kama haipo kwa ajili ya manufaa ya kuzalisha faida)
- Taasisi zenye madeni
- Waendesha Semina, warsha, na mikutano tu, isipokuwa kama ni sehemu ya shughuli zilizounganishwa na tokeo mahususi.
- Gharama kubwa zisizo tarajiwa (dharura)

**ANGALIZO KWA WAOMBAJI WOTE**
Foundation for Civil Society, ni asasi ya kiraia inayojitegemea kimamlaka. Tunayo sera ya kuendesha shughuli zetu zote kwa uaminifu, kimaadili na uwazi. Katu hatuvumilii hongo, rushwa wala aina yoyote ya ubadhirifu. Tumejitoa kuendesha mambo yetu kitaalamu, kwa haki, na uadilifu katika shughuli zetu na mahusiano yetu yote. Katika mchakato mzima wa kutoa ruzuku, FCS haitozi ada, wala kuomba fedha ama kupiga simu kwa wadau kwa minajili ya kuwasaidia ili wapitishwe kwenye ruzuku.
Hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa wapo matapeli wanaojifanya kuwaweza kuwasaidia. Tunawaalika wadau wote, iwapo unazo taarifa za uhakika zinazoashiria vitendo vya rushwa ama ubadhirifu katika mchakato huu au pia kwamba unaifahamu moja ya Taasisi iliyotuma maombi FCS na unajua kuwa wanachangamoto ya masuala ya rushwa ama ubadhirifu wa aina yoyote kama vile matumizi mabaya ya fedha za miradi, ikiwa ni pamoja na fedha za wafadhili wengine tafadhali usisite kutuandikia ili hatua stahiki zichukuliwe. Tafadhali zingatia njia sahihi za mawasilino kama inavyooneshwa hapa chini.

a. Kwa mawasilino ya kawaida na maulizo (Inquiries) tafadhali wasiliana nasi kwa kupiga simu kupitia nambari **+255 22 266 4890-2,** simu ya mkononi **+255 754 005708** au barua pepe: **information@thefoundation-tz.org**. Zingatia pia kuwa Maafisa wote na wafanyakazi wa FCS wanatumia barua pepe inayoishia na **@thefoundation-tz.org** na si vinginevyo iwapo una mashaka tafahdali usisiste kuwasiliana nasi kwa ufafanuzi na uhakika.
b. Kwa mawasiliano yote yanayohusu Rushwa, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za rushwa ama ubadhirifu tafadhali tuandikie kwenye barua pepe: **whistleblower@thefoundation-tz.org.** Taarifa zote zitakazotumwa kwenye narua pepe hii ni za siri na zitafanyiwa kazi kwa weledi na bila upendeleo. Kadhalika FCS inayo sera ya kulinda watoa taarifa.

**Utaratibu wa Uombaji**
Mashirika, ASASI na Taasisi zisizo za Serikali Zanzibar zinavyokidhi vigezo wanaalikwa kuomba ruzuku kwa Lugha ya Kiswahili ama Kingereza kwa kufuata utaratibu ufuatao.
a. Taasisi ijipime ni eneo gani kati ya maeneo 3 yaliyoainishwa imebobea zaidi na inauwezo wa kiutekelezaji ili kuleta matokeo tarajiwa (Mfano Haki za Ardhi kwa Wanawake) na haitakiwi kuomba eneo zaidi ya moja la matokeo yaliyoainishwa. Taasisi ambayo itatuma maombi zaidi ya nyanja zaidi ya moja itaondolewa kwenye hatua ya awali katika mchakato wa ruzuku.
b. Jaza fomu mahususi pamoja na viambatanisho vyake vinayopatikana katika tovuti ya Foundation for Civil Society www.thefoundation.or.tz
c. Weka viambatisho vyote muhimu (Orodha ya mambo yote muhimu imeambatanishwa katika fomu ya maombi)
d. Wasilisha maombi yako (Nakala 2) kwenda kwenye anuani hapo chini (Unaweza kuleta kwa mkono katika Ofisi ya FCS ama kutuma kwa njia ya EMS/Rejesta) kwenda:

**Kwa Mkurugenzi Mtendaji**
**Foundation for Civil Society**
**7 Madai Crescent, Ada Estate Plot Na. 154**
**S.L.B 7192**
**Dar es Salaam**
**Simu ya mezani +255 22 266 4890-2**
**Simu ya mkononi +255 754 005708**
**Tovuti: www.thefoundation.or.tz**

FCS haitapokea wala kufanyia kazi maombi yoyote yaliyoletwa kwa njia ya kieletroniki kama vile kupitia barua pepe.

215564702

# Bodaboda wanufaika kampeni MastaBoda

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Madereva na Wamiliki wa Bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD), Michael Masawe, ameitaja Kampeni ya NMB MastaBoda, inayolenga kuirasmisha sekta ya usafirishaji kwa njia ya pikipiki, kuwa mkombozi wa vijana katika mkoa wake na taifa kwa ujumla.

Masawe aliyasema hayo juzi wakati wa hafla ya kukabidhiwa simu janja 'smartphone' kwa madereva wanane wa pikipiki, maarufu kama bodaboda, waliotangazwa washindi wa simu janja na 60 walioshinda fedha taslimu.

NMB MastaBoda, inayoratibiwa na Benki ya NMB na Kampuni ya Mastercard QR, ilianzishwa Oktoba 16 na kutarajia kufikiwa ukomo mwishoni mwa Januari mwakani, ambako madereva watakaofanya miamala mingi kupitia Mastercard QR, watajipatia pikipiki aina ya Boxer.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi zawadi za simu janja aina ya Tecno Pop 2F na kofia ngumu za madereva pikipiki 'Helmet,' Masawe alisema katika kipindi cha miezi miwili ya uwepo wa NMB MastaBoda, maisha ya wengi miongoni mwa wanachama wake yamebadilika.

Alifafanua MastaBoda imesaidia kujenga heshima miongoni mwa madereva wa huduma hiyo, ambao sio tu wamepanua wigo wa kujituzia akiba kupitia mfumo rasmi wa Mastercard QR, bali pia kujiwezesha kushinda zawadi mbalimbali kulingana na uwingi wa miamala yao kwa wiki na mwezi. Madereva bodaboda wanane walijinyakulia simu hizo, hivyo kufanya idadi ya walionufaika na huduma hiyo kufikia 60, kwani kabla ya jana, madereva 60 walijishindia pesa taslimu kiasi cha Sh. 50,000 kila mmoja. Madereva waliojinyakulia simu janja jana na vituo vyao vya kazi kwenye mabano ni; John Haonga (Mabibo), Abdallah Mohamed (Morocco), Florian Celestine, Twalha Mfinanga na Mohamed Abdallah (Buguruni Rozana), Ebenezer Elisha (Mwenge), Ladislaus Laiza (Ubungo Plaza) na Adam Gunza (Mlimani UDSM).

Meneja Mwandamizi Kitengo cha Bidhaa za Kadi wa NMB, Rupia

Alisema kuelekea kuhitimisha kampeni hiyo mwishoni mwa mwezi ujao, wamejizatiti kuwafikia madereva bodaboda wapatao 75,000 kati ya milioni mbili wanaotoa huduma hiyo kote nchini, ili kuwaunganisha na mfumo huo wa utoaji huduma kisasa.

Aliwataka madereva bodaboda kuhakikisha wanajituma ili kuongeza miamala yao kwa siku, wiki na mwezi, ili kunufaika na zawadi mbalimbali.

Washindi hao waliipongeza NMB kwa wazo lililozaa huduma hiyo, na kwamba kupitia huduma hiyo, wameweza kujiwekea akiba pamoja na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima, sambamba na kumaliza tatizo la upotevu wa pesa zao nyakati za ajali.

# Polisi yakamata gongo lita 427

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limekamata pombe haramu aina ya gongo lita 427 pamoja na mitambo mitano ya kutengenezea pombe hiyo.

Jeshi la Polisi limesema gongo hiyo ilikuwa ikiuzwa kwenye maeneo mbalimbali ya mkoani hapa. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Sophia Jongo, kwa kipindi cha kuanzia Novemba hadi Desemba mwaka huu katika misako mbalimbali iliyofanywa ya kiuhalifu, wamekamata vitu mbalimbali vya wizi pamoja pombe hiyo haramu ambayo imepigwa marufuku. Alisema katika msako huo wa miezi miwili walikamata vitu vya uhalifu vikiwamo magodoro 24, pombe kali ambayo imepigwa marufuku na serikali katoni 1,490, simu za mkononi tatu, wire cable mita 48, pikipiki mbili, baiskeli tisa, pombe ya gongo lita 427 na mitambo yake, pamoja na Tv, jeki za gari, simu, redio na solar panel.

"Watu wote waliohusika na matukio haya ya uhalifu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani ili kujibu mashtaka yanayowakabili, natoa wito kwa wananchi wafike kwenye kituo cha polisi kuja kubaini vitu vyao ambavyo viliibiwa, ili wakabidhiwe kwa mujibu wa sheria," alisema Jongo na kuongeza:

"Pia natoa wito kwa wananchi kwenye kipindi hiki cha msimu wa sikukuu wawe makini na makazi yao, na kutoacha nyumba peke yake, kwa kuwa wahalifu hutumia mwanya huo kufanya uhalifu na kupora mali zao... bali watakapokuwa wakitoka waache mtu mmoja wa kulinda nyumba ili wasiibiwe." Katika hatua nyingine, alitangaza kupiga marufuku disko za watoto kwenye kumbi za starehe bali wawa peleke watoto wao kwenye maeneo ya wazi.

Kaimu Kamanda huyo alisema kwenye kumbi za starehe huwa kuna matukio mengi ya kihalifu.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga kushirikiana na jeshi hilo kikamilifu kwa kutoa taarifa za kihalifu ili wahusika watiwe nguvuni mapema kabla ya kuleta madhara.



Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Azza Hilali Hamadi (wa pili kushoto), akipanda mpunga kwenye mashamba yake yaliyopo kijiji cha Welezo, Kata ya Nsalala, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. **PICHA MARCO MADUHU**

# Agricom Africa yampa jeuri Sanare uchumi wa viwanda

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loatha Sanare, amerIdhishwa na kupongeza kazi zinazofanywa na kampuni ya Agricom Africa mkoani humo, akisema zinatafsiri kwa vitendo azma ya serikali ya kujenga ya

ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema hayo katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Mohamed Utaly katika hafla ya kuhitimu mafunzo ya wiki sita yalitolewa na Agricom Africa kwa vijana juu ya uendeshaji na utengenezaji wa zana za kisasa za kilimo yakiwamo matrekta na 'pawatila'.

"Natumia fursa hii kuishuru kampuni hii ya Agricom Africa kwa kazi kubwa inayofanya katika Mkoa wa Morogoro na hasa kuandaa mafunzo haya kwa vijana kwani yatasaidia kuchochea ukuaji wa teknolojia katika kilimo," alisema.

Sanare alisema uwekezaji katika sekta ya kilimo lazima utiliwe mkazo hasa katika kipindi hiki ambacho serikali imeazimia kuleta mageuzi ya uchumi wa kati na viwanda kwa sekta ya kilimo ndiyo mchagizaji mkubwa katika kufanikisha azma hiyo.

"Hakuna maendeleo ya viwanda kama sekta ya kilimo haitafanya mageuzi makubwa, hivyo wakati serikali ikiwa imejikita na azma ya ujenzi wa viwanda ifikapo 2025, lazima kuhamasisha wadau wa kilimo na maendeleo kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta hii ili kupata malighafi ya

kutosha ambazo zitatumika katika viwanda vyetu," alieleza Sanare.

Aidha, Sanare alitoa wito kwa wahitimu hao kutumia vyema mafunzo waliyoyapata ili waweze kujinufaisha kiuchumi na kuchangia mageuzi katika kilimo hali ambayo itaongeza pato la nchi.

Mwenyekiti wa Kampuni hiyo, Angelina Ngalula, aliishukuru serikali Mkoa wa Morogoro kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji licha ya mkoa huo kukabiliwa na migogoro mingi ya wakulima na wafugaji huko nyuma.

"Miaka kadhaa iliyopita ilitawaliwa na migogoro ya wakulima na wafugaji, hali hiyo haikuwa rafiki kwa wawekezaji, lakini serikali ya mkoa ilipambana na sasa Morogoro hali ni shwari na imetuvutia kuja

kuwekeza," alisema Ngalula.

Ngalula pia ni Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), alishukuru pia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ambayo imepewa jukumu la kusimamia miradi ya ujuzi nchini kuendelea kutoa pesa ili kuwaunganisha vijana na fursa mbalimbali.

# Tume Atomiki yajipanga mafunzo mionzi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

TUME ya Taifa ya Nguvu za Nyuklia, imejipanga kutoa mafunzo kwa mafundi wa mashine za mionzi ili kuondoa mikwamo ya mashine hizo zinapoharibika.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC), Prof. Lazaro Busagala, aliyasema hayo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya siku tano ya udhibiti wa usalama wa mionzi kutoka Idara za Diolojia kwenye hospitali na vitengo vya X-ray na Utrasound, yaliyoshirikisha wataalamu wa mionzi 104, kutoka hospitali mbalimbali nchini.

"Tunatoa mafunzo haya kutokana na ongezeko la matumizi ya sayansi na teknolojia, hivyo lazima tujipange kuelimisha wadau wetu ili hata mashine zao zinapokwama wafahamu jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo," alisema.

Busagala, alisema TAEC, ina vituo 664, ambavyo 106 kati ya hivyo, vilikaguliwa na kukidhi matumizi salama na vituo 10 vilifungiwa, lakini kwa sasa vimefunguliwa baada ya kutimiza masharti.

Alisema tume hiyo, haitaruhusu matumizi holela ya mionzi ambayo inaathiri afya za wananchi wakiwamo wajawazito na watoto.

Alisema mwaka 2018, kulitokea misuguano kati ya waganga wakuu wa hospitali na wataalamu wa picha za mionzi na kusababisha vituo hivyo, kufungiwa hatua iliyowalazimu kutoa mafunzo ya kuondoa misuguano ili kuboresha utendaji.

Aliwataka waajiri kuwasilisha taarifa na majina ya wataalamu hao kwenye tume hiyo ili kufanyika ukaguzi kwenye kitengo cha diologia na wapewe leseni ya kuendesha shughuli za mionzi.

"Kinyume na hili hamtaweza kamwe kupewa leseni wala kuruhusiwa kufanya kazi za mionzi," alisema.

Alisema usalama wa mionzi upo mikononi mwao hivyo kila mmoja azingatie sheria na taratibu zote zinazohusu mionzi ili watu wawe salama.

Aliwataka wataalamu hao, kutoa taarifa za haraka kwa tume pale wakaguzi wanapochelewa ili wakague ubora wa vifaa vya mionzi na kuondoa hali hatarishi ya afya za wananchi.

Mtaalamu Mkuu wa mionzi Mkoa wa Pwani, Faustini Mulyutiu, aliwaomba viongozi wa wizara kuwatembelea ili kusikiliza kilio chao na kuwapa ufadhili wa masomo yao kwa ajili ya kuboresha utendaji wao.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zuwena Omary, akizungumzia fursa ya mikopo kwa wanawake, vijana na walemavu katika kijiji cha Lengast juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanafunzi vyuo, sekondari kutembelea hifadhi

**Na Daniel Sabuni,** ARUMERU

WANAFUNZI wa vyuo na shule za sekondari wilayani Arumeru, kuanzia Januari mwaka 2020, wataanza kutalii kwenye hifadhi tatu za taifa za Arusha ili kuongeza mapato na idadi ya watalii wa ndani.

Licha ya kuongeza kipato kwa utalii wa ndani pia itatoa fursa kwa wanafunzi na wana vyuo hao, kufurahia vivutio na mandhari yaliyomo hifadhini.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, aliyasema hayo jana kwa watalii wa ndani wakati wa uzinduzi wa ofa maalum ya utalii wa ndani kuelekea maadhimisho ya sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya.

Shughuli hiyo ya kitalii itaanzia katika lango la Ngongongare katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha (ANAPA).

Muro alisema anasimamia na kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambayo ni kusimamia rasilimali na kukuza utalii wa ndani na wa nje kwa kuweka mkakati ya kushirikiana na wahifadhi, walimu na wazazi hadi kufikia malengo.

"Tulipitia mazingira magumu, kuvutana kukosoana, lakini mwisho mkakati wetu na mpango wetu na wazazi tumeelewana na kukubaliana ili uwe sehemu ya mtaala wa elimu, wanafunzi wanapofanya utalii ndani kuna vitu vingi wanajifunza kuhusu viumbe hai na uhifadhi wa mazingira na baada ya kupata fursa hii ya kujifunza watajikwamua na watakuwa mabalozi wazuri wa utalii wa ndani," Muro.

Alisema hadi kufikia mwaka 2021 wanatarajia idadi kubwa ya watalii wa ndani kuongezeka katika hifadhi ya Anapa kutokana na jitihada za uhamasishaji kwa kushirikiana na wataalamu wake. Alisema katika uzinduzi huo, aliambatana na Mwenyekiti wa Wilaya Arumeru na Katibu wake, ili kuona jitihada zinazofanywa na viongozi na watumishi wa serikali kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya.

"Nimewaleta hawa wa CCM, kuona kazi kubwa iliyofanywa ya kuhifadhi ikolojia iliyopo, naomba mkawaambie wananchi ardhi haiongezeki, lakini watu wanaongezeka sasa hivi Arumeru kuna watu 700,000 wanaoingia kwenye maeneo ya hifadhi," alisema.

Naye Kaimu Kamishna Msaidizi Maria Saidia, awali alimkaribisha mgeni rasmi, alisema ofa hiyo hutolewa na Anapa kila mwaka ili kuwashawishi Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea hifadhi kwa faida ya taifa. "Wazungu wanadunduliza fedha kidogo mpaka miaka mitatu waje kutembelea hifadhi zetu, lakini sisi tupo karibu na hatujawahi kufika, alisema.

Saidia alisema lengo la kuandaa mpango huo ni kuendelea kuongeza mapato kwa nchi yatokanayo na utalii wa ndani.

# Msaada kisheria wapunguza majukumu

**Na Allan Isack,** MANYARA

WAKUU wa Madawati ya Jinsia na Watoto, Polisi Mkoa wa Manyara, wamesema kuwapo kwa wasaidizi wa kisheria kwenye maeneo mbalimbali mkoani humo, kumewapunguzia majukumu ya kazi tofauti na awali kabla hawajatambulika rasmi kisheria.

Wakuu hao, waliyasema hayo, kwenye tamasha la wadau wa maendeleo wa mkoa wa Manyara, lililofanyika ukumbi wa White Rose Mjini Babati.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Polisi Wilaya ya Babati, Sada Gabi, alisema kupitia wasaidizi wa kisheria wamepunguza kesi kwa sababu mambo mengi wanayatekeleza wasaidizi wa kisheria.

Gabi alisema wasaidizi wa kisheria wanawaelekeza jamii yenye matatizo sehemu za kwenda kupata msaada ikiwamo kwenye baraza la ardhi, mahakama, ofisi za watendaji wa vijiji na kata au polisi.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Polisi wilayani Mbulu, Glory Daudi, alisema kwenye eneo hilo, wamekuwa na urahisi wa kufanya kazi zao, kwa kuwa wanashirikiana kwa ukaribu na wasaidizi wa kisheria.

Alisema kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na wasaidizi hao, kwa jamii, mabadiliko yanaonekana tofauti na awali, walikuwa wanatekeleza majukumu hayo bila ya kupata msaada popote.

Mkurugenzi wa Shirika la CSP, Nemence Iriya, alisema wanajipanga kutanua wigo wa shirika hilo, kufanya kazi zake kwenye baadhi ya mikoa nchini badala ya kuishia Mkoa wa Manyara pekee.

"Kwa kiasi kikubwa kwenye Mkoa wa Manyara tumefanikiwa kuwa na wasaidizi wa kisheria kwenye wilaya zote tano hivyo, tunatarajia kwenda kwenye baadhi ya mikoa mingine nchini," alisema Iriya.

Msaidizi wa kisheria kutoka wilayani Kiteto, Abasi Famau, ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Kiteto Legal and Humanity Aid Organization (KLHA), alisema kupitia Shirika la CSP, jamii nyingi zimefaidika kwa kupata ushauri wa kisheria bila malipo.

"Kupitia uwezeshaji wa CSP, jamii imepata misaada mbalimbali ikiwamo kuwatetea wananchi wa Wilaya ya Kiteto ambao nyumba zao zilitakiwa kuvunjwa bila ya kulipwa fidia na tuliwatetee walipwe haki zao," alisema Famau.





# Soko la maziwa Moshi lapasua vichwa wadau

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UKOSEFU wa soko la maziwa kwa wafugaji mkoani Kilimanjaro unaosababisha kiasi kikubwa cha chakula hicho kumwagwa, unawapasua vichwa baadhi ya wadau wakiwamo serikali na wahisani.

Meneja wa Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), linalosaidia uboreshaji wa uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, Tom Losikari, alisema wanatafuta dawa ya tatizo hilo.

Losikari alieleza, "wanapomwaga maziwa kwa kukosa soko inawakatisha tamaa sana, sasa SNV tunatafuta dawa yake, lakini tunataka na serikali ifikirie namna ya kutatua tatizo hili ili kutimiza malengo yake ya kuelekea katika uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya Tanzania ya Viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Kilio cha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa Kilimanjaro, kinafanana na cha wafugaji wengine nchini Tanzania, wakati wafugaji hao wakilalamikia soko la maziwa, kuna maeneo mengine watu wanahitaji maziwa lakini hawayapati."

Alisema iko haja ya kuanzishwa kwa mtandao wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa ili wawe na umoja wa kutafuta masoko ya maziwa ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, takwimu za Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) zinaonyesha kuwa unywaji wa maziwa nchini ni wastani wa lita 47 kwa mtu mmoja kwa mwaka, wakati Shirika la Chakula Duniani (FAO) linapendekeza kunywa lita 200.

Licha ya tatizo hilo, inaelezwa kuwa baadhi ya vyama vya ushirika vimekuwa kikwazo kwa kutokuwa na miundombinu mizuri ya kuhifadhia maziwa, hali ambayo inasababisha maziwa mengi kuharibika na kukosa soko.

Kutokana na malalamiko hayo, wiki iliyopita Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, aliagiza Bodi ya Maziwa Tanzania pamoja na serikali ya mkoa wa Kilimanjaro kuhakikisha wanatafuta suluhisho la tatizo hilo mara moja.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kippi Warioba, alikiri kupokea malalamiko ya wafugaji hao na kwamba changamoto kubwa ni wazalishaji wengi hawajaongeza thamani ya uchakataji maziwa.

Warioba alisema hali hiyo ndiyo inayosababisha maziwa mengi yanayokusanywa mitaani kuharibika kwa kukosa masoko.

# Wahitaji 25 hatarini kukwama kimasomo

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WATOTO wahitaji 25 walio katika Kituo cha Hope Evangelist Ministry cha Wilaya ya Siha, wanaomba wahisani kuwasaidia fedha za kulipia chakula na mahitaji mengine ya shule.

Mlezi wa watoto hao, Esther Mosi, alisema watoto hao ambao wametokea katika maeneo mbalimbali baada ya kupoteza wazazi wao, wanahitaji misaada ya hali na mali ili kukamilisha safari yao ya kielimu.

Mosi alisema hayo baada ya kupokea vifaa mbalimbali kwa ajili ya watoto hao vyenye thamani ya zaidi ya Sh. 2,000,000 vilivyotolewa na Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Walimu wa Wilaya za Hai na Siha.

Mbali na chakula, watoto hao pia hawana uwezo wa kupata vifaa vya masomo na sare za shule, huku wakilazimika kurudi kila siku kituoni kula chakula cha mchana kinachotolewa na mlezi wao ambaye analima na kutoa sehemu ya chakula cha familia yake kwa ajili ya watoto hao.

"Nawashukuru sana walimu kwa kutukumbuka na kutuletea misaada hii muhimu ya kibinadamu. Hawa watoto hawali shuleni na wenzao kwa sababu hawana fedha za kulipa michango ya chakula cha mchana. Nalazimika mimi kupika chakula chao na cha wanangu kila siku ili warudi shule wakasome, uwezo wangu ni mdogo kumudu watu wote hawa, ndio maana naomba misaada," alisema Mosi.

Alisema kwa sasa wamekuwa wakitafuta misaada kwa wasamaria wema ili kuwasaidia watoto hao, lakini haikidhi mahitaji ya watoto 25.

Kutokana na hali hiyo, Mosi ameiomba serikali na wadau kuangalia namna ya kuwezesha watoto hao kupata mahitaji ya kibinadamu pamoja na elimu.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Walimu wa Wilaya za Hai na Siha, Terewandumi Swai, akizungumza kabla ya kukabidhi misaada hiyo, alisema kutokana na hali ilivyo kituoni hapo, wanachama waliridhia kwa kauli moja kutoa misaada ya watoto hao ambao ni pamoja na kuwalipia michango ya shule wanafunzi watano wa Shule ya Sekondari Sanya juu wanaosoma kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Swai alisema: "Tumeona watoto hao jinsi walivyo na hali ngumu na namna wanavyoishi shuleni, tunaishukuru sana serikali kwa kuja na sera ya elimu bure, lakini changamoto kubwa ambayo watoto hawa wamekuwa wakiipata ni kurudishwa kituoni kula chakula cha mchana kutokana na kushindwa kulipa michango ya chakula shuleni."

Wakizungumza na Nipashe kituoni hapo walisema wamekuwa na ndoto nyingi katika maisha yao ya kuwa wataalamu mbalimbali baadaye, lakini wanaona kama wanaweza kuishia njiani kutokana na kukosa msaada.

Walisema changamoto zinazowakabili ni kukosa sare za shule na michango ya chakula shuleni.

Kutokana na changamoto hizo Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu Wilaya ya Hai kimewalipia watoto hao michango ya chakula shule kwa miaka mitatu zaidi ya milioni moja pamoja na kutoa vyakula na vifaa vya masomo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. 800,000 kwa watoto hao.




Watoto mkoani Kilimanjaro wakiwa kwenye lango kuu la kuingia hifadhini la Ngongongare, wakipata maelezo kutoka kwa mwongoza watalii wa mjini Moshi, kabla ya kutalii katika hifadhi hiyo, wakati wa uzinduzi wa dhifa maalum ya Watanzania kutembelea hifadhi hiyo. **PICHA: DANIEL**

# Jukwaa kujenga kituo cha kisasa cha saratani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATIKA jitihada za kupunguzia wagonjwa mzigo wa kusaka huduma nje ya mkoa, Jukwaa la Maendeleo la Mkoa wa Kilimanjaro (KDF), linakusudia kujenga kituo cha kisasa la saratani katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Mjumbe wa KDF, Balozi mstaafu, Fadhili Mmbaga, alisema wanautazama mradi huo kama njia mojawapo inayoweza kutumiwa kupunguza makali na mzigo wa wagonjwa wa saratani kufuata huduma nje ya mkoa huo.

"Jukwaa hili linalo uwezo wa kuwa na miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kuwekeza katika ujenzi wa kituo hicho cha saratani na nia yetu ni kurahisisha matibabu ya maradhi ya saratani. Yapo mambo mengi tunakusudia kuja nayo pia kama kujenga viwanda pamoja na kutoa huduma mbalimbali katika taasisi. "Tunadhani kwamba hata kutumika mapango ya asili kwa ajili ya shughuli za kitalii ambayo yalitumika enzi za ukoloni, kunaweza kutuingizia kipato kikubwa na kulisaidia taifa letu."

Aidha, alisema jukwaa hilo limeeleza mkakati wake wa pili wa kujenga kiwanda cha nguo mkoani Kilimanjaro kama moja ya fursa ya kutoa ajira kwa wananchi wengi.

Aidha, Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya, ambaye ni Mwenyekiti mstaafu wa KDF, alisema wananchi wa Kilimanjaro, marafiki na wadau wengine wanao uwezo wa kuunda chombo ambacho kitashawishi matumizi ya rasilimali zinazopatikana katika mkoa huo kusukuma maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii kwa ajili ya kutokomeza umaskini.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema miongoni mwa mambo yanayokumbukwa na KDF na ambayo hayatasahaulika ni juhudi za hayati Dk. Regnald Mengi kuboresha mazingira ya mkoa huo kwa kupanda miti zaidi ya milioni 24.

Alisema juhudi hizo za marehemu Dk. Mengi kuboresha mazingira mkoani Kilimanjaro, kumesaidia kupunguza athari za uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro.

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 23, 2019

# Nipashe Spotika



WAKALI 6 WA HAT-TRICK EPL UK. 16&17



## ISIKUPITE

KIUNGO wa Manchester City, Kevin de Bruyne amekuwa mchezaji wa kwanza Ligi Kuu England kufikisha tarakimu mbili za pasi za mwisho ['assists'] kabla ya Krismasi tangu kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil alipofanya hivyo msimu wa 2015-16 (akitoa pasi za mwisho 15).

## MKWAJU...

Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane, akijaribu kufunga huku akipata changamoto kutoka kwa beki wa pembeni wa Flamengo, Rafinha kwenye fainali ya Klabu Bingwa Dunia iliyopigwa Doha, Qatar juzi na miamba hiyo ya England kushinda 1-0. **HABARI UK. 29**




# MINAMINO KIDUME AMA GARASA LIVERPOOL?

**LIVERPOOL,** England

TAKUMI Minamino tayari ni mchezaji rasmi wa Liverpool. Wekundu hao baada ya mchezo wao dhidi ya Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, waandishi wa habari walianza kuripoti kwamba, kuna uwezekano wa mchezaji huyo kutua Liverpool.

**Baada ya saa kadhaa, klabu hiyo ya Ligi Kuu Austria ikathibitisha kwamba wamefikia makubaliano ya kumuuza mchezaji huyo kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 7.25.**

Liverpool waliona kile ambacho mchezaji huyo raia wa Japan anaweza kukifanya baada ya mechi zao mbili za Ulaya. Minamino tayari ameshafunga pale kwenye dimba la Anfield, akifunga wakati wakifungwa 4-3 Oktoba. Kuna video kwenye Twitter inamwonyesha kocha Jurgen Klopp akitikisa kichwa kulikubali bao la nyota huyo.

Minamino pia alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye kipindi cha kwanza cha mchezo wa marudiano nchini Austria, ingawa alishindwa kukinusuru kikosi chake kuepukana na kipigo na kuwafanya wao watue kwenye Ligi ya Europa.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, sasa anasubiri kuonyesha tena cheche zake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa sheria mpya za Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), inampa nafasi ya kuichezea timu nyingine kwenye hatua ya mtoano hata kama hatua ya makundi alikuwa na timu nyingine.

Kwa mujibu wa makubaliano kati ya klabu hizo mbili Minamino alisajiliwa kwa pauni milioni 7.25. Ingawa Klopp alionyesha kutokuwa na uhitaji wa kufanya usajili kipindi cha dirisha dogo la Januari, lakini usajili huo ni kwa ajili ya kukiimarisha zaidi kikosi chake.

Kwa sasa Minamino atakuwa na kazi ya ziada kupenya kwenye chaguo la kwanza la washambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane, Mohamed Salah na Roberto Firmino.

Pia Liverpool ina wachezaji wengine kama Divock Origi na Alex Oxlade-Chamberlain huku safu ya kiungo ina watu wengine kama Xherdan Shaqiri. Wakati akionekana kupenda zaidi kucheza kama winga, Minamino pia amekuwa akicheza nafasi ya kiungo pale Salzburg, na kuna wakati mwingine akicheza kama mshambuliaji wa kati na kiungo mshambuliaji.

Uwezo wake huo utamfanya Klopp kuwa na nafasi nzuri zaidi ya uchaguzi wa wachezaji wake katika kila mchezo kulingana na mahitaji halisi.

**TAKWIMU ZAKE**

Alisajiliwa kutoka Cerezo Osaka mwanzoni mwa 2015, Minamino alifunga mabao ya kuvutia kwenye misimu yake miwili ya kwanza.

Chini ya kocha Jesse Marsch, msimu huu amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 14 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Austria, ambayo pia inajulikana kama Bundesliga na mechi 11 alianza. Hakuna mchezaji wa Salzburg aliyetengeneza nafasi nyingi za mabao kama yeye.

Ana wastani wa kufunga bao na kutoa pasi ya mwisho katika kila dakika 91 kwenye mchezo wa Ligi Kuu msimu huu wa 2019-20, huku namba ikiongezeka hadi 102 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Inatakiwa kukumbuka kwamba, kama ilivyokuwa Liverpool, Salzburg pia walikuwa na nafasi ya kufuzu kutoka hatua ya makundi kwenda kwenye mtoano kwenye kundi ambalo lilikuwa na miamba wa Italia, Napoli.

Minamino pia analingana na Roberto Firmino kwa kutoa pasi za mwisho tatu kwenye Ligi ya Mabingwa na wastani wa 18.18, nyuma ya Mane na Salah wenye wastani wa 20.

Uhakika wa pasi zake ni asilimia 73.38 akimshinda Salah mwenye asilimia 72.19. Pia ametengeneza nafasi nyingi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya (12) akimshinda Salah mwenye tisa na amezidiwa moja na Mane mwenye 13. Aidha, amepiga chenga mara tisa akizidiwa na Mane (15) na Salah (16).

**WANACHOSEMA JUU YAKE**

Klopp akimzungumzia mchezaji huyo alinukuliwa akisema: "Takumi ni mchezaji mwenye kasi, akili na anajua kutafuta nafasi. Akiwa na mpira ni ngumu kumpokonya. Minamino pale Liverpool atavaa jezi namba 18 mgongoni.

**JE, WAJUA?**



MATOKEO ya sare tasa [0-0 ] Arsenal iliyoyapata juzi dhidi ya Everton ni mara ya kwanza kwa klabu hiyo ya London kuyapata katika mechi za 77 za Ligi Kuu ilizocheza tangu ilipopata matokeo kama hayo ugenini dhidi ya West Ham Desemba 2017.



# YANGA INAVYOWASHUKIA VIBONDE KOMBE FA

Mshambuliaji wa Yanga, Patrick Sibomana, akijaribu kumtoka beki wa Iringa United kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Uhuru. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi Yanga huwa haifanyi mzaha kabisa linapokuja suala la michuano ya Kombe la FA, ikicheza na timu ambazo si saizi yake.

**Ni tofauti kabisa na Simba ambayo ilitolewa mara mbili misimu miwili iliyopita na Green Warrios na kisha Mashujaa FC ya Kigoma, tena ikitolewa kwenye mechi zake za kwanza za michuano hiyo.**

Yanga haijawahi kutolewa kwenye mechi yake ya kwanza ya Kombe la FA, ambapo timu za Ligi Kuu huanza kucheza kwenye raundi ya tatu.

Jumamosi iliyopita Yanga ilifanikiwa kusonga mbele kwenye michuano ya Kombe la FA, kusaka bingwa atakayeiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Yanga iliifumua Iringa United mabao 4-0 na kufanikiwa kusonga mbele kwenye hatua ya raundi ya nne ya michuano hiyo.

Yalikuwa ni mabao ya mapema kabisa ya Papy Tshishimbi dakika ya saba na dakika mbili baadaye Patrick Sibomana alifunga bao la pili.

Beki aliyerejea tena baada ya kutokea kutokuelewana baina yao na matatizo kumalizwa, Lamine Moro, alifunga bao la tatu na David Molinga akafunga la nne dakika ya 68.

Hata hivyo, pamoja na Yanga kuwa ni timu iyojiwekea rekodi ya kutofungwa kwenye mechi za kwanza na kutoa vipigo kwa timu ambazo si saizi yake, lakini katika misimu mitatu iliyopita tangu michuano hiyo irejeshwe tena, imetwaa kombe hilo mara moja tu msimu wa 2015/16, huku Simba ambayo huwa na tabia ya kutolewa na vibonde misimu miwili mfululizo mwaka 2017/18 na 2018/19, nayo ilifanikiwa pia kutwaa Kombe la FA mara moja, msimu wa 2016/17.

Mwandishi wa makala haya amekusanya matokeo ya mechi za kwanza za Yanga Kombe la FA kuonyesha jinsi ilivyokuwa na uwezo wa kucheza mechi zake za kwanza za michuano hiyo dhidi ya vibonde, haijalishi kama inatolewa baadaye.

**YANGA 2-1 JKT MLALE-(2016)**

Yanga ilianza michuano hiyo dhidi ya JKT Mlale. Mechi hii ilichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Februari 24, 2016 na Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya JKT Mlale ya Ruvuma na kuiwezesha kusonga hatua inayofuata.

Mabao ya washindi yalifungwa na Paul Nonga ambaye kwa sasa anaichezea Lipuli FC kwenye dakika ya 38, huku Thabani Kamusoko ambaye kwa sasa yuko Zesco United, akifunga bao la pili dakika ya 58.

Bao la kufutia machozi la wageni lilifungwa na Shaaban Mgandila ambaye yeye ndiye aliyeanza kufunga dakika ya 22 na kuonekana kama vile amechokoza nyuki.

Ni mwaka ambao Yanga ilitwaa Kombe la FA na kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa kuifunga Azam FC mabao 3-1 kwenye mechi ya fainali, Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salam.

Mabao ya mabingwa hao yalifungwa na Amissi Tambwe aliyetupia mawili dakika ya tisa na 47, huku Deus Kaseke akifunga dakika ya 81. Kaseke alikuwapo kwenye mechi ya Jumamosi wakati Yanga ikiishindilia Iringa United mabao 4-0. Bao la kufutia machozi la Azam lilifungwa na Didier Kavumbagu.

**YANGA 2-0 REHA-(2017)**

Yanga ilianzia kwenye raundi ya tatu kwa kuicharaza Reha ya Dar es Salaam mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, mechi ikichezwa Desemba 24, 2017, siku moja tu kabla ya Sikukuu ya Krismasi.

Ilionekana kama timu hizo zingeenda kwenye mikwaju ya penalti, lakini dakika ya 82, mchezaji aliyetoka kwenye mzozo wa usajili wa dirisha dogo msimu huo kati ya klabu hizo kongwe za Simba na Yanga, Pius Buswita alifunga bao dakika nane kabla ya mechi hiyo kumalizika.

Buswita ambaye alikuwa amesimamishwa baada ya kubainika kusaini klabu zote mbili, alianza kuichezea Yanga baada ya Simba kuamua kuondoa jina lake kwenye usajili, kutokana na mvutano uliodumu kwa muda.

Straika hatari kipindi hicho, Amissi Tambwe, raia ya Burundi, aliipatia Yanga bao la pili dakika ya 84, dakika mbili baada ya bao la kwanza na kuihakikishia Yanga kusonga mbele kwenye hatua ya raundi ya nne ya michuano hiyo ya Kombe la FA.

**YANGA 4-3 IHEFU FC- (2018)**

Yanga iliiondoa Ihefu kwenye raundi ya tatu ya michuano hiyo kwa mikwaju 4-3 ya penalti, baada ya sare ya bao 1-1 kwa dakika 90, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya Januari 30, 2018.

Ihefu ilitangulia kupata bao dakika ya 36, lakini Yanga ikalirudisha dakika ya pili kati ya zile sita za nyongeza na kuifanya mechi hiyo kwenda hatua ya kupigiana penalti.

Yanga ilifunga penalti zao kupitia kwa Kelvin Yondani, Hassan Kessy ambaye kwa sasa anaichezea Nkana FC, Gadiel Michael anayeichezea Simba kwa sasa, na Rafael Daudi, huku Papy Tshishimbi na Obrey Chirwa anayekipiga Azam FC kwa sasa, wakikosa penalti zao, wakati Andrew Kayuni, Mando Mkumbwa, na Jonathan wakifunga upande wa Ihefu.

Wachezaji waliokosa ni Aboubakar Kidungwe, Emmanuel Mamba na Richard Ng'ondya na kuifanya Yanga kusonga mbele kwenye hatua ya raundi ya nne ya michuano hiyo.

## NJE YA UWANJA

KUTOKANA na mechi ya fainali ya Klabu Bingwa Dunia kati ya Liverpool ya England na Flamengo ya Brazil kuchezwa kwa dakika 120 juzi, hii inakuwa ni mara ya nne kwa mechi ya fainali ya michuano hiyo kufika muda huo baada ya mwaka 2000, 2009 na 2016. Kadhalika, klabu za Ulaya zimeshida mara 12 katika fainali 13 za Klabu Bingwa Dunia zilizopita, ikiwa ni pamoja na michuano saba iliyopita.



# WAKALI 6 WA HAT-TRICK EPL


SERGIO AGUERO

**LONDON,** England

TANGU kurekebishwa kwa muundo wa Ligi Kuu ya England msimu wa mwaka 1992-93, zaidi ya wachezaji 100 wamefunga hat-trick.

**Wachezaji 36 tofauti wamefunga zaidi ya mabao matatu au zaidi kwenye Ligi Kuu ya England mara nyingi tu.**

Eric Cantona kutoka Taifa la Ufaransa alifunga hat-trick ya kwanza kwenye Ligi Kuu kwenye mchezo wa Leeds United dhidi ya Tottenham Hotspur.

Tangu hapo wachezaji 42 kutoka mataifa tofauti wamefunga hat-trick.

Hat-trick 148 zimefunga na wachezaji wa Uingereza, huku 17 zikifungwa na wachezaji raia wa Argentina na ndio wanaongoza kwa wachezaji kutoka nje ya Ulaya waliofunga hat-trick nyingi kwenye Ligi Kuu ya England.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji sita waliofunga hat-trick nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya England...

## 6. MICHAEL OWEN (LIVERPOOL / NEWCASTLE UNITED) - 8

Michael Owen alifunga hat-trick yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu wakati akiwa na umri wa miaka 18, alifunga mabao yote matatu wakati Liverpool ikitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Sheffield United mwaka 1997-98.

Owen alifunga tena hat-trick dhidi ya Newcastle United na Nottingham Forest msimu wa 1998-99. Misimu miwili baadaye, mshambuliaji huyo wa Uingereza alifunga hat-trick mbili ambapo alifunga mabao yote matatu dhidi ya Aston Villa na Newcastle United.

Msimu wa 2002-03, Owen alifunga hat-trick dhidi ya Manchester City na West Bromwich Albion.

Hat-trick ya mwisho na ya nane kwa Owen kwenye Ligi Kuu alifunga wakati Newcastle United ikiibuka na ushindi wa 4-2 dhidi ya West Ham United msimu wa 2005-06.

## 5. HARRY KANE (TOTTENHAM HOTSPUR) - 8

Harry Kane alifunga hat-trick yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu wakati Tottenham Hostpur wakiibuka na ushindi wa 4-3 dhidi ya Leicester City msimu wa 2014-15. Na akafunga nyingine wakati akiisaidia Spurs kuifumua Bournemouth 5-1.

Msimu wa 2016-17 ulishuhudia Kane akifunga hat-trick nne. Akifunga wakati Spurs ikiibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya West Bromwich Albion na Stoke City akifuatia na mabao yake manne wakati wakishinda 6-1 dhidi ya Leicester City. Kane akafunga tena hat-trick yake ya nne kwenye msimu wakati wakiibuka na ushindi wa 7-1 dhidi ya Hull City.

Hat-trick yake dhidi ya Burnley na Southampton msimu wa 2017-18 ilimfanya Kane kufuata nyayo za Les Ferdinand, Ian Wright, Didier Drogba na Wayne Rooney kuwa mchezaji aliyefunga hat-trick kwenye mechi mbili mfululizo.

## 4. THIERRY HENRY (ARSENAL) - 8

Henry alifunga hat-trick yake ya kwanza msimu wa 2000-01 wakati Arsenal wakishinda 6-1 dhidi ya Leicester City. Huku hat-trick yake ya pili akifunga msimu wa 2002-03, wakati Mfaransa huyo alipoisaidia timu yake kupata ushindi wa 3-1 dhidi ya West Ham United.

Straika huyo wa zamani wa Arsenal alifunga hat-trick ya tatu na ya nne kwenye Ligi Kuu msimu wa 2003-04, wakati akiwasaidia 'Washika Bunduki' hao kuichapa Liverpool 4-2 na pia wakati wakiifunga Leeds United 5-0.

Sawa na msimu huo uliopita, Henry akafunga tena msimu wa 2004-05 kwa hat-trick mbili zaidi dhidi ya Portsmouth na Norwich City. Akafunga tena dhidi ya Middlesbrough na Wigan Athletic.

## 3. ROBBIE FOWLER (LIVERPOOL / LEEDS) - 9

Fowler alifunga hat-trick yake ya kwanza wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 4-2 dhidi ya Southampton msimu wa 1993-94. Baada ya hat-trick dhidi ya Chelsea msimu uliofuata, mshambuliaji huyo alifunga tena hat-trick msimu wa 1995-96 dhidi ya Bolton na Arsenal.

Fowler akafunga tena wakati Liverpool ikishinda 5-1 dhidi ya Middlesbrough. Msimu wa 1998-99, akatupia tena dhidi ya Aston Villa na Southampton.

Alitupia hat-trick ya nane wakati Liverpool wakiifunga Leicester City msimu wa 2001-02 kabla ya kufunga hat-trick yake ya tisa wakati Leeds United wakipata ushindi wa 3-0 dhidi ya Bolton Wanderers.

## 2. ALAN SHEARER (BLACKBURN ROVERS / NEWCASTLE UNITED) - 11

Kwa kipindi cha miongo miwili rekodi ya Alan Shearer ya kufunga hat-trick 11 kwenye Ligi Kuu haikufikiwa na mchezaji yeyote.

Shearer alifunga hat-trick yake ya kwanza wakati Blackburn Rover wakitoka sare ya 3-3 dhidi ya Leeds United. Akafunga tena dhidi ya Queens Park Rangers, West Ham United na Ipswich Town.

Msimu wa 1995-96, Shearer alikuwa mchezaji wa kwanza hadi leo hii kufunga hat-trick tano kwa msimu mmoja. Mchezaji huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England akafunga tena hat-trick dhidi ya Coventry City, Nottingham Forest, West Ham United, Bolton Wanderers na Tottenham Hotspur.

Shearer alifunga hat-trick yake ya 10 kwenye Ligi Kuu wakati Newcastle United ikiibuka na ushindi wa 4-3 dhidi ya Leicester City msimu wa 1996-97. Na mabao yake matano wakati wa ushindi wa 8-0 dhidi ya Sheffield United msimu wa 1999-2000 yakamfanya kuwa mchezaji wa kwanza baada ya Andy Cole, kufunga mabao matano kwenye mchezo mmoja wa Ligi Kuu.

## 1. SERGIO AGUERO (MANCHESTER CITY) - 11

Raia huyu wa Argentina alifunga hat-trick yake ya kwanza msimu wa 2011-12 wakati Manchester City, ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Wigan.

Aguero alilazimika kusubiri kwa miaka mitatu kufunga tena hat-trick wakati City ikishinda 4-1 dhidi ya Tottenham Hotspur msimu wa 2014-15. Halafu akafunga tena hat-trick dhidi ya Queens Park Rangers.

Msimu wa 2015-16, Aguero alifunga mabao matano wakati City ikiibuka na ushindi wa 6-1 dhidi ya Newcastle United.

Akafunga tena dhidi ya Chelsea, dhidi ya Watford, Newcastle United na Leicester City msimu wa 2017-18.

Akafunga nyingine dhidi ya Huddersfield, Arsenal na Chelsea.

Aguero sasa ameifikia rekodi ya Alan Shearer iliyodumu kwa miongo miwili ya kufunga hat-trick nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya England.

## Nukuu

"Napenda mageuzi yake, anatengeneza nafasi kuzunguka boksi ni wa kipekee, kulikuwa na vivuli vya Lionel Messi ndani yake na ninapenda mtu ambaye anaweza kufunga, lakini akiweza kutoa pasi za mwisho. Huyo ni mchezaji aliyekamilika. Ndiyo maana wote tunatamani na ndicho tunachokihitaji kutoka kwa wachezaji," **Arsene Wenger aliiambia beIN Sports, akimfananisha Mo Slaha na Messi.**



"Kocha ajaye wa Ufaransa anaweza kuwa Zizou [Zinedine Zidane]. Kwa upande mmoja au mwingine, anaweza kuwa yeye, " **Kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps ambaye amekuwa akiinoa timu hiyo tangu mwaka 2012.**



"Kwa nini ningetaka kuondoka? Bado nina miaka miwili katika mkataba wangu, timu inaendelea kupata maendeleo. Msimu huu, lengo ni Ligi ya Mabingwa. Na kipaumbele changu ni PSG, kwa jitihada kubwa kila wiki. Lengo mara zote ni kushinda mechi ijayo," **Neymar aliliambia Jarida la France Football akikana lengo la kujiunga na Barcelona ama Real Madrid kwa sasa.**



# WANAOSIKILIZIA SOKONI USAJILI WA DIRISHA DOGO



BUSWITA

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, Yanga ndiyo inaonekana iko 'bize' zaidi kuliko klabu nyingine yoyote ile.

**Tayari imetia kibindoni saini za wachezaji Ditram Nchimbi kutoka Polisi Tanzania alikokuwa akicheza kwa mkopo akitokea Azam FC, Adeiyum Selemani kutoka JKT Tanzania, Tariq Seif, huku Ofisa Mhamasishaji, Antonio Nugas alijigamba kuwa huo ni usajili wa rasharasha tu, masika bado yanakuja.**

Hii inaonyesha kuwa Yanga bado ina hamu ya kuendelea kusajili, na tayari imeshamshusha straika kutoka Gor Mahia raia wa Ivory Coast, Yikpe Gnamien ambaye inaweza kumtambulisha muda wowote.

Klabu zilizobaki zinaonekana kama vile zimeridhika na usajili wao wa mwanzo wa msimu, ingawa inaonekana baadhi zitasajili wachezaji wachache tu wa kuongezea nguvu.

Ofisa Mtendaji wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' amesema kuwa klabu yao itasajili wachezaji wawili tu ili kuziba mapengo iliyonayo.

Kwa upande wa Simba, taarifa zinaeleza kuwa huenda ikasajili straika mmoja tu kutoka nje ya nchi, au ikizidi basi na beki mmoja wa kati, huku kiungo mkabaji kutoka Polisi Tanzania, Baraka Majogolo akitajwa pia kuwindwa, hata hivyo, zipo taarifa zinaeleza kuwa huenda Simba ikaongeza wachezaji na kufikia watatu.

Kiungo huyo mkabaji, alionyesha uwezo mkubwa kwenye kikosi cha Kilimanjaro Stars nchini Uganda kwenye mechi moja tu aliyocheza dhidi ya Kenya, akiingia kipindi cha pili, Tanzania Bara ikipoteza kwa mabao 2-1.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, yeye amesema kuwa hatoongeza mchezaji yeyote yule kwenye kikosi chake kwa sababu waliopo wanatosha na wanafanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Thobias Kifaru, msemaji wa Mtibwa Sugar, amebainisha kuwa klabu hiyo haina haja ya kusajili mchezaji yoyote kipindi hiki cha dirisha dogo kwa sababu ina wachezaji mahiri na wanaoweza kupambana hadi mwisho wa msimu huu na kama ikilazimu basi watamulika kutoka U-20.

Kwa maana hiyo ukiondoa Yanga, klabu nyingi hazina mahitaji makubwa kwenye dirisha hili, hivyo kuwa na wachezaji wachache tu wanaohitajika. Kwa sasa kuna majina machache tu ya baadhi ya wachezaji ambao wanahusishwa kuondoka kwenye klabu zao na kusajiliwa na klabu zingine, haya hapa...

**1. BAKARI MWAMNYETO- COASTAL UNION**

Huyu ni beki wa kati wa Coastal Union ya Tanga ambaye tangu alipochaguliwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars na hata Kilimanjaro Stars, kiwango chake kimezidi kukua, akipata pia uzoefu na kila mechi anayocheza amekuwa akifanya vema kiasi cha kumezewa mate na klabu mbalimbali kubwa.

Mwamnyeto ambaye amebakisha mkataba wa mwaka mmoja na Coastal, amekuwa akiwaniwa na klabu zote kubwa nchini, Simba, Yanga na Azam FC, ingawa klabu yake inasema kuwa kwa sasa haitomruhusu kusajiliwa na klabu ya hapa nchini, labda nje ya nchi.

Pamoja na hayo, hadi Januari 15 mwakani kipindi cha kufungwa kwa dirisha dogo, chochote kinaweza kutokea.

**2. BARAKA MAJOGOLO- POLISI TANZANIA**

Polisi Tanzania imempoteza Nchimbi aliyetimkia Yanga, lakini huenda pia ikampoteza kiungo wake mkabaji, Baraka Majogolo ambaye anadaiwa kuwaniwa kwa udi na uvumba na klabu ya Simba.

Taarifa zinaeleza kuwa Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Selemani Matola ndiye anayeishinikiza Simba kusajili kiungo huyo ambaye alionyesha uwezo mkubwa kwenye mechi moja tu aliyocheza nchini Uganda ya kutafuta mshindi wa tatu, Kilimanjaro Stars ikicheza dhidi ya Kenya na kufungwa mabao 2-1. Majogolo akiingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Jonas Mkude, aliituliza timu na kubadilisha kabisa mchezo, Kili Stars ikaanza kuishambulia Kenya na kupata bao la kufutia machozi dakika ya 85.

**3. CLEOPHACE MKANDALA- PRISONS**

Ni mmoja wa viungo washambuliaji chipukizi ambaye kama atajitunza anaweza kuwa staa mkubwa nchini.

Mkandala ambaye anaichezea Prisons, alikuwapo kwenye kikosi cha Kilimanjaro Stars kilichocheza michuano ya Kombe la Chalenji nchini Uganda.

Ni mchezaji anayedaiwa kutaka kusajiliwa na Yanga kipindi hiki cha dirisha dogo.

Kocha Mkuu wa Prisons, Mohamed Rishard 'Adolf', amesema kuwa amesikia taarifa hizo na kama Yanga wanamtaka basi wafuate taratibu na yeye atamruhusu tu kujiunga na klabu hiyo bila tatizo lolote.

**4. YUSUPH MHILU- KAGERA SUGAR**

Huyu ni winga wa zamani wa Yanga. Huwezi kuamini kuwa msimu huu amekuwa kwenye kiwango kikubwa ambacho hajapata kuwa nacho tangu aanze kucheza Ligi Kuu.

Msimu uliopita aliichezea Ndanda kwa mkopo akitokea Yanga, akifunga mabao matatu, na msimu huu amesajiliwa na Kagera Sugar kama mchezaji huru.

Tayari ana mabao matano kibindoni akikimbizana na mastraika akina Meddie Kagere anayeongoza ufungaji akiwa na mabao nane.

Inadaiwa kuwa winga huyo wa kulia alimvutia hata Ofisa Mtendaji wa Simba, Senzo Mazingisa alipomshuhudia kwenye mechi kati ya Simba dhidi ya Kagera Sugar, Uwanja wa Kaitaba, japo Simba ilishinda mabao 3-0. Mhilu anadaiwa kutakiwa na Simba ili kuongeza nguvu kwenye safu ya mawinga.

**5. PETER MAPUNDA- MBEYA CITY**

Ni winga mwenye uwezo wa kucheza kulia na kushoto. Ana kasi na uwezo mkubwa wa kufunga mabao.

Ana sifa zingine za ziada ambazo ni kupiga faulo za hatari na pia mpiga penalti ambaye ni nadra sana kukosa. Ameshafunga mabao matano mpaka sasa. Kutokana na klabu yake kusuasua kwenye mwenendo wa ligi ana uwezekano mkubwa wa kuondoka, huku Azam FC ikitajwa kuwa inafanya mipango hiyo. Azam inaonekana imenogewa na wachezaji wa Mbeya City, baada ya kufanikiwa kwa Idd Selemani 'Nado' na sasa Mapunda.

**6. PIUS BUSWITA- YANGA**

Habari zinasema kuwa JKT Tanzania inamchukua Pius Buswita kutoka Yanga ikiwa ni makubaliano ya pande zote mbili baada ya timu hiyo kumsajili Selemani Adeiyum, hivyo ni kama vile wamebadilishana.

**7. MATHEO ANTONY- YANGA**

Kuna taarifa kuwa Matheo Antony anatarajiwa kujiunga na Polisi Tanzania, ikiwa ni mpango wa klabu ya Yanga kuwapoza kwa kopo maafande hao ambao wanalalamika juu ya kuchukuliwa kwa straika wao Ditram Nchimbi aliyekuwa akiicheza kwa mkopo akitokea Azam FC.

**NAJUA WAJUA**



EVERTON imemaliza mechi bila kuruhusu bao ('clean sheets') dhidi ya Arsenal kwa mara ya kwanza tangu Agosti 1978. Hiyo ni kufuatia matokeo ya sare tasa timu hizo ziliyoyapata juzi.

## SOKA

# NYOTA WANAOITIBULIA ARSENAL MSIMU HUU




SOKRATIS

**LONDON,** England

UMEKUWA ni msimu wa machungu kwa Arsenal na mashabiki wake. Kwa sasa wapo nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu kabla ya mechi za jana, na 'Washika Bunduki hao wameshindwa kuwa kwenye kiwango bora licha ya kufanya usajili wa nguvu.

**Hakuna mchezaji hata mmoja anayeonekana kuipigania timu na sasa ile nukuu maarufu aliyoitoa Thierry Henry inajidhihirisha wazi, ambapo alipata kusema, "Unahitaji mabega makubwa kuichezea Arsenal."**

Wachezaji kama Pierre-Emerick Aubameyang, Granit Xhaka na Alexandre Lacazette, hakuna hata mmoja anayeweza kujisifia kwa kiwango chake kilivyoisaidia timu.

Hapa tunawaangalia wachezaji wanne ambao wamechemka kabisa kuonyesha kiwango chao pale Arsenal msimu huu...

**4. DAVID LUIZ**

Pamoja na uzoefu wote alioupata akicheza katika ligi mbalimbali Ulaya, mlinzi huyu mwenye umri wa miaka 32, hajawa na msaada wowote kwa timu ambayo inaonekana imepwaya mno kwenye safu ya ulinzi. Bila shaka David Luiz hakuwa suluhisho la kudumu, lakini kwa sababu Arsenal ilishindwa kukamilisha dili la kumsajili beki wa Ufaransa, Dayotchanculle Upamecano, mkongwe huyo alionekana kama suluhisho la muda mfupi la kumaliza tatizo la ulinzi. Hata hivyo, mambo hayakwenda kama yalivyopangwa.

Arsenal imecheza mchezo mmoja tu bila kuruhusu bao msimu huu ikiwa na Luiz.

**3. SOKRATIS PAPASTATHOPOULOS**

Mlinzi huyu wa kimataifa wa Ugiriki alikuwa kwenye kiwango bora zaidi wakati akicheza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, chini ya kocha Jurgen Klopp, lakini hakuna shabiki anayeweza kusema beki huyo mwenye umri wa miaka 31 amekuwa bora zaidi kuliko Shkodran Mustafi kwa msimu.

Wakati wake wa uchezaji pale Dortmund ulikuwa bora zaidi na Arsenal wakaona wamefanya usajili wa nguvu. Sven Mislintat alifanya kazi kubwa kumleta London, lakini kwa sasa pengine anajilaumu.

Sokratis amekuwa akifanya makosa mengi ya wazi na kuigharimu Arsenal na ndio maana hata kocha wa muda, Freddie Ljungberg aliamua kumtema kwenye mchezo wake wa kwanza.

**2. NICOLAS PEPE**

Winga huyu wa zamani wa Lille alinunuliwa na Arsenal huku kukiwa na matumaini makubwa kwake. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 24, bado hajaonyesha kiwango chake. Pepe si tu kwamba amekuwa akihaha kupata dakika za kucheza, lakini uwapo wake dimbani haujawa na msaada wowote kwa timu.

Kwa nini mambo yamekuwa magumu kwa mchezaji huyo raia wa Ivory Coast? Kukosa kwake kipindi cha maandalizi ya msimu mpya na Arsenal kumeathiri kiwango chake na kujiamini.

Tangu dili la usajili wake lilipokamilika kati ya Lille na Arsenal, alilazimika kukosa kipindi cha maandalizi ya msimu mpya kwa sababu alikuwa kwenye majukumu na timu yake ya taifa.

"Naweza kusema kwamba, mwanzo wangu umekuwa hasi. Hasa kutokana na matarajio niliyojiwekea mwenyewe, nilitarajia mengi zaidi. Nilitarajia mengi zaidi na kufanya tofauti, lakini mambo yamekwenda tofauti kabisa. Ni kawaida watu kukushutumu kwa sababu sijaonyesha tofauti yoyote hadi sasa kwa kila mechi. Nawaelewa.

Pepe anajua kwamba, ameshindwa kufanya kile ambacho mashabiki walikuwa wakikitarajia kutoka kwake.


**1. MESUT OZIL**

Sasa ni msimu wa tatu, Washika Bunduki hao bado wanasubiri Mesut Ozil arudi kwenye kile kiwango cha msimu wa 2015/16. Ozil anaonekana ubora wake ni kama umeshamalizika na kwa sasa si yule wa kipindi kile.

Raia huyo wa Ujerumani, kiwango chake kimeporomoka na inaonekana wazi kwamba, uwezekano wa kukirudisha ni mgumu.

Ozil ndiye mshambuliaji pekee wa Arsenal ambaye hajachangia mabao hata mawili msimu huu.

TANGU alipoanza kucheza Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza Machi 2012, Raheem Sterling ameshinda penalti nyingi kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye ligi hiyo (penalti 17).



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika



TANGU kurekebishwa kwa muundo wa Ligi Kuu ya England msimu wa mwaka 1992-93, zaidi ya wachezaji 100 wamefunga hat-trick.

Uk. 16&17



# KLABU 5 BORA ULAYA 2019

**PARIS,** Ufaransa

RATIBA ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tayari imeshawekwa hadharani kwa msimu wa 2019-20. Hiyo ni pamoja na ile la Ligi ya Europa.

Bingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya (Liverpool) na yule wa Ligi ya Europa (Chelsea) zote zimefuzu kwenye hatua hiyo.

Pamoja na klabu nyingine zilizocheza zaidi ya mechi 45 kwenye mashindano hayo, ni Manchester City (England) na Paris Saint-Germain (Ufaransa) wameshinda mechi 40 kwa mwaka 2019, huku Liverpool ikifungwa mara tatu tu na kuwa klabu iliyopoteza mechi chache zaidi katika mashindano yote.

Makala haya yanakuchambulia klabu tano bora za Ulaya kwenye mwaka huu...

### 5. BAYERN MUNICH (UJERUMANI)

Miamba hao wa Bavaria wameshinda mechi zao saba mfululizo na wakiweka rekodi ya kutwaa taji la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kwa mara ya 29 msimu wa 2018-19.

Hata hivyo, utawala wao wa ligi ya nyumbani ulishindwa kuhamia Ulaya wakati walipofungwa na Liverpool katika raundi ya mtoano wa timu 16.

Licha ya Robert Lewandowski kufunga katika mechi 11 mfululizo tangu kuanza kwa ligi hiyo, Bayern Munich imekuwa na mwanzo tofauti kwa msimu wa 2019-20.

Baada ya kufungwa mara nne kwenye Ligi Kuu katika mechi 15, ikiwamo kichapo cha 5-1 na Eintracht Frankfurt kukaifanya klabu hiyo kuwa na kichapo kibaya zaidi kwenye Bundesliga kwa kipindi cha miaka 10.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Bayern ilishinda mechi zake zote sita kwenye hatua ya makundi.

### 4. JUVENTUS (ITALIA)

'Bianconeri' hao waliweka rekodi ya kushinda taji lao la nane mfululizo kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu wa 2018-19, lakini wakatolewa na Ajax hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwenye Serie A msimu huu, Juventus wanaongoza ligi pamoja na Inter Milan baada ya mechi 16. Miamba hao wa Italia waliongoza kundi lao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya lililokuwa na timu za Atletico Madrid, Bayer Leverkusen na Lokomotiv Moscow na kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16 kwa msimu wa sita mfululizo.

### 3. BARCELONA (HISPANIA)

Barcelona walishinda taji lao la nne la Ligi Kuu ya Hispania kwa misimu mitano iliyopita, lakini walishindwa kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya nne mfululizo, licha ya kushinda 3-0 dhidi ya Liverpool kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali.

Barcelona ilifungwa mara tano mwaka huu kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na sasa inaongoza msimamo kwa pamoja na Real Madrid baada ya mechi 16.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, Barcelona walikuwa moja ya timu sita ambazo hazijafungwa kwenye hatua ya makundi. Huku nahodha wao Lionel Messi akiwa mchezaji wa kwanza kuzifunga timu 34 tofauti kwenye mashindano hayo.

### 2. MANCHESTER CITY (ENGLAND)

Timu pekee kwenye Ligi Kuu ya England kufikisha pointi 100 kwa msimu. Manchester City walishinda mechi 14 za kwanza na kuwashinda Liverpool kutwaa taji lao la nne kwenye Ligi Kuu msimu wa 2018-19. City ilifungwa na Tottenham Hotspur kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiwango cha City kwenye Ligi Kuu msimu huu kimekuwa tofauti, wakati bingwa huyo mtetezi akishika nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Tangu kuondolewa kwao kwenye hatua ya makundi mara mbili msimu wa 2011-12 na 2012-13, City ilifika hatua ya mtoano kwa mara ya saba mfululizo kutoka kwenye kundi lililokuwa na za Atalanta, Shakhtar Donetsk, na Dinamo Zagreb. Kwa ushindi wake wa mechi 44 kutoka michezo 56 kwenye mashindano yote mwaka 2019, City imeshinda mechi nyingi zaidi Ulaya ikiwa sawa na asilimia 79.

### 1. LIVERPOOL (ENGLAND)

Licha ya kushinda mechi zake zote tisa zilizopita kwenye ligi na kupoteza mmoja kwa msimu wote, Liverpool ilishindwa kuwapiku Manchester City kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu uliopita.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool ilipindua meza baada ya mchezo wa kwanza wa nusu fainali kufungwa 3-0 dhidi ya Barcelona kabla ya kwenda kucheza fainali dhidi ya Tottenham Hotspur na kushinda taji lao la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya na la kwanza tangu mwaka 2005.

Liverpool imeendelea kuwa na msimu mzuri, ikiwa haijafungwa katika mechi 16, huku ikishinda 15. Wanawaongoza Leicester City kwa tofauti ya pointi 10 na bingwa mtetezi kwa tofauti ya pointi 11, ambao wapo mchezo mmoja mbele.

Liverpool imefungwa mechi tatu kati ya mechi 51 ilizocheza kwenye mashindano yote mwaka 2019, lakini juzi ikiichapa Flamengo ya Brazil bao 1-0 kwenye fainali ya Klabu Bingwa Dunia na kutwaa kombe hilo.

**USILOLIJUA**



USHINDI wa bao 1-0 Liverpool iliyoupata dhidi ya Flamengo kwenye fainali ya Klabu Bingwa Dunia juzi, hii inakuwa ni mara ya pili pekee kwa klabu kutoka England kuweza kuifunga klabu kutoka Brazil kwenye mechi ya kimashindano, baada ya Manchester United nayo kushinda 1-0 dhidi ya Palmeiras mwaka 1999 kwenye fainali ya Kombe la Mabara.



# Mchakato waanza msitu kuhifadhiwa TFS

**NA Nebart Msokwa,** CHUNYA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya imetembelea na kuridhishwa na mipaka ya Msitu wa Kambikatoto wilayani Chunya ambao Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inakusudia kuuhifadhi kisheria ili kuokoa mazingira.

Kamati hiyo ilitembelea msitu huo mwishoni mwa wiki ikiwa ni utekelezaji wa ushauri uliotolewa na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa kwenye kikao cha Novemba 27, mwaka huu ambao waliishauri kujiridhisha ili kuepuka kuibua migogoro.

Wananchi hao walithibitisha kushirikishwa katika hatua zote na kwamba na wao waliridhia ili kuokoa msitu hiyo isiharibiwe na wavamizi ambao huwa wanavuna miti kinyemela kwa ajili ya mbao na mkaa.

Mmoja wa wananchi hao, Petro Mwakipandule ambaye ni Mkazi wa Kata ya Bitimanyanga, aliiambia kamati hiyo kuwa msitu huo ulikuwa unasimamiwa na vijiji vinavyouzunguka, lakini usimamizi ulikuwa hafifu kutokana na kutokuwa na rasilimali.

Alisema kutokana na hali hiyo ndio maana walikubali kuukabidhi kwa TFS ambayo ni taasisi imara na yenye rasilimali ili ishirikiane nao kuutunza. "Sisi ndio tunanufaika na misitu hii, ninyi viongozi yawezekana hamna hata ndugu katika eneo hili, lakini mnafanya hivyo kwa sababu ya kutuhurumia sisi na vizazi vyetu, tulikubali msitu huu uhifadhiwe kwa sababu ndio vyanzo vya maji tunayotumia," alisema Mwakipandule.

Diwani wa Kambikatoto, Christopher Mchafu, alisema lengo la serikali ni zuri, na kwamba mchakato wa kuuhifadhi msitu huo ulianza mwaka 2006, lakini wananchi walikuwa bado hawana uelewa wa kutosha.

Alisema kutokana na elimu iliyokuwa inatolewa na maofisa wa TFS kwa muda mrefu, umefika wakati wananchi wake wakaelewa na wakakubali kuwa msitu huo ni muhimu kuhifadhiwa.

Hata hivyo alisema katika kata hiyo vijiji vyote vina mpango wa matumizi bora ya ardhi, ambapo baadhi ya maeneo yametengwa kwa ajili ya misitu, makazi, kilimo na maeneo ya kuchungia mifugo.

"Sisi hatuna pingamizi lolote kwa TFS kuhifadhi msitu huu maana tunaamini utakuwa salama zaidi kutokana na wenzetu kuwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi misitu kuliko ilivyo kwa vijiji," alisema Mchafu.

Kaimu Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, alisema waliamua kuuhifadhi kwa sababu umekuwa ukivamiwa mara kwa mara na kuharibiwa ikolojia yake. Alisema msitu huo una ukubwa wa hekta 100,008 na kwamba awali wakati wanapima walikosea wakayaingiza na maeneo ambayo yalikuwa hayatakiwi na hivyo kuufanya kuwa na ukubwa wa hekta 179,078.

Alisema msitu huo unahifadhi vyanzo vya maji vya mito mbalimbali inayomwaga maji katika Ziwa Rukwa na Mto Ruaha Mkuu pamoja na vyanzo vya maji yanayotumiwa na wananchi wa kata hizo mbili.

"Lakini msitu huu ni ushoroba (njia ya kupita wanyama) unaounganisha hifadhi za Ruaha na Katavi, sasa tusipochukua hatua utaharibiwa na wanyama watakuwa wanashindwa kupita na itakuwa vurugu," alisema Lupembe.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama, alisema ni kuimarisha ulinzi wa msitu huo, serikali inakusudia kujenga Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Gereza la Wilaya.

Aliwataka wananchi hao kuwa walinzi wa misitu hiyo ili waendelee kupata maji kutoka kwenye vyanzo vya maji vilivyomo msituni humo na kupata mvua ya uhakika.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akizungumza na wananchi wa Kata ya Kambikatoto wilayani Chunya mwishoni mwa wiki, kuhusu umuhimu wa kutunza Msitu wa Kambikatoto ambao TFS wanakusudia kuuhifadhi kisheria. **PICHA : NEBART MSOKWA**

# Waanza kukamilisha madarasa wanafunzi 1,665 kidato kwanza

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WILAYA ya Mbarali imeanza kushirikiana na wadau wa elimu kukamilisha vyumba vya madarasa 36 kwa ajili ya wanafunzi 1,665 wa kidato cha kwanza ambao majina yao yamezuiliwa kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri, Kivuma Msangi, waliitisha harambee mwishoni mwa wiki kwa ajili ya kukusanya fedha hizo.

Mfune alisema lengo la zoezi hilo ni kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanaanza masomo mapema ili wasipishane na wenzao ambao majina yao yametangazwa na wanatarajiwa kuanza masomo mapema mwezi Januari. Alisema mwaka huu pamoja na kwamba ndio wilaya inayoongoza kwa kuwa na upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, lakini kuna utofauti na ilivyokuwa katika mwaka wa masomo wa 2018/2019.

"Mwaka uliopita tulikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 37 mwaka huu tuna upungufu wa vyumba vya madarasa 36 lakini tayari tumeanza ujenzi wa shule mpya tisa ambazo baadhi lazima tuzifungue mwakani," alisema Mfune.

Aliwaomba wadau mbalimbali wa elimu wilayani humo kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha vyumba hivyo vinakamilika kwa wakati.

Alisema kwa sasa serikali inapotekeleza sera ya elimu bila malipo wananchi wamekuwa na mwamko mkubwa wa kuwapeleka watoto wao shuleni hali ambayo imekuwa pia changamoto kwa kuzalisha tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa.

Alisema mbali na upungufu huo wa vyumba vya madarasa pia kuna upungufu wa madawati kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu na hivyo akawataka wananchi kushiriki pia kuchangia pale wanapokuwa na kibali.

# Watoto wahitimu mafunzo ya maarifa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO 1,200 wenye umri kati ya miaka mitatu na mitano kutoka katika mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam, wamehitimu mafunzo ya kujifunza maarifa kupitia michezo (Play lab) yanayotolewa na Shirika la Brack kupitia Mradi wa Makuzi na Malezi ya Watoto.

Watoto hao walihitimu mafunzo hayo mwishoni mwa wiki ambapo kila mkoa ulikuwa na watoto 600 na vituo 20 vyenye watoto 30 kila kimoja na kwa Mkoa wa Mbeya mradi huo unatekelezwa katika halmashauri mbili za Wilaya ya Mbeya.

Akizungumza wakati wa mahafali ya watoto hao yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Meneja wa Mradi huo, Crepton Madunda, alisema mradi huo unalenga kuwafundisha watoto hao maarifa mbalimbali kupitia michezo mbalimbali.

Alisema lengo la mradi ni kuwajenga watoto hao kimwili, kiakili, lugha na mawasiliano ili wanapofikia umri wa kujiunga na elimu ya awali ambayo ndiyo inaanza kutambuliwa na serikali katika mfumo wa elimu ya msingi wawe na uelewa mkubwa.

Madunda alisema Brack inatekeleza mradi huo kwa kushirikiana na wazazi ambao wanashiriki katika uandaaji wa baadhi ya vifaa vya kufundishia vinavyotokana na malighafi za kawaida zinazopatikana kwenye mazingira wanayoishi.

"Lakini tunawashirikisha wazazi ili baadaye mradi ukifikia ukomo tuwakabidhi waendelee kuviendesha vituo hivi, tulianzisha mradi baada ya kubaini kuwa mfumo wa elimu yetu unawabagua watoto wa umri huu wa kuanzia miaka sifuri mpaka mitano," alisema Madunda.

Vilevile, alisema kwa sasa wameshirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuandaa mtaala wa kufundishia watoto wa umri huo ambao alidai upo katika hatua za mwisho na utakuwa unatumika kwenye vituo vyote vinavyolea watoto.

Akizungumza kabla ya kuwakabidhi watoto 600 wa Mkoa wa Mbeya waliohitimu, Ofisa Elimu Msingi wa Jiji la Mbeya, Christina Mwakyusa, alilishukuru Shirika la Brack kwa kubuni mpango huo ambao alisema unasaidia kuonyesha vipaji vya watoto.

Alisema watoto wanajifunza ujasiri pamoja na shughuli mbalimbali za mikono ambazo nyingi ni za ubunifu ikiwamo kuchora, kupika, kuandika kusoma pamoja na kuandika.

Aliliomba shirika hilo kuwajumuisha pia watoto wenye ulemavu kwenye vituo hivyo badala ya kuwatenga ili na wao wajifunze kupitia elimu jumuishi ambayo inasaidia kupunguza unyanyapaa.

"Wakijumuishwa hata hali yao ya ulemavu inapungua na wanakuwa wanajisikia kuwa wapo sawa na wenzao ambao hawana ulemavu, hivi vituo vi muhimu sana na tunawaomba mwendelee navyo.

Nao baadhi ya wazazi wa watoto waliohitimu walilishukuru shirika hilo kwa kuanzisha vituo hivyo na kwamba wao wataendelee kutoa ushirikiano mpaka watakapoachiwa kwa ajili ya kuviendeleza.

Mmoja wa wazazi hao, Leah Ifugo, alisema awali mtoto wake alikuwa hakubali kubaki kwenye kituo hicho kwa kutokubali kubaki wakati anapompeleka na kwamba baada ya kukaa kwa muda na walimu alibadilika.





# Kituo cha mabasi kuwa cha kimataifa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MRADI wa ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi mkoani Dodoma utakapokamilika utakuwa na huduma kama zilizopo kwenye viwanja vya ndege vya kimataifa.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa kampuni ya ujenzi ya Mohammedi Builders Ltd, Mohammedi Jafrej, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea mradi huo wa kituo cha mabasi uliopo eneo la Nzuguni jijini hapa.

Jafrej alisema mradi huo utakapokamili utakuwa na huduma za kisasa mfano wa huduma za viwanja vya ndege kutokana na uwepo wa maeneo maalumu ya huduma kwa abiria na wananchi wengine.

Alisema kituo hicho tofauti na vingine kitakuwa na eneo maalumu la VIP, ambalo litakuwa na huduma zote hapo bila kuingiliana na watu wengine wanaotumia kituo hicho.

Aliongeza kuwa kutakuwa na kumbi kubwa tatu zenye huduma zote ndani bila kuingiliana zitakazotumika kwa abiria wengine na wananchi wakisubiri usafiri au wageni wao.

Pia alisema eneo hilo litakuwa na uwezo wa kuingiza mabasi zaidi ya 300, kwa wakati mmoja pamoja na eneo la maegesho ya magari mengine ndani na nje ya kituo hicho.

Kuhusu ujenzi wa kituo hicho, alisema ulitarajiwa kukamilika Desemba 2019, lakini kutokana na kuongezewa eneo la ujenzi unatarajiwa kukamilika Februari 2020.

Alitaja baadhi ya maeneo yaliyoongezwa kwenye mkataba ni miundombinu ya barabara ndani na nje ya kituo hicho ambayo itatumika kwa ajili ya kuingia na kutoka. Jafrej alibainisha maeneo mengine waliyoongezewa katika mkataba ni pamoja na maegesho ya magari ndani ya kituo hicho na wanaendelea na ujenzi ili kukamilisha ndani ya wakati.

Daudi Ezekiel, mkazi wa Nzuguni aliomba mradi huo utakapokamilika kuwekwe mikakati ya kutunzwa ili kutumika kwa malengo na mipango iliyopangwa ndani ya kituo hicho.

Aliuomba uongozi wa jiji kuweka mikakati ya wafanyabiashara ndogondogo pamoja na wajasiriamali wengine ili kuepuka vurugu ndani ya kituo hicho.

"Tunaomba kituo kitakapokamilika pawepo watu maalumu getini kwa ajili ya kuwasaidia wasiojua eneo la kupata huduma husika, nasikia kutakuwa na hoteli kubwa humo ndani na huduma zingine nadhani si kila atakayefika hapo atahitaji kusafiri wengine watakwenda kupata huduma," alisema.




Baadhi ya mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Mohammed Builders Ltd wakiendelea na ujenzi wa kituo kikuu cha kisasa cha mabasi jijini Dodoma jana. Kituo hicho kinatarajiwa kukamilika Februari 2020 na kitakuwa na huduma kama za uwanja wa ndege wa kimataifa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Uhaba misitu waikosesha fedha Tanzania

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UHABA wa misitu katika baadhi ya maeneo nchini umetajwa kuwa ni sababu ya Tanzania kukosa mamilioni ya fedha zinazotolewa na kampuni kubwa duniani zinazozalisha hewa chafu za viwandani.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Miradi wa Shirika la Lead Foundation, Njamasi Chiwanga, wakati wa kikao cha pamoja na viongozi wa vijiji wakiwamo watendaji na wenyeviti katika Tarafa ya Mima na Kibakwe, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Alisema kwa mujibu wa sheria za kimataifa za uhifadhi wa mazingira, kampuni kubwa zenye viwanda duniani zinatakiwa kutoa sehemu ya faida kufadhili miradi ya mazingira.

Alisema kutokana na hali hiyo, Shirika la Lead Foundation limeteua wakulima 18, kutoka katika kila kijiji katika tarafa hizo za Kibakwe na Mima kwa ajili ya kustawisha miti 200,000 kupitia njia ya kisiki hai.

Alisema shirika hilo kwa kushirikiana na vikundi hivyo 18, vya wakulima wa mfano wamefanikiwa kupanda jumla ya miti milioni 3.5.

Waziri wa Elimu mstaafu katika serikali ya awamu ya kwanza chini ya Hayati Julius Nyerere na Askofu mstaafu wa kanisa Aglikani Tanzania Dayosisi ya Mpwapwa, Simon Chiwanga, alisema uharibifu wa misitu katika nchi ni mkubwa.

Askofu huyo aliitaka jamii kutunza miti ili kukomboa ardhi iliyochakaa huku akidai misitu ni rasilimali muhimu hususani katika ulimwengu wa sasa ambapo kumekuwa na biashara ya uuzaji wa hewa chafu (Cabon Trade).

Aliwataka wananchi kustawisha miti kwa wingi kwani ni biashara kubwa na waone kama ni mgodi wa almasi licha ya mahitaji yao ya leo ya kuni, miti ya kujengea, pamoja na mbao.

Alisema kustawisha miti kwa kisiki hai ni gharama nafuu kuliko kupanda miti hasa katika maeneo kame, huku akisisitiza hakuna kisingizio na kuzitaka serikali za vijiji kuiga mfano wa Rais John Magufuli kutoka na uchungu alionao kwa ukombozi wa watu na maendeleo ya nchi.

"Kila mtu katika serikali ya kijiji, kata, tarafa aone uchungu wa uharibifu wa mazingira na watu ukali ule anautumia Rais Magufuli na mamlaka kuthibiti wakorofi wanaoharibu miti," alisema Askofu Chiwanga.

Mmoja wa wakulima walio katika kikundi cha wakulima wa mfano, Harold Madihi, aliwataka viongozi wa vijijini kusimamia mradi huo ipasavyo ili kuja kupata manufaa siku za baadaye.

## Vyanzo chakula Dodoma vyatajwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UPATIKANAJI wa chakula katika Jiji la Dodoma unategemea uzalishaji wa ndani wa mazao ikiwamo uingizaji wa vyakula kutoka mikoa mbalimbali.

Hayo yamebainishwa na Mshauri wa Kilimo Sekretarieti ya Mkoa, Bernard Abraham, wakati wa kuwasilisha mada ya hali ya upatikanaji wa chakula katika kikoa cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Abraham alisema hali ya upatikanaji wa chakula imekuwa ikifanyika kila mwezi na wataalamu waliopo ngazi ya halmashauri na mkoa kufuatilia mwenendo katika kaya na masoko, hata na hivyo tathmini imebainisha kuwa upatikanaji wa chakula ni wa kuridhisha.

"Hali ya upatikanaji wa chakula kwa Mkoa wa Dodoma ni ya kuridhisha ingawa kumekuwapo na ongezeko la bei kwa baadhi ya vyakula," alisema Abraham.

Alisema kumekuwa na ongezeko la bei ya baadhi ya vyakula ilhali kwa bidhaa nyingine haijabadilika kwa kiwango kikubwa.

Akitolea ufafanuzi kwa baadhi ya bidhaa za vyakula, Abraham alisema kwa Novemba unga wa dona unauzwa kati ya Sh. 1,300 hadi Sh. 1,500 ikilinganishwa na Sh. 1,200 iliyouzwa mwezi Julai wakati Sembe imeuzwa kwa kati ya Sh. 1,600 hadi 1,700 kwa kila mwezi Novemba ikilinganishwa na Sh. 1,200 iliyouzwa Julai.

Alisema kwa mchele Novemba umeuzwa kwa kati ya Sh. 1,800 hadi 2,500 kwa Novemba ikilinganishwa na Sh. 1,800 hadi 2,000 mwezi Julai, wakati maharagwe ni Sh. 2,400 hadi 2,600 kwa Novemba na Julai yaliuzwa kati ya Sh. 1,800 hadi 2,000.

Alisema mahindi yameuzwa kwa Sh. 900-hadi 1,000 kwa kilo mwezi Novemba ukilinganisha na Sh. 650 Julai wakati bei ya muhogo imebakia ile ile ya Sh. 1,000 kwa fungu.

Hata hivyo, alisema RCC, ilipitisha kwa kauli moja maazimio ya utekelezaji ikiwamo kila halmashauri kuwa na mkakati wa kuwa na mazao ya kudumu na yenye thamani kubwa.

Akisoma maazimio, Katibu Tawala Mkoa, Maduka Kessy, alisema wamekubaliana kuchukua hatua za kufufua mabwawa, kuanzisha mabwawa mapya ili kuongeza uvunaji wa maji ya mvua na kupanua kilimo cha umwagiliaji.



## HABARI ZANZIBAR

# Miongozo yaja kuwalinda vijana dhidi ya udhalilishaji

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idrissa Muslim Hijja, amesema wizara hiyo imeandaa miongozo maalum kwa ajili ya kutoa stadi za maisha na afya ya uzazi kwa vijana waliopo shule na nje ya shule ili kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

Alibainisha hayo alipokuwa akizungumza katika uzinduzi wa mradi wa kuimarisha stadi za maisha na afya ya uzazi kwa vijana hafla ambayo ilifanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mtakwimu uliopo Mazizini Mjini Unguja.

Alisema miongozo hiyo itaweza kuwasaidia kujikinga na vitendo hivyo, ambapo vijana wamekuwa wakipewa elimu mara kwa mara ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kujiepusha na vishawishi ambavyo vitawasababisha kujiingiza katika makundi hatarishi.

Alisema katika kipindi cha kwanza cha mradi huo uliweza kuwafikia wanafunzi 14,347, ambapo vijana walikuwa 13,460 na wazazi 887 kutoka shule 19 zikiwamo 12 Unguja na Pemba shule saba na walimu 57.

Dk. Hijja alizipongeza uongozi wa jumuiya ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (Zapha +) kwa kuwapa elimu vijana na namna ya kujilinda na vitendo vya udhalilishaji na kujiepusha na maradhi ya kujamiiana, kujua athari za mimba za utotoni na kutambua athari za dawa za kulevya. Aidha, alisema kuwa imani yake ni kuona awamu ya pili ya mradi huo ni fursa ya kuendeleza mazuri yaliyotekelezwa na mradi na kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza ili kujenga vijana kulinda na mila na desturi zinazokubalika.

Alisema serikali inatambua mchango wanaoutoa jumuiya hiyo, katika kupambana na VVU ambapo kwa sasa wameonyesha kuwa wapo katika mstari wa mbele katika uelewa juu ya umuhimu wa upatikanaji wa elimu ya afya ya uzazi na stadi za maisha kama ni sehemu ya kinga dhidi ya VVU na Ukimwi, maradhi ya kujamiiana, dawa za kulevya na udhalilishaji.

Mratibu wa mradi huo, Mussa Tanu Juma, alisema lengo la mradi huo ni kujenga uwelewa na kuimarisha elimu ya afya ya uzazi na upatikanaji wa huduma kwa vijana ili kujikinga na maradhi na waweze kutumia vipaji vyao katika kujiendeleza na kuwa watu bora.

Aidha, alisema kufuatia elimu hiyo wataweza kuepuka tabia hatarishi na vitendo vya udhalilishaji, kupungua kwa idadi ya mimba kwa watoto maskulini na uwezo wa wanafunzi kimasomo kuengezeka.

Kwa upande wao washiriki wakitoa michango katika hafla hiyo, walisema kuwa katika mradi uliokwisha watoto wengi walifikiwa na mradi huo, hivyo aliahidi kuendeleza kutoa elimu ili kuweza kupunguza maambukizi na vitendo vya udhalilishaji na kuja kuwa viongozi wazuri.



Mjumbe wa Maskani ya Kachorora, Suleiman Omar 'Ganzi', akitoa nasaha juu ya umuhimu wa wanachama wa CCM kuwarithisha watoto itikadi na fikra za ukombozi kabla na baada ya Mapinduzi ili wakue wakijua historia halisi ya nchi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sekta ya anga yachochea ukuaji uchumi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Dk. Sira Ubwa Mamboya, amesema kuimarika kwa usafiri wa anga kunaongeza ukuaji mkubwa wa uchumi kupitia sekta ya utalii nchini.

Aliyasema hayo, wakati wa uzinduzi wa safari za ndege za moja kwa moja kutoka Uganda hadi Zanzibar kwa kutumia ndege ya Shirika la Ndege la Uganda.

Alisema uamuzi wa kuanzisha safari hizo, utaweza kuzidisha ushirikiano uliopo kati ya Zanzibar na Uganda.

Alisema kwa sasa Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, umekuwa mdogo kutokana na mashirika mengi ya ndege ulimwenguni kuanzisha safari zake Zanzibar.

Aidha, alisema kuwa mikakati ya serikali kukamilisha kwa haraka ujenzi wa jengo jipya la abiria terminal III ili kupunguza changamoto ya wageni kurundikana wakati wa ukaguzi wanapoingia nchini.

Alifafanua kuwa pia ujio wa ndege hiyo utaweza pia kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar ambapo kwa sasa umekuwa ukiimarika katika sekta mbalimbali za kimaendeleo.

"Hii inaonyesha kuwa bidii ya awamu ya saba ina dhamira njema ya kuendeleza maendeleo katika kuimarisha uchumi na kukuza maendeleo ya nchi," alisema.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Uganda, Aggrey Bagiire, alisema wakati umefika kwa Zanzibar kuimarisha biashara kati ya Uganda na Zanzibar ili kuimarisha pia utalii wa nchi hizo.

Baadhi ya viongozi walioshuhudia uzinduzi huo walisema safari za ndege kutoka Uganda hadi Zanzibar zitafungua milango ya ukuaji wa uchumi kupitia sekta ya utalii.

Ndege hiyo ya shirika la ndege la Uganda ilitua kwa mara ya kwanza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

# NEC yatoa neno daftari wapigakura

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Taifa (NEC), Jaji mstaafu, Semitocles Kaijage, amesema wadau wana nafasi kubwa ya kutoa maoni katika uboreshwaji wa daftari la wapigakura ili kufikia malengo ya mchakato huo.

Alisema NEC imekuwa ikifanya kazi zake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuleta tija katika uboreshaji wa daftari hilo.

Alisema hayo katika mkutano wa tume na wadau wa uchaguzi katika ukumbi wa Idrisa Abul Wakil Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema kila mtu anafahamu kuwa Tanzania ipo katika maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, hivyo kuna haja ya kufanya maboresho katika daftari la wapigakura.

Alisema uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ni sehemu ya maandalizi ya uchaguzi huo kwa mujibu wa ibara ya 74[6] ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeipa tume mamlaka ya kutekeleza majukumu mbalimbali.

Jaji Kaijage alisema zoezi hilo litahusisha pia kuboresha taarifa za wale wenye sifa na walioandikishwa awali kwa ajili ya uchaguzi wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamehama kutoka maeneo yao ya uchaguzi na waliopoteza kadi za mpigakura.

Alisema pia watafanya uhakiki wa vituo vya uandikishaji wa majaribio, maandalizi ya vifaa vya uboreshaji wa daftari na kuandaa mikakati ya elimu kwa mpigakura.

Kwa muijibu wa Mwenyekiti huyo, zoezi la uhakiki wa vituo vya kujiandikisha wapigakura nchi nzima lilifanyika mwaka jana lengo lake lilikuwa ni kuona vituo hivyo bado vipo na kama bado vina sifa na hadhi ya kuwa vituo vya uandikishaji kwa wapigakura kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi.

Alisema uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura umekwishaanza Tanzania Bara na mikoa 18 imeshakamilisha zoezi hilo.

Naye Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Mahera Charles, wakati akitoa mada katika mkutano huo, alisema NEC imepewa jukumu la kikatiba la kusimamia na kuratibu uandikishwaji wa wapigakuwa katika uchaguzi wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge na madiwani Tanzania Bara.

Alisema baada ya zoezi la uboreshwaji kukamilika tume ya uchaguzi itaanda daftari la wapigakura ambalo litatumika katika uchaguzi ambao utawahusu wale wenyesifa tu waliyoandikishwa.

Wadau hao walisema katika harakati za uchaguzi kuna kuwa na mambo mengi yanayotokea ikiwamo baadhi ya watu kupingwa kwa sababu za kisiasa.

Walisema ipo haja kwa tume hiyo kuwa na ofisi yake Zanzibar baada ya kumalizika kwa uchaguzi.

# JPM afagiliwa kwa kuboresha bandari

**Na Elizabeth Zaya,** MKASI

WAFANYABIASHARA wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wamempongeza Rais John Magufuli kwa jitihada anazofanya kuboresha mazingira ya biashara Tanzania ikiwamo kuboresha bandari nchini.

Wakizungumza katika Bandari ya Kirando iliyopo katika Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, walisema wamekuwa wakishuhudia maboresho yanayofanywa na Rais Magufuli katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya usafirishaji.

Mouse Labola Kaswela, alisema pamoja na jitihada za Rais Magufuli za kuboresha maeneo mbalimbali katika sekta ya biashara, lakini wamemshukuru kwa kuboresha sekta ya usafirishaji kupitia njia ya maji kwa kuboresha bandari ambazo nyingi zilikuwa na changamoto kipindi cha nyuma.

"Tunampongeza Rais Magufuli kwa kuboresha miundombinu katika bandari za Ziwa Tanganyika, sisi wafanyabiashara tunatoka DRC, lakini tunafanya kazi ya kuchukua bidhaa Tanzania, tunajua umuhimu wa maboresho haya, tunafahamu changamoto tulizokuwa tunakutana nazo zamani sasa hivi hazipo, na ikitokea siku tukamwona Rais Magufuli tutamwelezea furaha yetu," alisema Kaswela.

"Kiukweli kwa sasa mazingira ya biashara kwa Tanzania ni mazuri na ndiyo maana tunakuja kuchukua bidhaa zetu huku, tunamwomba azidi kuendeleza huu ujirani mwema.

Mkazi wa Kirando anayefanya biashara katika Bandari ya Kirando, Seif Kassim Seba, alisema kwa sasa miundombinu ya bandari imeimarika tofauti na ilivyokuwa awali na kwamba kasi ya biashara imeongezeka.

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Percival Salama, alisema lengo la Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), ni kuhakikisha inaboresha bandari zote katika ziwa hilo na kurahisisha usafiri wa njia ya maji ili kuvutia shughuli za kibiashara kutoka nchi za DRC, Burundi, Zambia na nyinginezo.

Akizungumzia Bandari ya Kipili ambayo pia inaboreshwa na TPA katika wilaya hiyo ya Nkasi mkoani Rukwa, Salama alisema tayari uboreshaji wake umefikia asilimia 100 ukihusisha ujenzi wa barabara inayoingia bandarini hapo, jengo la kupumzikia abiria na miundombinu mingine inayoizunguka.




Mkuu wa Kitengo cha Bima cha Benki ya NBC, Benjamin Nkaka (kushoto), akikabidhi zawadi mbalimbali kwa mteja wa kwanza kukata bima ya gari kupitia huduma za bima za NBC na Sanlam, Robert Danford Buguru, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya bima ya magari inayowalenga zaidi watumia vyombo vya usafiri katika msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka. Kampeni hiyo inayoendeshwa kwa kushirikiana na Kampuni ya Sanlam ilizinduliwa jana. Wanaoangalia ni wawakilishi kutoka NBC, Sanlam na Total. **MPIGAPICHA WETU**

# Wabuni mkakati wa kukabili udumavu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

KATIKA kupambana na hali ya udumavu mkoani Kagera, wasindikaji wa nafaka kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wameazimia kuwa na mashine ambazo zina uwezo wa kuchanganya virutubishi katika bidhaa ya nafaka.

Maazimio hayo yametokana na changamoto kubwa ya upatikanaji wa lishe kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Akizungumza na wadau wa usindikaji katika kikao cha kuweka mikakati ya kuongeza urutubishaji wa vyakula na usalama wake, mtaalamu wa chakula na lishe kutoka Sanku, Josephine Kimario, alisema kwa kuona kuwa nchi ina uhitaji mkubwa wa lishe bora hasa kwa watoto wadogo wanahitaji makuzi.

Alisema mashirika yaliyoingia mikataba na serikali kwa kufanya usambazaji wa vifaa vya mashine zenye uwezo wa kusindika nafaka ambayo inatumiwa na wananchi kuanzisha utoaji wa viini lishe kwa wasindikaji.

"Ili kumrahisishia mlaji, wataalamu wameamua kutengeneza virutubishi vya moja kwa moja ambavyo vinachanganywa kwenye nafaka pale anapokwenda kutumia inakuwa imekamilika tayari kwa matumizi," alisema na kuongeza:

"Na lengo kubwa ni kuwafikia wananchi wengi na kuondoa hali ya ukosefu wa lishe kwa Kagera, ambayo ina idadi ya watoto wenye udumavu inafahamika hivyo ni jitihada tu," alisema Kimario.

Mrutubishaji wa vyakula aina ya vimiminika na nafaka kutoka Shirika la Gain Tanzania, Archard Ngemela, alisema jamii imekuwa ikishindwa kuboresha lishe kwa bidhaa ambazo zina udhibiti wa TBS na TMDA kubaini vitu ambavyo havina aina yoyote ya lishe.

Ngemela alisema hali hiyo imekuwa changamoto kwa wananchi kwani bidhaa nyingi hutunzwa kinyume cha inavyostahili kuhifadhiwa.

Naye Katibu Tawala wa mkoa huo, Prof. Faustine Kamzora, alisema ili kufanikiwa na zoezi hili jitihada zaidi zielekezwe vijijini kwa kubainisha watoto walio na hali mbaya zaidi.

# Fursa ya bima yaja kwa wenye magari

**Na Mwandishi Wetu**

WAMILIKI wa magari wamewezeshwa baada ya kuzinduliwa kwa kampeni ya bima ya magari lengo likiwa kusogezewa huduma.

Kampeni hiyo imezinduliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Sanlam, ambayo itaanza Desemba mwaka huu hadi Januari mwakani.

Imeelezwa kuwa kampeni hiyo ni sehemu ya malengo ya benki kusogeza huduma zake karibu zaidi na wateja kwa kuwapa mahitaji muhimu kupitia huduma bora zilizoandaliwa mahsusi kwa ajili yao.

Kwa kutambua umuhimu wa usalama kwa wasafiri na watumiaji wote wa vyombo vya moto kwa ujumla, katika kipindi hiki cha msimu wa sikukuu, benki hiyo imerahisishia mteja kupata kifurushi kizuri cha bima kwa ajili ya magari kikiambatana na nyongeza kadhaa za kuvutia.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Bima wa NBC, Benjamin Nkaka, alisema kampeni hiyo imezinduliwa katika kipindi sahihi cha mwaka ambapo kwa kawaida huwa na idadi kubwa ya wasafiri.

Alisema wamedhamiria kuboresha huduma za bima na kufanya kasi ya matumizi ya bima nchini kuongezeka, kwa kupitia kampeni hii, wateja watakaonunua bima katika matawi ya NBC watapata ofa kadha wa kadha zikiwamo huduma ya bure ya mafuta ya kilainishi cha injini na mafuta ya bure kutoka vituo vya mafuta vya Total pamoja na bima ya bure ya ajali ulemavu wa kudumu na gharama za matibabu kutokana na ajali.

Meneja Mahusiano wa Bima wa benki hiyo, Kuruthum Mwaluwinga, alisema, wamiliki wa magari yenye thamani ya Sh. 50,000,000 na zaidi watanufaika na mafuta bure pamoja na bima ya bure ya ajali, ulemavu wa kudumu na gharama za matibabu kutokana na ajali.

Aliongeza kwa wateja wenye magari yenye thamani ya kuanzia Sh. 15,000,000 hadi Sh. 49,900,000, watapata lita 10 za mafuta bure katika kituo chochote cha Total nchi nzima, bima ya ajali ama ulemavu wa kudumu na gharama za matibabu.

Mwisho kwa wateja wenye magari yenye thamani ya kuanzia Sh. 7,000,000 hadi Sh. 14,900,000, watapata lita tano za bure za mafuta katika kituo chochote cha Total nchini, bima ya ajali ya bure ama ulemavu wa kudumu na gharama za matibabu. Wateja wote kwenye vipengele tajwa watapata kadi ya Total kwa ajili ya kujazia mafuta.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Binafsi wa NBC, Elibariki Masuke, alisema kuzinduliwa kwa kampeni hiyo ni ishara wazi ya dhamira NBC kutoa huduma bora za kifedha kwa wateja wake hapa Tanzania.

**HABARI KIMATAIFA**

## Waliokufa India sasa wafikia 23

**NEW DELHI,** India

MAELFU ya watu wamejiunga na wimbi jipya la maandamano dhidi ya sheria mpya ya uraia nchini India, huku idadi ya waliokufa ikifikia 23.

Idadi ya vifo imepanda siku moja baada ya kuzuka maandamano ya vurugu kwenye Jimbo la Uttar Pradesh ambako watu 15 akiwamo mtoto wa miaka 8 waliuawa.

Hasira inaongezeka juu ya sheria hiyo iliyopitishwa na Bunge Desemba 11, inayotoa nafasi ya kupatiwa uraia wahamiaji wasio Waislamu kutoka jamii za wachache kwenye mataifa matatu yaliyo jirani na India. Wakosoaji wake wanasema sheria hiyo inawabagua Waislamu na ni sehemu ya mpango wa chama cha Kihindu cha Waziri Mkuu Narendra Modi, madai ambayo mwenyewe amekanusha.

Mamlaka za India zimetangaza sheria za dharura, kuzima mtandao wa intaneti pamoja na kufunga maduka kote nchini humo ili kujaribu kudhibiti vurugu zinazoendelea. **DW**



## Marekani, China zakubaliana kumaliza vita vya kibiashara

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema nchi yake itatiliana saini na China, baada ya mazungunzo ya awamu ya kwanza ya makubaliano ya kibiashara kukamilika.

Awamu ya kwanza ya makubaliano ilitangazwa mapema mwezi Desemba kama sehemu ya juhudi za kumaliza miezi kadhaa ya vita vya kibishara kati ya mataifa hayo mawili yenye uchumi mkubwa.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha wa Marekani, Steven Mnuchin, makubaliano hayo yanaweza kutiwa saini mapema mwezi Januari, na kwamba sasa yanafanyiwa marekebisho ya mwisho.

Chini ya makubaliano hayo, Marekani itaridhia kupunguza baadhi ya ushuru kwa ahadi kuwa China itaongeza ununuaji wa bidhaa za kilimo kutoka Marekani. **DW**



# Trump aanzisha kikosi cha vita anga za juu

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesaini pesa dola bilioni 738 kuwezesha Wizara ya Ulinzi (Pentagon) kuanzisha mradi wa kuunda kikosi kipya cha vita vya anga za juu kinachojulikana kama US Space Force.

Kikosi hicho kipya katika Jeshi la Marekani, kitakuwa cha kwanza katika huduma za jeshi hilo, kwa miaka 70.

Akiwa katika ngome ya kijeshi karibu na Washington, Trump alielezea anga za juu kama eneo jipya la dunia la mapigano ya kivita.

"Huku kukiwa na ongezeko kubwa la vitisho kwa usalama wa taifa letu, ukuu wa Marekani katika anga ni muhimu sana," alisema Rais Trump.

**Tunaongoza, lakini hatuongozi vya kutosha, lakini muda mfupi sana tutakuwa tunaongoza kwa kiwango kikubwa.**

"Tunaongoza, lakini hatuongozi vya kutosha, lakini muda mfupi sana tutakuwa tunaongoza kwa kiwango kikubwa."

Rais Trump aliongeza zaidi: "Jeshi la anga za juu litatusaidia kuzuwia uchokozi na kudhibiti anga za juu."

Pesa zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za kikosi hicho zilithibitishwa Ijumaa wakati Rais Trump aliposaini bajeti ya mwaka ya Jeshi la Marekani.

Uzinduzi huo utagharimu dola milioni 40 kwa mwaka wa kwanza.

Marekani haina lengo la kuweka majeshi yake katika uzio wa dunia, lakini italinda mali za Marekani kwa kutumia mamia ya satelaiti za mawasiliano na uchunguzi.

Hii inakuja wakati wakuu wa Jeshi la Marekani wakiyaona mataifa ya China na Urusi yakijiimarisha kijeshi.

Kikosi cha anga za juu cha Marekani kitaanza shughuli zake kwa kuzingatia ushauri wa kituo kilichopo kwa sasa cha maagizo ya kijeshi ya anga za juu (SpaceCom), ambacho kilibuniwa mwezi Agosti kushughulikia operesheni za Jeshi la Marekani za anga za mbali.

Mkuu wa Kikosi cha Anga cha Marekani, Barbara Barrett, alisema kuwa kikosi cha anga za juu kitajumuisha wanajeshi wa anga 16,000 na wafanyakazi wa kawaida.

Kitaongozwa na Generali wa Kikosi cha Anga, Jay Raymond, ambaye kwa sasa anaongoza kituo cha anga za juu SpaceCom. **BBC**



Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, akikagua moja ya kituo cha kutengenezea makombora hivi karibuni. Japan imelalamika nchi hiyo imeagiza shehena ya mafuta ghafi kwa ajili ya kurushia makombora mapya. **PICHA: REUTERS**

# Kijana aomba afungwe kwa kukosa makazi

**BERLIN,** Ujerumani

KIJANA mmoja nchini Ujerumani, ambaye hana kazi wala mahali pa kuishi, aliamua kumgonga mtu aliyekuwa anaendesha baiskeli kwa makusudi ili aweze kufungwa gerezani na kupata sehemu ya kuishi.

Mahakimu katika mji wa Oldenburg, wanasema kuwa mwanaume huyo mwenye umri wa miaka 62 alifanya tukio hilo kwa nia ya kutafuta makazi ya kuishi.

Mahakama ilisikiliza namna ambavyo mwanaume huyo jinsi alivyopoteza ajira yake ya utaalamu wa sayansi ya kompyuta na hakuwa na namna nyingine ya kuishi baada ya kumaliza fedha zote za akiba wakati akitafuta ajira.

Wakati alipokamatwa, alikuwa hana nyumba bali alikuwa anaishi katika gari lake ambalo lilikuwa halina vibali vya kutembelea kwa muda mrefu.

Mshtakiwa huyo aliamua kuendesha gari na kumjeruhi mwanaume mwenye miaka 48 aliyekuwa anaendesha baiskeli.

Majaji wamemuhukumu kutokana na kitendo chake na kukubaliana na matakwa yake ya kutaka makazi ya kudumu jela. Hata hivyo wamedai bado anahaki ya kukaa gerezani kwa kuwa alifanya jaribio la kuua.

Mwendesha baiskeli bado anapatiwa matibabu kutokana na athari alizopata kwa kuumia katika ajali hiyo. **BBC**

# TCCIA yapewa majukumu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekitaka Chama cha Wenye Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), kufuata na kusimamia misingi ya sheria na taratibu ya nchi ili kiweze kufanikiwa zaidi na kwenda sambamba na azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akifungua Mkutano wa Mwaka wa 31 wa TCCIA mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, alisema TCCIA ipo katika nafasi nzuri ya kufanikisha azma ya serikali kwa vitendo ukizingatia mtandao iliyonayo nchi nzima kinachotakiwa ni kufuata na kusimamia misingi ya sheria na taratibu zote zinazoongoza sekta hizo.

"Serikali inatambua na kuheshimu mchango wa sekta binafsi, hivyo basi wajumbe changamkieni fursa za masoko kutoka nchi za SADC na nyingine kutoka Ulaya na Asia ili muweze kuuza kwa wingi bidhaa zetu ili kuendelea kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Manyanya.

Alisema TCCIA na wanachama wake ni vizuri wakawa mstari wa mbele kuhakikisha maadili ya kibiashara na kisheria zinafuatwa katika utekelezaji majukumu yao kama njia ya kuunga mkono jitihada za serikali.

"Mjenge chemba imara itakayojitegemea na kujitambua. Isiwe chemba ya kulalamika bali inayotoa dira kuweza kusimama husussani katika kutekeleza azma ya serikali ya awamu ya tano kujenga ya uchumi wa kati na viwanda," alisisitiza Manyanya.

Manyanya alipongeza safu mpya ya uongozi TCCIA na kuwataka wafanye kazi kwa bidii na kufanikisha malengo ya wanachama wake waliopo kila kona ya nchi kwa kuwa wamewaamini.

Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema kazi iliyopo mbele ya chemba ni kuimairisha na kujenga ofisi zake katika ngazi ya mkoa na wilaya ili wanachama wake na Watanzania kwa ujumla waweze kunufaika moja kwa moja na chama hicho.

Alisema TCCIA ina mikakati mingi ya kuhakikisha kuwa chemba hiyo inajitegemea na kuimarisha sekta ya biashara. Alitaja baadhi ya mikakati ni kujenga uhusiano mzuri na serikali, kutoa mafunzo kwa wanachama ili waweze kutambua firsa zinazowazunguka na kuzitumia.

"Naishukuru serikali kwa kutuamini TCCIA na pia tutaufanya kazi ushauri aliotupa Mheshimiwa Naibu Waziri na ifikapo mwakani wakati kama huu tutamwomba atuulize tumefikia wapi na tutakujibu," alisema Koyi.

Makamu Mwenyekiti wa TCCIA chemba ya Dar es Salaam (Biashara), Dk. Mtemi Kingu, alisema wamejipanga kufanya kazi sambamba na azma ya serikali ya kuhakikisha Tanzania inafikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 kwa vitendo.

Naye Mwenyekiti TCCIA Chemba ya Kilimanjaro, Patrick Shizima, alisema wanachama wana matumaini makubwa na Rais mpya wa TCCIA kutokana na mikakati madhubuti aliyokuja nayo na kuahidi kumpa ushirikiano.

## Mwalimu wa madrasa

INATOKA UK. 2

Mussa Omar, uliofunga ushahidi, ambapo hakimu alimweleza mtuhumiwa huyo kuwa ana kesi ya kujibu.

Ndipo Desemba 19, mwaka huu ilipofika zamu ya hakimu huyo, kumsomea hukumu yake, alitumia kifungu cha 114 (1) cha Sheria ya Adhabu namba 6 ya mwaka 2018, na kumtia hatiani kwa kwenda jela miaka 10.

"Mshtakiwa utatumikia chuo cha mafunzo kwa muda wa miaka 10, kutokana na mahakama hii kubaini kwamba bila ya halali na kwa njia ya aibu, ulimshambulia kwa aibu mtoto wa miaka tisa," alisema hakimu huyo.

Aidha, hakimu huyo, alimweleza mshtakiwa huyo kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria za Zanzibar, kumwingiza vidole tena sehemu za siri mtu yeyote bila ya ridhaa yake.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, wakili wa serikali, Juma Mussa Omar, aliiomba mahakama hiyo kumpa adhabu kali mshtakiwa, kwa madai kuwa vitendo vya kikatili dhidi ya watoto katika siku za karibuni, vimeongezeka kwa kasi.

Mshtakiwa huyo, ambaye alikuwa ni mwalimu wa madrasa ya Alkhalil eneo la Afrikana mjini Chakechake, katika utetezi wake, aliiomba mahakama hiyo, impunguzie adhabu kutokana na kuwa na familia inayomtegemea.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Agosti 20, mwaka 2019, ambapo, kwenye hati ya mashtaka, mshtakiwa alidaiwa kutenda kosa hilo Julai 18, mwaka 2019 majira ya jioni, ndani ya madrassa eneo la Afrikana mjini Chakechake Pemba.

Ilielezwa kuwa mshtakiwa huyo anayeishi Michweni mkoa wa Kaskazini Pemba, bila ya halali na kwa njia ya aibu, alimshambulia kwa vidole mwanafunzi wake katika sehemu za siri na kumsababishia maumivu makali.






## Mambo 5 ya Chadema

INATOKA UK. 2

Kwa mujibu wa Mnyika, Chadema imeamua kuanza mchakato wa

kuwaandaa wagombea wa nafasi za udiwani, ubunge na urais wa mwaka 2020 ili kupata wagombea bora watakaowezesha kushinda katika uchaguzi huo.

Alisema kuwa sekretarieti ya chama hicho itapitia sera ya chama na kupata maoni ya wananchi kulingana na mazingira ya sasa ili kuandaa ilani ya uchaguzi mkuu mwakani.

Kuhusu Chadema digitali, Mnyika alisema baada ya uzinduzi uliofanyika Desemba 18, mwaka huu, alieleza kuwa kazi kubwa iliyobaki kwa sekretarieti ni kuweka mifumo na utaratibu wa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuleta mabadiliko.

Alisema mfumo wa digitali utasaidia kuchangia vuguvugu, harakati na siasa za mabadiliko na kwamba Chadema itatumia mpango huo kujiimarisha kimapato katika uungwaji mkono, kupata wanachama na kusaidia kushinda uchaguzi.

Alisema katika Chadema lengo kuu ni kujenga taasisi imara ya 'People's Power' kuanzia ngazi ya chini ya kitongoji, kijiji, kata na shehia kwa Zanzibar, majimboni, wilayani, mkoani, kanda na taifa.

Aidha, alisema chama hicho kimejipanga kuendeleza zoezi la Chadema ni msingi ili kujenga mtandao wa chama hicho na kile alichosema nguvu ya umma katika kujihakikishia ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

HABARI KITAIFA

# Exim yaibuka kinara Tuzo Mwajiri Bora 2019

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imeendelea kuwa kinara kwenye Tuzo za Mwajiri Bora za mwaka 2019, baada ya kutwaa Tuzo ya mshindi wa jumla ya Mwajiri Bora kutoka ndani ya nchi ya mwaka 2019 zilizoandaliwa na kutolewa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) wiki iliyopita.

Mbali na tuzo hiyo ilishuhudiwa pia benki hiyo ikiibuka kinara kwenye tuzo ya mshindi wa jumla ya ushirikishaji mzuri wa wafanyakazi ya mwaka 2019 sambamba na kutangazwa kuwa miongoni mwa waajiri kumi bora hapa nchini kati ya waajiri 800 walioshiriki kuwania tuzo hiyo.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilifanyika jijini Dar es Salaam ikipambwa na uwapo wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Mkuu wa Idara wa Rasilimali Watu wa benki hiyo, Frederick Kanga, alisema tuzo hiyo ni kiashiria tosha mbele ya jamii kuhusiana na namna ambavyo benki hiyo imewekeza kwenye rasilimali watu, hatua ambayo ina umuhimu mkubwa katika kufanikisha malengo ya benki hiyo.

"Tuzo zote hizo tatu ni heshima kubwa kwetu na ni matokeo ya uwekezaji wa muda mrefu ambao tumekuwa tukiufanya kwa rasilimali watu kwenye taasisi yetu katika kuwasaidia waweze kutoa mchango wao kiutendaji katika ubora tunaoutarajia na ikibidi zaidi ya matarajio," alibainisha Kanga.

Aliongeza kuwa moja ya vipaumbele vya benki hiyo ni pamoja na kuwaandaa watendaji wake kwa kuwaongezea ujuzi unaowawezesha kuwa mbele ya wakati katika utendaji wao ili kuleta matokeo bora na yenye ubunifu mpya kwa wateja.

Katika tuzo za hizo kwa mwaka huu zaidi ya waajili 800 kote nchini walishiriki kuwania tuzo mbalimbali ikilinganishwa na idadi ya waajiri 150 tu walioshiriki mwaka jana.

Kwa mujibu wa Kanga, benki hiyo imedhamiria kuandaa wafanyakazi wenye ushirikiano katika kuunda timu imara ya pamoja kwa kuandaa mazingira ambayo wafanyakazi hao watajihisi kuwa wanathaminiwa, wanashirikishwa sambamba na kupewa fursa ya kukua na kujiendeleza kitaaluma.



Mkuu wa Idara wa Rasilimali Watu wa Benki ya Exim Tanzania, Frederick Kanga (wa pili kushoto) pamoja na wafanyakazi wengine wa benki hiyo, wakifurahia baada ya kutwaa tuzo ya mshindi wa jumla ya Mwajiri Bora ya mwaka 2019 pamoja na tuzo ya mshindi wa jumla ya ushirikishaji mzuri wa wafanyakazi ya mwaka 2019 jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania wahimizwa kusoma vitabu

**Na Enock Charles**

WATANZANIA hususani vijana wametakiwa kujenga utamaduni wa kusoma vitabu ili waweze kupata na kuongeza maarifa yatakayo wawezesha kufikia ndoto zao katika maisha.

Wito huo ulitolewa na mwandishi wa kitabu cha "Talk to God" (Ongea na Mola), Masija Buchafwe, alipozungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana wakati akitambulisha kitabu hicho.

"Ndani ya vitabu kuna maarifa mengi ambayo ni msaada mkubwa kwa watu wa rika mbalimbali katika kukabiliana na changamoto za maisha za kila siku, hivyo itakuwa ni jambo muhimu sana kama taifa watu wake wakawa na utamaduni wa kujisomea vitabu.

Mimi naweza kuzungumzia Tanzania. Kwa maoni yangu tofauti na miaka ya 1950 hadi 1970 Tanzania ya leo haina watu wenye kiu ya kusoma vitabu," alisema Buchafwe.

Aliwaomba wazazi na viongozi katika taasisi za elimu kuwatia moyo na kuwahimiza vijana kusoma vitabu, na kueleza kwamba kwa tabia watu wenye elimu na maarifa ya kisasa ni watu wanaosoma sana na watu wasiosoma wana maarifa kidogo ya kileo.

"Kitabu hiki mbali ya kuangazia mambo ya kiimani, lakini pia kimeangazia mambo ya biashara, siasa, uchumi na upendo ambayo yamekuwa muhimu katika kuchochea maendeleo ya mtu binafsi na Taifa kwa ujumla," alieleza Buchafwe, na kuongeza kwamba angefurahi kupokea mrejesho wasomaji wa imani zote.

Buchafwe alisema imemchukua takribani miaka 16 kuandaa na kupata mchapishaji ambaye ameyaunganisha mashairi na kuwa kitabu cha kurasa 84.

"Haikuwa kazi rahisi kukamilisha kitabu hiki, changamoto zilikuwa nyingi, lakini nilizitumia katika kujenga maudhui yaliyo bora zaidi kwa faida ya wasomaji," alisema.

# Wasio na sifa uchaguzi Z'bar wajisajili kupiga kura Muungano

**Na Rashid Omar,** PEMBA

TUME ya Uchaguzi (NEC), imewataka wasio na sifa za kuandikishwa kupiga kura Zanzibar, wajiandikishe kwenye daftari la kudumu la wapigakura ili wawachague Rais wa Jamhuri ya Muungano na wabunge.

Makamu Mwenyekiti NEC, Jaji Mbarok Salim Mbarok, aliwataka wajiandikishe wakati wa kuboresha daftari la kudumu ili wachague viongozi hao.

Alisema NEC imekamilisha maandalizi yote muhimu kwa ajili ya uandikishaji wa wapiga kura wapya na kufanyia uhakiki daftari hilo ili kulitumia kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Alisema kabla ya kukamilisha maandalizi hayo awali walifanya uhakiki wa vituo vya kupigia kura Bara na Zanzibar ikiwa na lengo lakujua kuwa vituo hivyo bado vipo na bado vina sifa ya kusajili wapigakura.

Alifahamisha kuwa kwa kuzingatia matakwa ya katiba na vifungu vya sheria, Tume ya Uchaguzi itaendelea kuboresha daftari la kudumu la wapigakura ikiwa ni maandalizi ya uchaguzi mkuu wa 2020.

Alisema NEC inasimamia na kuratibu uandikishaji wapigakura wa Rais na wabunge kwa Jamhuri ya Muungano na madiwani kwa Tanzania Bara, kwa mujibu wa ibara 74(6)(a) na (d) ya katiba ya Tanzania.

Alifafanua kuwa kila kijiji na mtaa kutakuwa na angalau kituo kimoja ili kila mwenye sifa apate nafasi ya kujiandisha katika vituo hivyo vilivyopangwa katika majengo ya umma au maeneo ya wazi yaliyokubalika.

Alisema tume haitaweka vituo katika maeneo yasiyo kubalika kisheria kama nyumba za ibada, kambi za ulinzi na vituo vya polisi.

Akitoa maelezo yake Salimu Seif Khalifani wa ACT-Wazalendo alitaka tume hiyo kuweka ofisi ya kudumu Pemba na kujitahidi kuona kuwa hakuna malalamiko kwa wananchi.

Omar Hamad wa Msikiti wa Ijumaa, Wete alitaka tume hiyo wakati wa kusajili na kuboresha iwashirikishe viongozi wa dini ili waweze kuitaarifu na kuishauri pale inapohitajika kufanya hivyo.




HABARI MICHEZO




# OXLADE-CHAMBERLAIN APATA PANCHA TENA

**DOHA,** Qatar

ALEX Oxlade-Chamberlain alilazimika kuvaa kiatu kigumu cha kulinda mguu na kutembelea magongo wakati Liverpool ikibeba Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia juzi Jumamosi.

Kiungo huyo wa kimataifa wa England aliumia kwenye dakika ya 72, wakati Liverpool wakipata ushindi wa 1-0 katika dakika za nyongeza dhidi ya Flamengo, na alionekana wazi kuumia kifundo cha mguu.

Machela yalipelekwa uwanjani kwa ajili ya kumsaidia Oxlade-Chamberlain kuondoka dimbani, lakini aliamua kutembea mwenyewe na nafasi yake ikachukuliwa na Adam Lallana.

Majeraha hayo ya Oxlade-Chamberlain sasa yanaongeza orodha ya wachezaji wa kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp, wakati huu Georginio Wijnaldum na Fabinho wakiwa wanaendelea kuuguza majaraha nje ya dimba.

Klopp alisema baada ya mchezo huo: "Anajihisi vizuri, tutaona. Si sawa, lakini tutaona hapo baadaye. Ni pigo kubwa kwetu, lakini tutaona kitakachotokea."

Oxlade-Chamberlain awali alikuwa nje ya dimba kwa mwaka mzima, akicheza mechi mbili tu kwa msimu wa 2018/19, baada ya kuumia goti kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya AS Roma.

Hata hivyo, amekuwa kwenye kiwango kizuri kwa Liverpool msimu huu, huku akifunga mabao sita kwenye mechi 24 alizocheza kwenye mashindano yote.

'Wekundu' hao wa Anfield walibeba taji la Klabu Bingwa Dunia kwa bao la Roberto Firmino katika muda wa ziada, na lilikuwa taji lao la kwanza kwa mashindano hayo.

# Neymar, Mbappe wamkuna Tuchel

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, anaamini Neymar na Kylian Mbappe wanahamasisha kila mmoja baada ya kung'ara kwenye ushindi wa 4-1 dhidi ya Amiens, Jumamosi.

Mbappe alifunga mara mbili na Neymar pia akafunga kabla ya Mauro Icardi kufunga la nne hapo kwenye dimba la Parc des Princes.

Desemba PSG imefunga mabao 22 katika ushindi wa mechi sita, huku Mbappe (akifunga nane) na Neymar akifunga matano.

Alipoulizwa kama wanaweza kuwa bora, Tuchel hakuwa na uhakika na namna ya kuwaelezea na aliwasifia tu nyota wake hao.

"Nini unachomaanisha, ubora? Wanachezaji vizuri mno wakiwa pamoja. Wamejipanga na wanajiamini kwelikweli na wako fiti, hicho ndio kitu cha muhimu zaidi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Wote wawili ni hatari wakiwa pamoja kwa sababu wanacheza kwa umoja na nalipenda hilo. Wapo karibu zaidi wakiwa uwanjani na wanapenda kucheza kama vile."

Tuchel aliongeza: "Neymar anampa hamasa Mbappe, na Mbappe anamhamasisha Neymar, hilo ni jambo zuri."






# Zidane: Guardiola kocha bora duniani

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesifia uwezo wa Pep Guardiola baada ya Real Madrid kupangwa kucheza na timu ya kocha huyo wa zamani wa Barcelona, Manchester City kwenye hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezo wa kwanza utapigwa kwenye dimba la Santiago Bernabeu Februaria 26, mwakani na mshindi wa jumla atasonga mbele kwenye hatua ya robo fainali.

Guardiola awali aliukaribisha mchezo huo, akisema utakuwa "maalumu" kukutana na Zidane, mtu ambaye "aliota" kucheza naye.

Mfaransa huyo akiwa kwenye maandalizi ya mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, dhidi ya Athletic Bilbao uliopigwa jana, alimuita Guardiola kuwa ni kocha anayeongoza duniani.

"Ndio (itakuwa maalumu). Nilicheza dhidi yake mara nyingi," alisema Zidane juzi, Jumamosi.

"Nilimheshima kama mchezaji na namheshimu kama kocha. Nafikiri yeye ni bora duniani na ameshalithibitisha hilo kwa kazi kubwa aliyofanya.

"Bila shaka, nataka sana kukutana naye, kucheza dhidi yake na timu yake. Si kwa sababu yangu, lakini kwa ajili ya wote."



# GUARDIOLA: HUYU DE BRUYNE ACHA KABISA

**MANCHESTER,** England

KIWANGO kilichoonyeshwa na Kevin de Bruyne wakati Manchester City wakipata ushindi dhidi ya Leicester "ndicho kiwango bora zaidi alichocheza kwa muda mrefu," kwa mujibu wa kocha, Pep Guardiola.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, De Bruyne mwenye umri wa miaka 28, alitawala nafasi ya kiungo kwa kiwango cha kuvutia, wakati mabingwa hao watetezi wakipunguza pengo la Leicester waliopo nafasi ya pili na kufikia moja.

De Bruyne alitengeneza bao la Gabriel Jesus, huku Riyad Mahrez na Ilkay Gundogan kila mmoja akifunga moja kwenye ushindi huo wa 3-1.

"Ni mchezaji anayenivutia haswa," alisema Guardiola baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari. "Alishinda mchezo wetu."

De Bruyne alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwenye mechi za City zilizopita kwenye Ligi Kuu dhidi ya Arsenal, akifunga mara mbili na ingawa hakufunga kwenye mchezo huo dhidi ya Leicester, kiwango chake ndio kiliubeba mchezo huo wa mwisho kabla ya Sikukuu ya Krismasi.

Kwenye ushambuliaji msimu huu, mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea, De Bruyne anashika nafasi ya tano kwa kuwa na mashuti 52, matatu yakigonga mwamba, huku akitengeneza krosi 170.

Guardiola alisema: "Nilifurahishwa na namna alivyocheza. Tulitengeneza nafasi nyingi na tulicheza vizuri. Nilifurahia zaidi kuliko mchezo ule dhidi ya Arsenal."

# Klopp abeba ubingwa akikiri Flamengo balaa

**DOHA,** Qatar

JURGEN Klopp amewasifia wachezaji wote wa Liverpool kwa kutwaa ubingwa wa Klabu Bingwa Dunia dhidi ya Flamengo, akidai kwamba ugumu wa mchezo huo umemfanya kutoa heshima kwa wachezaji wake kwa maneno.

Liverpool walionekana kubanwa na mabingwa hao wa Copa Libertadores, Flamengo kwenye mchezo huo wa Jumapili mjini Doha.

Ubao wa matokeo ulikuwa hauna mabao hadi kumalizika kwa dakika 90, lakini Roberto Firmino alifunga bao pekee kwenye mchezo huo dakika ya 99.

Licha ya Flamengo kuonyesha kiwango kizuri na kuipa presha kubwa Liverpool, lakini Wekundu hao walifanikiwa kulitwaa taji hilo kwa mara yao ya kwanza na Klopp alielezea ugumu wa mchezo huo.

"Napata shida kutafuta maneno mazuri ya kuonyesha hisia zangu kwa vijana wangu, ilikuwa ni ya kuvutia. Tulifanya vingi vizuri," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari mjini Doha.

"Niliona nyakati nyingi za kiwango cha kuvutia na kwa uhakika nina furaha. Nafikiri tulistahili ushindi. Tulikuwa timu bora.

"Katika nyakati za kuamua matokeo kwa uhakika tulikuwa vizuri na golikipa alicheza kwa kujituma na umakini mkubwa na wakati mwingine tulitawala mchezo, hivyo nina furaha kubwa.



# *Arteta avuta kocha Man United kumsaidia Arsenal*



**LONDON,** England

KOCHA msaidizi wa zamani wa Manchester United na Everton, Steve Round amejiunga na Mikel Arteta kwenye benchi la ufundi pale Arsenal, kwa mujibu wa Sky Sports.

Round alijiunga na Arteta jukwaani katika Uwanja wa Goodison Park Jumamosi kushuhudia Arsenal ikicheza na Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliomalizika kwa sare ya bila kufungana.

Round alifanya kazi chini ya Steve McClaren wakati akifundisha pale Middlesbrough na England kabla ya kujiunga na Sam Allardyce kule Newcastle mwaka 2007.

Mwaka uliofuata alikuwa msaidizi wa David Moyes pale Everton na alijiunga naye pale Manchester United, kabla ya kuondoka klabuni hapo mwaka 2014 wakati raia huyo wa Scotland alipofukuzwa.

Round baadaye alitumia miaka miwili akiwa mkurugenzi wa soka pale Aston Villa kabla ya kuondoka klabuni hapo mwaka 2018.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 49, atajiunga na Arteta, ambaye aliteuliwa kuwa kocha mkuu wa Arsenal Ijumaa na kusaini mkataba wa miaka mitatu na nusu ya kukaa hapo kwenye dimba la Emirates.

Raia huyo wa Hispania amechukua nafasi ya Unai Emery, ambaye alifukuzwa Novemba mwaka huu baada ya kucheza mechi saba bila ushindi.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATUPIA LA 50 KWA MWAKA 2019

●●● Mambo haya yanatokea kwake, tuliona wote kwa wakati ule, kitu kama kile kinaweza...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amefikisha mabao 50 kwa mara ya sita mfululizo kwenye kalenda ya mwaka baada ya kuifungia Barcelona dhidi ya Deportivo Alaves juzi, Jumamosi.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alifunga bao hilo kwa shuti kali akiwa umbali wa yadi 20 katika dakika ya 69 kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Camp Nou wakati Barca wakipaa kileleni mwa msimamo mwa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.**

Jitihada za Messi ziliipa Barca mabao mawili ya uongozi baada ya Alaves kufunga wakijibu mabao ya Antoine Griezmann na Arturo Vidal kwa kazi nzuri aliyoifanya Pere Pons.

Mshambuliaji huyo wa Argentina, Messi alifikisha mabao 50 kutoka katika mechi 58 alizoichezea klabu hiyo na nchi yake kwa mwaka 2019.

Pia ametoa pasi za mwisho 'asisti' 18 kwa mwaka mzima na akiwa ametoka kutwaa tuzo ya Ballon d'Or kwa mara ya sita na kuweka rekodi.

Mabao hayo 50 ya Messi mwaka huu, 34 amefunga katika mechi 32 za Ligi Kuu ya Hispania, mabao nane kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na matatu kwenye Kombe la Copa del Rey. Matano akiifungia Argentina, ambapo kwa mwaka huu ameichezea jumla ya mechi 10.

Messi sasa amekuwa akifunga angalau mabao 50 kila mwaka kwa kipindi cha miaka 10, mwaka pekee ambao hakufikisha mabao 50 ilikuwa ni 2013, ambapo alifunga mabao 45. Mwaka wake bora zaidi ulikuwa ni 2012 ambapo alifunga mabao 91 kwa jina lake.

Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde alimsifia Messi kwa uwezo wake huo na kiwango alichokionyesha wakati wakipata ushindi huo wa 4-1 dhidi ya Deportivo Alaves.

Ingawa Barca ilikwenda mapumziko ikiwa inaongoza kwa mabao 2-0, Alaves ilifunga mapema kipindi cha pili na kuongeza kujiamini hadi pale Messi alipofunga bao lake la 50 mwaka huu.

Akionekana kuzungukwa na mabeki, Messi aliweza kuachia shuti kali kwa mguu wake wa kushoto akiwa umbali wa yadi 25 na Luis Suarez - ambaye alitoa 'asisti' kwa mabao mawili ya kwanza, akafunga la nne kwa mkwaju wa penalti.

Licha ya Suarez kuonekana kama kuwa nyota wa mchezo huo, Valverde akili yake aliiwekeza kwa Messi ambaye alionekana kuwasumbua zaidi mabeki wa timu pinzani.

"Mechi zote zinahitaji ubunifu," alisema kocha huyo. "Wakati walipofunga, walitunyamazisha na kuonekana walikuwa na nafasi ya kusawazisha, lakini leo alifunga bao zuri kutoka njia tofauti.

"Nafikiri tulicheza mchezo ule vizuri, naweza kusema kipindi cha kwanza kilikuwa kizuri, halafu tulionyesha kiwango kidogo mwanzoni mwa kipindi cha pili. Bao la tatu liliuongezea nguvu.

"Mambo haya yanatokea kwa Messi. Tuliona wote kwa wakati ule. Kitu kama kile kinaweza kutokea, ni nafasi nzuri kuwa na Messi."

## ZISIKUPITE

### YAJIONGEZA KWA SANCHO

CHELSEA itazipiku Manchester United na Liverpool kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 19, huku wakiwa tayari kufikia bei wanayoitaka Borussia Dortmund ya pauni milioni 120 kwa ajili ya kumsajili. ***(Sun)***

### SIRI ARTETA KUTUA ARSENAL

MIKEL Arteta ameamua kukubali kuwa kocha wa Arsenal baada ya kushindwa kuhakikishiwa na Manchester City kuwa mrithi wa Pep Guardiola atakapoondoka hapo kwenye dimba la Etihad. ***(Mirror)***

### SPURS YATUA FLAMENGO

KLABU ya Tottenham imefanya mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Flamengo, Gerson mwenye umri wa miaka 22 na inataka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kabla ya dirisha la Januari kufunguliwa. ***(90min)***

### KUMKOMALIA HAALAND

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema klabu hiyo ipo tayari kufanya mazungumzo na wakala Mino Raiola kwa ajili ya kutoa ofa kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 19, Erling Braut Haaland kutoka RB Salzburg. ***(Mirror)***

### CHELSEA KWA KINDA MNORWAY

CHELSEA imefikia makubaliano ya kumsajili kinda Bryan Fiabema mwenye umri wa miaka 16, kutoka Tromso na raia huyo wa Norway atakwenda kujiunga na akademi ya klabu hiyo. ***(Metro)***

### MERTENS AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Arsenal, Borussia Dortmund na Bayern Munich zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Dries Mertens mwenye umri wa miaka 32, akitokea Napoli kwa ada ya pauni milioni 8.5. ***(Calciomercato)***

### YAICHOKONOA FLAMENGO

KLABU ya West Ham ilituma maskauti wake kwenda nchini Qatar kumfuatilia mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Barbosa mwenye umri wa miaaka 23 na Bruno Henrique, 28, wote wakiwa wanaiwakilisha klabu ya Flamengo kwenye michuano ya Klabu Bingwa Dunia iliyomalizika juzi Jumamosi kwa Liver kutwaa ubingwa. ***(90min)***

### NYOTA BARCA AGOMBEWA EPL

KLABU za Manchester United, Everton na Southampton ni kati ya timu zilizoonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa Barcelona, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 19, kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 17. ***(Sport)***

### MILAN, ATLETICO KWA NEMANJA

TIMU za AC Milan na Atletico Madrid zinawania kumsajili kiungo wa Manchester United, raia wa Serbia, Nemanja Matic mwenye umri wa miaka 31. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### BEN ARFA LULU GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray imetoa ofa kwa Mfaransa, Hatem Ben Arfa mwenye umri wa miaka 32, baada ya mchezaji huyo wa zamani wa Newcastle kuondoka kipindi cha majira ya joto pale Rennes. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

# TENGA AMPONGEZA KARIA, TULIA NDANI, NYAMLANI SASA RASMI

**Na Somoe Ng'itu**

MWENYEKITI wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Leodegar Tenga, amempongeza Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, kwa kuhakikisha timu za Taifa zinashiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa katika siku za hivi karibuni.

**Tenga alitoa kauli hiyo jana, jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa anafahamu changamoto za kusafirisha timu, lakini kwa kipindi kifupi cha Karia, hali imekuwa tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.**

Kiongozi huyo alisema nchi kushiriki mashindano mbalimbali ni jambo la msingi kwa maendeleo ya mpira wa miguu na anaamini mafanikio yako karibu kwa timu za hapa nchini.

"Nawapongeza sana kwa kushiriki mashindano mbalimbali, kupata mafanikio ni jambo moja na kushiriki mashindano ni jambo lingine, hivyo ni lazima tujivunie kwa hali ilivyo sasa, huwa najiuliza wanakwendaje hawa, wanawezaje, maana najua shughuli yake ilivyo," alisema rais huyo wa zamani wa TFF.

Aliwataka wajumbe wa mkutano mkuu pia kuendeleza mipango ya maendeleo iliyopo ili kufikia malengo na kuweka pembeni tofauti "binafsi" zilizopo kwa sababu zitawarudisha nyuma.

"Utawala bora, uwazi na kufanya kazi kwa weledi, kutasaidia sana nchi yetu iendelee kupata misaada kutoka kwa wakubwa (Fifa na Caf)," alisema Tenga.

Katika mkutano huo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alipitishwa kuwa Mjumbe la Baraza la Wadhamini wa TFF akichukua nafasi iliyoachwa na marehemu Joel Bendera wakati Athumani Nyamlani naye alithibitishwa rasmi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa shirikisho hilo.

Nyamlani amechukua nafasi iliyoachwa na Michael Wambura, ambaye aliamua kustaafu nafasi zake zote za uongozi za mpira wa miguu, siku chache baada ya kutuhumiwa makosa mbalimbali.



Rapa Bora wa Cheza Kidansi 2019, Totoo Kalala, akikabidhiwa tuzo hiyo na Agnes Kiwaga (kulia) kutoka Baraza la Basata, jijini Mwanza usiku wa kuamkia jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# *Washiriki 12 waibuka kidedea cheza kidansi*

**Na Neema Emmauel,** MWANZA

KILELE cha Tuzo za Cheza Kidansi 2019 nchini Tanzania kimefikia tamati, huku washiriki 12 wakiibuka kidedea kwenye nyanja mbalimbali zilizokuwa zikishindaniwa katika kinyang'anyiro hicho ikiwamo cha msanii mwenye mchango mkubwa kwenye muziki wa dansi ambapo Diamond Platnum aliibuka mshindi.

Washindi kwa msimu huu wa kwanza walioibuka kidedea katika vipengele mbalimbali ikiwamo cha Rapa Bora akiwa ni Totoo Kalala, Mpigaji Bora wa Vyombo ikienda kwa Dekanto Bass, Mwanamziki Chipukizi, Kelly Haso akiibuka kidedea, wakati Mtayarishaji Bora akiwa ni Erasto Mashine.

Tuzo ya Mnenguaji Bora ilienda kwa Queen Suzy, Mtunzi Bora ikitua kwa Jimy Manzoka na Video Bora "Chozi Langu" ya Jimy Manzoka ikishinda.

Nafasi ya Mwanamziki Bora, Nyoshi El Saadat alishinda, Wimbo Bora ukiwa ni "Usiku wa Manane" kutoka Mjengoni Classic Bendi, Bendi Bora ikiwa ni Sky Melodies, wakati Tuzo ya Heshima akitunukiwa King Kikii na nafasi ya msanii mwenye mchango mkubwa kwenye muziki wa dansi ikichukuliwa na Diamond Platnum.

Akizungumza wakati wa utoaji tuzo hizo zilizotolewa juzi jijini Mwanza, Agnes Kiwanga kutoka Baraza la Sanaa Tanzania (Basata), aliwataka wasanii wa dansi kutokata tamaa kutokana na changamoto wanazozipitia bali wazitumie kuwa fursa itakayowapatia matunda na cha msingi kwao ni kufanya kazi zilizo bora za kisanaa zenye maadili kwa mwimbaji na mtazamaji ili waweze kupata tuzo za kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wake mratibu wa tuzo hizo, Bernard James, alisema wamejipanga kuchochea muziki wa dansi kutoka hapo ulipo kwenda hatua nyingine, hivyo ushirikiano ukiwapo watalifanikisha hilo kwa kuwa wameanza na ushindi wa kufanikisha hilo, hivyo wametambua, wamethamini na wanaunga mkono jitihada, juhudi na maarifa katika muziki wa dansi ili kuhakikisha unasonga mbele, lakini ushirikiano unahitajika katika kutekeleza adhima hiyo.

"Mashindano haya tulianzisha mwaka huu lengo likiwa ni kuinua na kuuthamini muziki wa dansi nchini unaokabiliwa na changamoto nyingi, hivyo uanzishwaji wa tuzo itakuwa chachu ya kuleta ushindani na mafanikio katika sekta hii," alisema James.

Pia aliwataka wasanii kujitokeza kwa wingi kumenyana kwenye mashindano hayo ambayo yatakuwa endelevu, hivyo waongeze ubunifu na kufanya utafiti kujua mashabiki wao wanataka nini ili kutoa kitu kilicho na ubora na kuchochea muziki kwenda mbele zaidi.

Wakizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo ya Rapa Bora, Totoo Kalala na Kelly Haso aliyejinyakulia tuzo ya mwanamziki chipukizi, walisema wanamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufanikisha hayo ambapo ushindi huo umeongeza chachu kwenye safari yao ya muziki kwa sababu vitu hivyo kwenye tasnia yao havikuwapo hivyo uanzishwaji wa tuzo zitaongeza ushindani katika kazi zao.

# Molinga aitishia Simba kwa bao FA

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuwa mmoja miongoni mwa wafungaji wa Yanga wakati ikishinda 4-0 dhidi ya Iringa United kwenye mechi ya kuwania Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu FA Cup, mshambuliaji David Molinga amesema ataendeleza ushindani wake pindi watakapokutana na Simba Januari 4, mwakani.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Molinga alisema bao alilolifunga ni salamu kwa wanachama wake pamoja na Simba.

"Mimi naahidi kujituma zaidi ili nizidi kuwapa furaha mashabiki wangu pamoja na uongozi wangu," alisema Molinga.

Aliomba mashabiki wake wazidi kumpa ushirikiano ili atimize malengo yake na kudai hakuna linaloshindikana.

Vilevile alisema anaahidi kuitumikia timu hiyo kwa moyo mmoja.

# Ngasa alia wazawa 'kubinywa' Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA wa Yanga, Mrisho Ngassa, ametuma ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram, ambao unaonyesha kilio cha wachezaji wazawa ndani ya klabu hiyo kutokupewa kipaumbele katika malipo kama ilivyo kwa wageni.

Aidha, inaelezwa kuwa Ngasa bado hajalipwa fedha zake za usajili ambazo zinatajwa kuwa ni Sh. milioni 15 za Kitanzania.



Katika ukurasa wake wa Instagramu, Ngasa ameandika: "Kiukweli mnavyotufanyia wazawa kwa kuwa mmetuzoea haya maisha daah? Mtu hajaumbwa kugoma wanatumia madhaifu yako kukuendesha, lakini mpira ni mchezo wa kuonekana uwanjani 'enjoy soccer' [furahia soka]. Pole mama yangu sina kitu, lakini utapona ngoja nirudi nyumbani nikupambanie mama yangu wewe ndio kioo changu."

Ngasa, ambaye amerejea katika ubora wake msimu huu, ametoa mchango mkubwa kwa klabu hiyo katika mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika kabla ya Yanga kutolewa na Pyramids FC ya Misri.

Mabingwa hao wa kihistoria Ligi Kuu Bara, watashuka dimbani kesho kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine kuivaa Mbeya City katika mwendelezo wa ligi hiyo msimu huu.

# Michezo

Jumatatu Desemba 23, 2019

Nipashe




Messi atupia la 50 kwa mwaka 2019

HABARI UK.30




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), katika harakati za kumiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Arusha FC, kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu FA Cup, uliochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana na Wekundu wa Msimbazi hao kushinda 6-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba hii ya Sven, Matola ya gharika

## ●●● Yaanza kwa kupiga mtu 6-0 Kombe la FA, wachezaji warejea katika kasi yao huku...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck na msaidizi wake, Selemani Matola wameanza vema kibarua chao cha kuinoa timu hiyo baada ya jana kuipa ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Arusha United kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu FA Cup iliyopigwa katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Vandenbroeck, aliyechukua nafasi ya raia mwenzake wa Ubelgiji, Patrick Aussems huku Matola akichukua nafasi ya Dennis Kitambi, waliweka rekodi ya kuivusha timu hiyo kwenye raundi ya tatu ya michuano ya Kombe la FA, tangu 2016 mwaka ambao timu hiyo ilitwaa kombe hilo, lakini baada ya hapo ikawa inaishia kwenye raundi hiyo ikicheza mechi moja tu na kutolewa.

Mwaka 2017, ilifungwa na Green Warrios kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya sare ya bao 1-1 kwa dakika 90 na mwaka jana, iliaga mashindano hayo kwa kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya Mashujaa ya Kigoma.

**Mashabiki wa Simba walilazimika kusubiri hadi dakika ya 18 kupata bao la kwanza lililofungwa na Clautus Chama, baada ya kuumalizia mpira uliotemwa na kipa, kufuatia shuti kali la Meddie Kagere.**

Mbrazil Gerson Fraga, alifunga bao lake la kwanza tangu ajiunge na klabu hiyo, alipokuta mpira unazagaa eneo la hatari, akaubetua mpira uliokwenda moja kwa moja hadi wavuni na kuandika bao la pili.

Dakika nne baadaye, Mkongomani Deo Kanda alifunga bao safi kwa mguu wa kushoto, baada ya krosi ndefu iliyopigwa na Shomari Kapombe.

Ibrahim Ajibu, alifunga bao la nne dakika ya 33, baada ya wachezaji wa Simba kugongeana mpira karibu na lango la Arusha United.

Kipindi cha pili, timu zote zilifanya mabadiliko, lakini walikuwa ni Simba tena walioweza kuandika mabao mengine mawili, yakifungwa na straika wao tegemeo, Kagere dakika ya 56, aliyeukuta mpira uliotemwa na kipa wa Arusha FC, kabla ya Fransis Kahata kufunga bao la sita dakika kumi baadaye akiunganisha krosi kutoka kwa Kanda.

Simba inayoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 25 baada ya kushuka dimbani mara 10 msimu huu, sasa inarejea kujiandaa na mechi ya ligi hiyo dhidi ya Lipuli United itakayopigwa Uwanja wa Uhuru keshokutwa, Jumatano.

Baada ya mechi hiyo, Simba itarudi tena katika uwanja huo kuikaribisha KMC FC siku tatu baadaye kabla ya kufunga mwaka na Ndanda FC, Desemba 31.

# Karia amulika bil. 20/- TFF

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, akiwataka wajumbe wa mkutano mkuu wa shirishiko hilo kudumisha umoja na ushirikiano, anataka kuona mapato yanaongezeka kutoka Sh. bilioni 13.9 hadi kufikia Sh. bilioni 20.

Karia alisema ongezeko hilo litakuwa ni la asilimia 80 na anahitaji kuona wanafikia malengo hayo ifikapo Desemba mwakani.

Rais huyo mpya wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), alisema ili malengo hayo yaweze kutimia, wadau wote wanatakiwa kuwa na ajenda moja ya kuendeleza mpira wa miguu nchini na si jambo lingine.

Karia alisema hayo jana wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa TFF uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Rais huyo aliwashukuru viongozi wenzake kwa kuhakikisha Tanzania imeanza kurejesha heshima yake katika soka la kimataifa na kutamba kufuzu fainali zilizopita za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) na fainali za Kombe la Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), haikuwa kazi rahisi.



Alisema anataka kuona viongozi wote wanaendelea kuweka nguvu katika masuala ya maendeleo na kuacha kufanya mambo yatakayowarudisha nyuma.

"Tunamshukuru Mungu, katika kipindi changu cha miaka miwili madarakani, tumeshinda makombe nane, nataka tuendelee kufanya vizuri zaidi, kama kuna mtu ana ajenda binafsi, aende kwingine," alisema Karia.

Aliongeza kuwa anahitaji kuona timu ya Taifa ( Taifa Stars) inafanya vema katika mashindano yake inayoshiriki na hatimaye kuwa kati ya timu bora 20 ifikapo mwaka 2022 wakati kwa upande wa wanawake (Twiga Stars), inakuwa katika 10 bora Afrika.

Alisema pia TFF inajipanga kuhakikisha timu zake za vijana za wanawake (U-17 na U-20), zinafuzu tiketi ya kushiriki fainali za Afrika zitakazofanyika baadaye mwakani.

"Tunataka kuwa na mchakato ambao utaongeza idadi kubwa ya wasichana wanaocheza mpira wa miguu hapa Tanzania kwa kufikia milioni moja ifikapo mwaka 2021," alisema Karia katika hotuba yake.

Aliongeza kuwa chini ya utawala wake anaamini mafanikio hupatikana kwa kufanya kazi kwa weledi, uaminifu, ushirikiano, uwazi na kuimarisha uhusiano.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >